Hii ni nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Nne - Tarehe 16 Juni, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza, ningependa kumtambua rasmi Kiongozi Mpya wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Wilfred M. Lwakatare, pamoja na Baraza lake la Wasemaji Wakuu kwa kila Wizara ya Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

## HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI**:

Taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2003/2004 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/2004.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 30

### Malipo ya Waliokuwa Wafanyakazi wa Shamba la Katani la Mnazi

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa wafanyakazi wa Shamba la Katani la Mnazi lililobinafsishwa bado wanadai mafao yao sawa na Sh. 52,000,000/=; na kwa kuwa mmiliki wa shamba hilo amekuwa akiuza zana mbalimbali bila kuwalipa haki zao na sasa amewakatisha tamaa kabisa kwa kuwadhalilisha na hata kuwatukana:-

(a) Je, baada ya ubinafsishaji, ni nani anayetakiwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wa eneo husika wanalipwa haki zao?

(b) Je, ni lini sasa wafanyakazi wa Shamba la Katani la Mnazi watalipwa mafao yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Shamba la Katani la Mnazi lilibinafsishwa mwezi Julai, 1997 kwa njia ya ufilisi na Mamlaka ya Mkonge kwa Kampuni ya *M/S. Le Marsha Enterprises Limited,* likiwa na ukubwa wa hekta 1,350. Shamba hilo lilibinafsishwa kwa lengo la kufufua na kuendeleza zao la Mkonge. Taarifa ya Kamati ya Serikali iliyotembelea shamba hilo mwezi Novemba, 2002 ilibainisha kuwa wafanyakazi waliokuwepo kabla ya ubinafsishaji walilipwa haki zao na Mamlaka ya Mkonge *(TSA)*. Kampuni ina wafanyakazi 73 wa kudumu na 120 wa muda. Hivyo, wafanyakazi waliochukuliwa katika shamba hilo walipaswa kulipwa na mwekezaji haki zao ikiwemo mafao yao.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mafao ya wafanyakazi wanaohusika yanasimamiwa na Bodi ya Mkonge na yanapaswa yalipwe na Kampuni kutokana na mauzo ya mkonge. Shamba hili lilibainishwa baada ya kufanyika kwa kikao kati ya wafanyakazi na Uongozi wa Wilaya mwaka 2002. Kutokana na kupatikana kwa Meneja mwenye uzoefu, aliyetafutwa na Bodi ya Mkonge, yapo matumaini ya kuongeza uzalishaji kwa kuwa tayari hekta 100 zimetayarishwa na upandaji unaendelea ambapo hadi Desemba, 2002 hekta 40 zilikuwa zimeshapandwa kwa kulinganisha na kipindi cha miaka mitatu iliyopita ambapo hakukuwa na mkonge uliopandwa. Ni matarajio yangu kuwa kwa utaratibu maalum ambao unasimamiwa na Bodi ya Mkonge, mafao ya wafanyakazi yatalipwa na mwekezaji kutokana na ongezeko la uzalishaji wa mkonge.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, lakini ukweli ni kwamba, wafanyakazi walio wengi pale na hasa vibarua walikuwa hawajalipwa haki zao mpaka majuzi nilipotoka nyumbani walikuwa bado hawajalipwa na kwa sababu Mheshimiwa Waziri tulimwomba pia akipata nafasi atembelee pale ashuhudie haya tunayoyasema.

Je, Waziri akipata kanafasi baada ya Bunge hili, ataamua kufika pale kwenye Shamba la Mnazi, ili awasikilize wale wafanyakazi mwenyewe na kupata ukweli kama haniamini?

La pili, kwa kuwa maendeleo ya mashamba ya mkonge na hasa yale ya Mkoa wa Tanga kwa kweli hayaendelezwi na wale ambao wamenunua, pamoja na Shamba hili la Mnazi, ni kweli kwamba huyu bwana anauza vifaa, alitaka kuuza hata *Corona,* wananchi wakaandamana pale. Je, watu wa namna hii, hivi ni vizuri bado waendelee kuachiwa mashamba hayo au wanaweza aakanyang'anywa, wakapewa watu wengine wenye uwezo wa kuyaendeleza? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba niko tayari kwenda Shamba la Mnazi kuwaona wafanyakazi hao, niongee nao na kujua hali halisi ilivyo. Lakini vile vile ningependa kumwarifu Mheshimiwa Kagonji kwamba, tayari tumekwishaanza taratibu za kuzungumza na Wanachama wa Bodi ya Shirika la Mkonge, ambao wengine ni Waheshimiwa Wabunge hapa katika kuendelea kumaliza tatizo lile.

Pili, nakubaliana na Mheshimiwa Kagonji kwamba, yapo baadhi ya mashamba hususan ya Katani, ambayo hayajaendelezwa katika Mkoa wa Tanga, hilo tunakubaliana nalo kabisa. Moja ya mashamba hayo ni yale yaliyochukuliwa na *Katani Limited*, ambayo sasa hivi Serikali karibu itafikia utaratibu wa *negotiations,* baada ya kutoka kwenye *depression* kati ya Katani na Serikali kuona ni maeneo yapi ambayo Katani wanaweza kuyamudu kwa uzuri zaidi na kuachia mashamba mengine.

Lakini vile vile sehemu zile ambazo mashamba haya hayaendeshwi, hasa yale yanayofuatiliwa na Bodi, uko utaratibu wa kuzungumza na hawa wawekezaji ambao wengi ni Watanzania, kuona ni jinsi gani tunaweza kuboresha utendaji kazi wa mashamba yale.

**Mfuko Maalum wa Ubinafsishaji**

**MHE. ABDULA S. LUTAVI** aliuliza:-

Kwa kuwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1997 iliunda Mfuko Maalum wa Ubinafsishaji *(Privatization Trust)* uliokusudiwa kuwa na uhai wa miaka mitano kwa kuanzia:-

(a) Je, Mfuko huo sasa una fedha kiasi gani?

(b) Je, ni kwa kiasi gani Mfuko huo umekidhi madhumuni yaliyokusudiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Abdula Lutavi, Mbunge wa Tandahimba, naomba nitoe maelezo ya ujumla kama ifuatavyo:-

Serikali ilianzisha Taasisi ya *Privatization Trust (PT)* chini ya Sheria Na. 7 ya mwaka 1997 ikiwa ni chombo cha kuweka utaratibu wa kuanzisha dhana ya uwekezaji wa pamoja *(Collective Investment)* na siyo Mfuko. Lengo la kuanzishwa kwa Taasisi hii ni kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kuchukua Hisa za Serikali toka baadhi ya Mashamba yanayobinafsishwa kwa lengo la kuwauzia wananchi;

(ii) Kuhamasisha ushiriki mpana wa wananchi katika kumiliki mashirika yanayobinafsishwa kwa njia ya ununuzi wa hisa;

(iii) Kuhakikisha kwamba hisa inazokabidhiwa *Privatization Trust* kisheria zinauzwa kwa wananchi kwa bei nafuu;

(iv) Kushirikiana na Asasi za fedha hapa nchini, kuanzisha vyombo vya uwekezaji wa pamoja yaani *Collective Investment Schemes (CIS),* kwa lengo la kuwashirikisha wawekezaji wadogo katika Soko la Mtaji na Dhamana.

Mheshimiwa Spika, Soko la Hisa pia hutumika kama njia mbadala ambapo wananchi huuziwa hisa wakati wa kuandikishwa makampuni yanayofanya vizuri kujiunga na Soko la Hisa la Dar es Salaam. Yamkini njia hii imekuwa ikinufaisha zaidi wananchi wenye vipato vizuri kuliko wale wenye vipato vidogo.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika hotuba ya sasa ya Bajeti ya Serikali, *PT* imemaliza muda wake jana tarehe 15 Juni, 2003. Aidha, chombo cha uwekezaji wa pamoja yaani *Unit Trust of Tanzania (UTT),* kimeanza kazi leo 16 Juni, 2003 baada ya taratibu zote kukamilika. *UTT* ambayo imeandikishwa chini ya Sheria ya *Trustees Ordinance* itasimamiwa na Mamlaka ya Masoko na Dhamana *(CMSA)*, kwa mujibu wa Sheria husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la msingi kama ifuatavyo:-

(i) Kwa maelezo yaliyotolewa hapo juu, *Privatization Trust* siyo Mfuko *(Fund),* ila ni Taasisi iliyoanzishwa kuchukua baadhi ya hisa za mashirika yanayobinafsishwa na yasiyohitaji wenye hisa wadogo kuchangia katika uwekezaji kwa madhumuni ya kuzihifadhi kwa ajili ya kuwauzia wananchi katika muda muafaka. Hivyo, *PT* ilikuwa na jukumu la kuhifadhi *(warehouse)* hisa na siyo fedha. Aidha, uendeshaji wa *PT* uligharamiwa na mapato yaliyotokana na ubinafsishaji chini ya *PSRC* na haikuwa na vyanzo vingine vya mapato.

(ii) *Privatization Trust* kwa miaka mitano ya uhai wake ilitoa hamasa na mafunzo kwa wananchi ikiwa ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, kuelezea dhana ya uwekezaji mdogo na kuweka utaratibu wa kuanzishwa kwa *Unit Trust of Tanzania (UTT)*. *UTT* itanadi hisa walizokabidhiwa na kuziuza kwa wananchi kwa viwango vidogo vidogo *(Units).* Mpaka sasa, Serikali imeshakabidhi asimilia 10 ya hisa

hizo, sawa na hisa za kiasi cha shilingi 23,942,277 katika Kampuni ya Bia *(TBL)* na asilimia 3.0 ya hisa zake, sawa na hisa milioni 5 katika Kampuni ya Sigara *(TCC)* kwa ajili ya kuwauzia wananchi. Aidha, *UTT* itatakiwa kubuni na kuanzisha *Investment Schemes* za aina mbalimbali ili ziuziwe wananchi na kuwekeza fedha na faida zitakazopatikana kwa uangalifu. Hii ni pamoja na kutekeleza majukumu ambayo hayakukamilishwa na *PT* kama nilivyoyaainisha katika maelezo yangu ya ujumla.

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, ingawa sijaridhika sana na tathmini ya Serikali kwamba Mfuko huu kweli umekidhi dhamira ya awali ya kuundwa kwake. Ningeomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Sasa pamoja na hisa hizi ambazo ziko kule kwenye Mfuko ule ambao umekufa na sasa unaanza Mfuko mwingine. Nini mpango wa Serikali wa hivi sasa kuhakikisha kwamba ile dhamira inayohamia kwenye *UTT* inakamilishwa katika muda mfupi ujao? *(Makofi)*

Swali la pili, nataka kuuliza kwamba, kwa nini sasa tunaambiwa kwamba zoezi zima la ubinafsishaji linafikia hatma na moja ya vyanzo vya hizi Amana au Hisa kwa ajili ya Mfuko huo ambao sasa unarithiwa na mwingine, ilikuwa kwenye hii *PSRC* ambayo karibu itakamilisha kazi yake. Mimi nataka kuuliza sasa Serikali inategemea kwamba mpaka itakapofikia hatma ya zoezi hili, *PSRC* itakuwa imechangia kiasi gani katika kuipa hii Taasisi mpya hizo Amana na fedha ambazo zinatakiwa kuendelea na kazi yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, leo *UTT officially* ndiyo inaanza kazi zake na kwa muda wote huo ilikuwa inajifunza kutoka nchi mbalimbali, namna ya kuuza hisa hizi kwa wananchi wenye vipato vidogo vidogo na kugawiwa kwa *units* ndogo ndogo, ina maana kwamba hisa moja ambayo pengine kwa mwananchi wa kawaida asingeweza kuinunua kwa bei yake ilivyo, zinakuwa zote zinanunuliwa kwa pamoja na wote kama wanachangia kwa pamoja na faida, gawio linalotoka watagawiwa wananchi kwa mujibu wa hisa walizozinunua.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, hii Taasisi itakuwa inaendelea na itaendelea kwa muda mrefu na itategemea vile vile wawekezaji wengine. Lakini *PSRC* siyo kwamba kila Shirika linalouzwa tu fedha zile zitakwenda katika *Unit Trust*, lazima kwanza hili Shirika lionekane kwamba lina faida, ndiyo zile hisa zinaweza kuuziwa wananchi wenye vipato vidogo vidogo siyo kwamba Shirika limeuza tu pale pale mkaanza kutoa hisa, itakuwa kama umekaa bila kupata gawio, inakuwa haina faida kwao. Lakini pale *PSRC* ikishathibitisha kwamba hili lina faida, hisa zake ndiyo zitanunuliwa na *Privatezation Trust* na *UTT* ili waweze kuwauzia wananchi.

Na. 32

**Kuweka Mabomba Mapya ya Maji - Mwika Kaskazini**
**Jimbo la Vunjo**

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa bomba la maji la *Mtiro Pipe Line* lililoko Kata ya Mwika Kaskazini, Jimbo la Vunjo, Mkoani Kilimanjaro lilijengwa mwaka 1958 na lilitumiwa na watu wachache sana ikilinganishwa na Sensa ya watu kwa mwaka wa 2002; na kwa kuwa kampuni ya *GTZ* na *KfW* za Kijerumani ziliwatangazia wananchi wa maeneo hayo kuwa wameleta Sh.3.3 bilioni mwaka 2001 kwa ajili ya kuweka mabomba makubwa na mapya ya kutosheleza mahitaji ya maji kwa watu wa sasa na vizazi vijavyo wa Wilaya ya Rombo na Kata ya Mwika; na kwa kuwa badala ya kulaza mabomba mapya, mabomba machakavu ya miaka 56 iliyopita yamewekwa mita za maji na kuwatoza wananchi gharama za maji kwa *flat rate* ya Sh.900 kwa mwezi na mwenye bomba nyumbani alitozwa Sh. 150/= kwa mwezi kwenye vilula chini ya *KILIWATER Co. Ltd.* yenye makao yake makuu Rombo:-

(a) Je, ahadi ya kuweka mabomba mapya kwa thamani ya Sh.bilioni 3.3 imeishia wapi?

(b) Je, fedha zilizokusanywa hadi sasa zaidi ya Sh.9.8 Milioni sawa na asilimia 10 kwa Mfuko wa Maji Kanda ya Mwika ni shilingi ngapi, zimewekwa kwenye benki gani, akaunti gani na Tawi lipi Mkoani Kilimanjaro?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni busara kulaza mabomba mapya kabla ya kuweka mita za maji na kuwagawia Tawi la Mwika bomba la maji na inchi tatu au nne (3" au 4") ili wajitegemee na kufungua akaunti yao ya maji kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Bunge hapo tarehe 20 Novemba, 2000?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** atajibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse J. Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli *GTZ* na *KfW* waliahidi kuweka mabomba mapya kwa thamani ya Sh.3.3 bilioni katika maeneo ya Wilaya ya Rombo na vijiji 13 eneo la Mwika. Hata hivyo, kutokana na wananchi wa maeneo hayo kutokuwa tayari kulipia, ilibidi zielekezwe sehemu nyingine za mradi ambako wananchi wameitikia wito wa kulipia na sehemu hizo ni maeneo ya Wilaya ya Rombo na ukarabati wa bomba kuu la maji la *East Kilimanjaro Trunck Main I.* Aidha, mfadhili amekubali kutoa fedha za awamu ya pili ambazo ni Sh.7.1 bilioni na eneo la Mwika Kaskazini linaweza kuingia katika awamu hii endapo tu wananchi, pamoja na Mheshimiwa Mbunge, watakubali kuchangia gharama. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, awahamasishe wananchi wa Mwika ili waweze kuchangia gharama kama wenzao kinyume na ilivyo hivi sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, asilimia 10 ya mapato ambayo Kampuni ya *KILIWATER* iliahidi kurudisha kwenye Mfuko wa Maji, ilikuwa itokane na malipo ya wananchi kwenye vilula. Kwa kuwa wananchi hawakulipia gharama kwenye vilula, Kampuni ya *KILIWATER* haikuwa na fedha za kuweka kwenye Mfuko wa Maji wa Kanda ya Mwika. Mapato ambayo yalipatikana katika Kanda ya Mwika yalitokana na malipo ya maji kwa mabomba ya nyumbani au vyanzo vingine na sio vilula.

(b) Mheshimiwa Spika, bomba la maji lililopo sasa katika Tawi la Mwika ni la nchi 4 ambalo huchukua asilimia 33 ya maji yote ya mradi. Maji haya ni zaidi ya matumizi ya watu wa Mwika. Aidha, ufungaji wa mita za maji ni sehemu ya ukarabati na udhibiti wa matumizi mabaya ya maji.

Mheshimiwa Spika, watu wa Mwika ambao pia ni wana hisa ndani ya Kampuni ya *KILIWATER* wanaweza kuwekewa tawi na *bulk meter* ili mradi tu wananchi na Mheshimiwa Mbunge, wakubaliane kwanza na mmiliki mkuu wa bomba kuu la maji, Kampuni ya *KILIWATER* kuhusu jinsi ya kulipia maji.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza sahihisho tu kwamba mimi naitwa Meja Jesse Makundi na siyo James Makundi kama ulivyotamka.

La pili, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Mifugo, kwa kuwa Kampuni hii ya *KILIWATER* kwa kipindi cha miaka 10 imekuwa na biashara ya maji na Kata za Mwika na Rombo na kuwa na mzozo kwa kipindi chote hicho na nilipoingia madarakani mwaka 2000 mpaka 2003 mwezi wa nne iliweza kukusanya shilingi milioni 9,898,313. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kuwa ni vizuri zaidi uchumi huu wa Mwika kurudishiwa *ten percent* ili waweze kutengeneza miundombinu ya mabomba hayo bila kuharibika? *(Makofi)*

Pili, kwa kuwa Kampuni ya *KILIWATER* iling'oa asilimia 95 ya vilula vyote vya Mwika na kufanya wananchi wahemee maji kila siku ya Mungu kwa masafa marefu, je hii Kampuni *KILIWATER* iko tayari kurudishia vilula hivi kama ilivyoagizwa na Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya nilipokuwa natembea naye katika vijiji hivyo na pia kusafisha matenki ambayo ni machafu kupindukia? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba radhi kwa kutamka, jina ambalo siyo lake.

Mheshimiwa Spika, makusanyo aliyoyasema ya shilingi milioni 9.8 zikirudishwa *ten percent* yake ni laki tisa na themanini elfu. Laki tisa na themanini elfu kwa kipindi cha karibu miaka saba ni hela ndogo sana ambayo naona aibu hata kusema kwamba inaweza kufanya matengenezo ya aina yoyote.

Vilula vilivyoondolewa kama Mheshimiwa Mbunge, anavyo-*claim* asilimia 95, viliondolewa baada ya wananchi wakiongozwa na Mheshimiwa Mbunge, kutokuwa na ari kubwa ya kulipia maji kama ilivyotakiwa. Kwa hiyo, ilibidi waondoe baadhi ya vilula ili viende sehemu ambako wananchi walikuwa tayari kulipia. Hivyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge na itakuwa ni ombi la nne. Ombi la kwanza *DC* amemwomba sana Mheshimiwa Mbunge. Pili, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa amemwomba sana Mheshimiwa Mbunge na tatu, nilipita mimi kule kwenye huo mradi pamoja na Ofisini kwake Mheshimiwa Mbunge kumwomba awahamasishe wananchi walipie maji ili kuweza kuuendeleza mradi huu ambao ni wa manufaa sana kwa wananchi wa Jimbo lake. *(Makofi)*

Na. 33

**Bwawa la Maji la Manchira**

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (k.n.y. MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Mji wa Mugumu Wilayani Serengeti Oktoba 2000 aliahidi kwamba Bwawa la Machira litachimbwa na kumalizika kabla ya mwaka 2005 kwa lengo la kuondoa kero ya maji kwa wakazi wa mji huo; na kwa kuwa mwezi Julai, 2001 Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo aliahidi kutekeleza ahadi hiyo ya Mhesihmiwa Rais lakini hadi sasa kazi ya uchimbaji wa Bwawa hilo bado haijaanza:-

(a) Je, ni lini kazi ya uchimbaji wa bwawa hilo itaanza na kukamilika?

(b) Je, ni fedha kiasi gani zilitengwa katika bajeti za miaka ya 2001/2002 na 2002/2003?

(c) Je, kazi ya uchimbaji wa bwawa hilo itagharimu fedha kiasi gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJINA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Bwawa la Manchira lililopo Mji wa Mugumu Wilaya ya Serengeti, lilianza kujengwa na Serikali miaka ya 1981/82. Baadaye fedha za kuendeleza ujenzi zilikosekana na hivyo kazi ya ujenzi wa bwawa ilisimama. Wakati huo msingi wa tuta ulikuwa umefikia asilimia 90 na sehemu ya utoro wa maji ilikuwa imechimbwa. Kazi ya uchimbaji wa bwawa itaanza katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 ikiwa kiasi cha shilingi milioni 200 zilizotengwa mwaka huu wa fedha wa 2003/2004 kwa ajili ya kuanza kazi zitatolewa. Kazi hiyo inakadiriwa kuchukua mwaka mmoja kama fedha za kugharamia ujenzi zitapatikana.

(b) Katika bajeti ya mwaka 2001/2002 mradi huu ulitengewa shilingi 37,889,000. Hata hivyo, kutokana na upasukaji wa Bwawa la Mwanyahina, Wilayani Meatu, fedha hizo zilitumika kukarabati bwawa hilo kama hatua ya dharura.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu (a) ya jibu langu, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa bwawa hilo la Manchira.

(c) Kwa ujumla kazi ya ujenzi wa Bwawa la Manchira inakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 1.2.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwawa hili zilishatengwa katika mwaka 2001/2002 na tena katika mwaka 2002/2003. Je, ni fedha ngapi ilitolewa na katika kila mwaka ilitumika kufanya nini?

Pili ni kwa nini katika ujenzi wa bwawa hili Serikali haikuwa makini kutumia fedha za Ba jeti kama zilivyotengwa fedha hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi fedha zilitengwa shilingi milioni 200 na katika ujenzi wowote fedha zinahitajika kwanza, kwa ajili ya *mobilization*. Pili, kama *down payment* kwa mkandarasi yeyote ambaye anaanza kazi ya ujenzi. Kwa hiyo, Wizara iliona haitakuwa busara kwa fedha zilizotolewa na Hazina shilingi milioni 200 wakati huo kuweza kutuwezesha kuanzisha ujenzi wakati huo.

Kwa hiyo, fedha hizo zimewekwa ili zitakapojumlishwa na fedha tulizoomba kwenye mwaka huu wa fedha wa 2003/2004, tutakuwa na kifungu ambacho tunaweza kulipa *down payment* kwa mkandarasi ambaye ataanza kazi ya ujenzi. Lakini *part of that money*, kifungu kilichotajwa katika jibu langu la msingi kilitolewa kwa ajili ya kufanya matengenezo ya dharura kwenye Bwawa la Manchira ambalo tayari lilikuwa limemalizika .

Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Mbunge, awe na subira kazi hiyo, tunaijua ni ya muhimu na pia tunafahamu kwamba, Mheshimiwa Rais, aliahidi bwawa hili litajengwa na tunaweza kuanza hii kazi mwaka huu wa fedha wa 2003/2004.

**MHE. TEMBE K. NYABURI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, Serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga jumla ya shilingi milioni 200 kukamilisha kazi hii na kama alivyosema bwawa litagharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.2; sasa kiasi kilichotengwa ni kidogo sana; je, sehemu ile inayobaki itatolewa na nani na itapatikana vipi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa bwawa hili hauwezi kumalizika katika kipindi kimoja cha mwaka wa fedha. Hivyo, kama nilivyoeleza kutokana na upatikanaji wa fedha kuwa ni md ogo na hatuwezi kuacha kuanza kazi ya ujenzi kwa sababu ya fedha ni kidogo.

Kwa hiyo, fedha tutakazopata ambazo Waheshimiwa Wabunge wataturuhusu kupitia Bunge lako Tukufu tupewe kwa ajili ya kazi hii, pamoja na fedha kidogo iliyobaki mwaka 2002/03, itatuwezesha kuanza hii kazi na nina hakika kwamba katika kipindi cha miaka miwili, mitatu, hili bwawa linaweza kumalizika kwa kupata fedha kidogo kidogo kila mwaka.

Na. 34

**Huduma ya Simu za *VODACOM***

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu sasa Kampuni ya Simu za Mkononi ya *VODACOM* imekuwa ikitoa huduma zake kwenye Jimbo la Siha; na kwa kuwa huduma hizo zimekuwa zikififia kadri wateja wanavyozidi kuongezeka na kuhamasika kununua simu za mkononi ili kupatiwa huduma hiyo:-

(a) Je, ni kitu gani kinachosababisha huduma hizo ziendelee kuwa duni na kutosikika vizuri katika Jimbo hilo?

(b) Je, mtambo wa kupokea mawasiliano uliopo katika Mji mdogo wa Sanya Juu upo kwenye hali gani?

(c) Je, Serikali inachukua hatua gani katika kuboresha huduma zinazotolewa na kampuni hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa hali ya kawaida huduma za *Vodacom* katika Jimbo la Siha ni nzuri hasa kwa sehemu zilizo ndani ya uwezo wa mtambo uliopo Sanya Juu. Kama kuna wateja wanaopata huduma duni, basi wateja hao watakuwa mbali sana kutoka kwenye mtambo au watakuwa kwenye sehemu za bondeni au sehemu zilizozibwa na miti mikubwa au zilizokingwa na vilima. Hata hivyo, *Vodacom* imeahidi kuchunguza malalamiko ya Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, mtambo uliopo Mji mdogo wa Sanya Juu upo kwenye hali nzuri. Kwa ufanisi na ubora wa mtambo huu pamoja na mingine nchi nzima mafundi huangalia muda wa saa 24 kwa njia ya mtandao wa kompyuta. Kukitokea matatizo yoyote huwa yanaonekana na hushughulikiwa mara moja.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Tume ya Mawasiliano Tanzania *(TCC),* inadhibiti masuala yote ya mawasiliano na kuhakikisha kwamba, utekelezaji huo unakwenda sambamba na utoaji wa huduma bora na wenye viwango vinavyokubalika. Aidha, Tume ya Mawasiliano ina jukumu la kuhimiza usambazaji wote wa huduma za simu Mijini na Vijijini ikiwa ni pamoja na zile za *Vodacom.*

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, naomba nishukuru kwa majibu mazuri ambayo yametolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpaka jana jioni nilikuwa naendelea kuwasiliana na Jimbo langu la Siha na nilikuwa najaribu ku-*test* kwa sababu nilijua leo nitapata majibu hapa Bungeni na inaonekana bado ni sogea, kaa pembeni kidogo au kaa hapo hapo ili niweze kukusikia; je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya Kikao cha Bunge hili tuondoke mimi na yeye ili twende katika Jimbo langu la Siha, pamoja na wataalam wa *Vodacom* ili twende tukathibitishe hiyo hali ambayo nimeisema kwamba inajitokeza katika Jimbo langu la Siha? Nashukuru. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, inawezekana wakati wanawasiliana huwa wako nje ya eneo au ule umbali ambao nimeuzungumza au wako mahali penye *black spot* ndiyo maana anakwambia sogea huku au simama hapo hapo ulipo ndiyo utanipata. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, wataalam wa *Vodacom* watakwenda na mimi nampa ahadi kwamba nitatembelea Jimbo lake. *(Makofi)*

Na. 35

**Ujenzi wa Gati - Mafia**

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH** aliuliza:-

Kwa kuwa ni lengo la Serikali kujiondoa kwenye biashara na kubakia na jukumu la ukusanyaji kodi; na kwa kuwa ni katika msingi huo Serikali imeamua kukodisha/kubinafsisha mashirika na makampuni mbalimbali yaliyokuwa yanamilikiwa na Serikali hapa nchini; na kwa kuwa Hoteli ya Kitalii ya *Mafia Island Lodge* iliyopo katika Wilaya ya Mafia imeshapata mwekezaji, ambaye anategemea wakati wowote kulipa fedha kwa Serikali ili aweze kukabidhiwa hoteli hiyo; na kwa kuwa katika Bajeti ya Serikali ya mwaka 2002/2003 Serikali ilitenga shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Ujenzi wa Gati la Mafia kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania, lakini gharama halisi kwa ujenzi huo ni shilingi bilioni nne:-

(a) Je, kwa nini Serikali isizitoe fedha atakazolipa mwekezaji huyo kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania kwa lengo la kuongeza mtaji walionao ili wakamilishe ujenzi wa Gati hilo?

(b) Kwa kuwa gharama halisi ya ujenzi wa Gati hilo ni shilingi bilioni nne na tayari Serikali imeshatenga shilingi bilioni mbili; je, Serikali inaendeleaje na jitihada zake za kutafuta shilingi bilioni mbili zilizobakia ili ujenzi huo uanze?

(c) Je, ni nini mipango ya Serikali ya kuimarisha kukamilisha miundombinu ya Gati, Uwanja wa Ndege na simu za *digital?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mbunge wa Mafia, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Serikali imebuni mipango mingi ya kuendeleza Kisiwa cha Mafia. Kwa upande wa bandari ndogo ya Mafia, Serikali imekuwa na mpango wa kujenga Gati tangu mwaka 1977. Hata hivyo, ukosefu wa fedha umekuwa ndiyo kikwazo kikubwa. Tafiti mbalimbali zimefanywa na ya mwisho ilifanywa mwaka 1993 na *Howard Humphrey's Cooper and Lybrand Associates* na kupendekeza ujenzi wa Gati katika maeneo ya Kilindoni. Gharama za ujenzi kwa sasa inakisiwa kuwa shilingi bilioni 3.5

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdulkarim E. H. Shah, Mbunge wa Mafia, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekubali pendekezo la kujenga Gati sehemu ya Kilindoni kwa gharama ya shilingi bilioni 3.5. Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Bandari Tanzania, tayari imeshatenga kiasi cha shilingi bilioni 1.96, ambazo ni asilimia 56 ya fedha zinazohitajika. Jitihada mbalimbali za kupata kiasi kilichosalia zinaendelea. Ni matumaini yetu kwamba, kiasi kilichosalia kitapatikana na kuwezesha mradi kutekelezwa. Inatarajiwa kwamba usanifu utakamilika katika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uwanja wa ndege, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, imekwishafanya usanifu kwa kuitumia Kampuni ya *M-Consult* ya Tanzania, kwa kushirikiana na Kampuni ya Usanifu ya Kimataifa ya *Scott Wilson Kirpatrick* ya Uingereza kwa gharama ya shilingi milioni 34.7. Sambamba na hatua hiyo, Wizara yangu imekuwa ikitafuta wafadhili mbalimbali wa kukamilisha mradi huo kwa kuwa gharama ya ujenzi ni kubwa. Aidha, tumeomba mkopo wa riba wa Sh. 6.6 bilioni kwenye Benki ya Ulaya *(European Investment Bank)* na bado tunasubiri majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa simu za *digital,* Kampuni ya Simu Tanzania katika awamu ya kwanza ya mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2003, imepanga kuweka *Digital Microwave Link* kuanzia Dar es Salaam hadi Mtwara na mchepuo kwenda Mafia. Zabuni za mradi huu zimeshasambazwa

kwa wakandarasi mbalimbali. Mradi huu unategemewa kukamilika na kuanza kazi ifikapo mwishoni mwa mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, kwa juhudi zake za karibu sana katika kutafuta maendeleo ya Jimbo lake. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa Gati ya Mafia ni kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa kubwa kama ya *Santolin*; je, Serikali inaweza kulieleza nini Bunge na wananchi kwani meli hiyo ya *Santolin* ambayo ilizinduliwa kwa mbwembwe kubwa sana hivi imesitisha safari zake za kwenda Mafia, Mtwara na Mikoa yote ya Kusini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ingawa swali la msingi halihusiani na *Santolin* lakini naomba nichukue nafasi hii nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, *Santolin* imeanza kazi na shughuli hizi zinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, masuala ya *Santolin* ni mazito na ni makubwa yanahitaji muda kuyaelezea. Nitapenda kumwomba Mheshimiwa Mbunge, tukutane ili nimwelezee kwa kirefu kabisa, la sivyo nitapoteza muda mrefu sana hapa. *(Makofi)*

Na. 36

**Soko Huria kwa Mazao ya Kilimo - *East African***

**MHE. THOMAS NGAWAIYA** aliuliza:-

Kwa kuwa tumekubali soko huru kwa bidhaa mbalimbali Afrika Mashariki; na kwa kuwa bidhaa tulizonazo hapa Tanzania zimetokana na kilimo kama vile karafuu, kahawa, pamba, korosho na kadhalika; na kwa kuwa mkulima anahitaji kuuza mazao yake kwa bei nzuri ili aweze kupata faida na kuondokana na umaskini:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali inawazuia wakulima wa mazao niliyoyataja kuuza mazao hayo nchi jirani za Afrika Mashariki?

(b) Je, kwa kufanya hivyo, Serikali haioni kwamba inarudisha nyuma maendeleo ya kiuchumi kwa wakulima na Taifa kwa ujumla?

(c) Je, Serikali kuwazuia wakulima wa karafuu, Pemba na wa kahawa wa Tanzania kuuza bidhaa hizo kwenye nchi jirani za Afrika ya Mashariki, haioni kwamba inakwenda kinyume na matakwa ya soko huria?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipoamua kufuata Sera ya Soko Huru, mazao ya chakula ndiyo yaliyotangulia kuuzwa katika soko huru miaka ya 1980. Mazao ya biashara yakiwemo pamba, korosho, kahawa na kadhalika, yalifuatia na kuanza kuuzwa kufuata mfumo wa soko huru mapema miaka ya 1990. Tangu wakati huo, mazao yote ya kilimo yakiwemo ya chakula na biashara yananunuliwa na kuuzwa na wafanyabiashara binafsi, vikiwemo Vyama vya Ushirika. Jukumu la Serikali kupitia Bodi za Mazao ni kutunza na kusimamia kanuni na taratibu za ununuzi na uuzaji wa mazao hayo ili kulinda ubora na sifa ya mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijijini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika maelezo yangu mafupi ya awali, wanunuzi binafsi wa mazao ya kilimo kutoka ndani na nje ya nchi, wakiwemo wafanyabiashara kutoka nchi jirani za Afrika Mashariki, wanaruhusiwa kununua mazao hayo katika mfumo wa soko huria. Hata hivyo, wanunuzi hao wanatakiwa kufuata kanuni, taratibu na Sheria za kununua mazao kwa madhumuni niliyoyataja hapo juu, yaani kulinda ubora na sifa za mazao kutoka Tanzania. Kwa mfano, mnunuzi kutoka nchi jirani ya Afrika Mashariki, anaruhusiwa kununua kiasi chochote cha kahawa kutoka kwenye mnada wa kuuzia kahawa ulioko Moshi, baada ya kutimiza masharti yanayotakiwa ambayo ni pamoja na kupata leseni ya kununua kahawa. Utaratibu huu unatumika katika nchi zote za Afrika Mashariki kwa uuzaji wa mazao makuu ya biashara yanayozalishwa na nchi hizo hadi hapo utakapowekwa utaratibu mwingine utakaokubaliwa na nchi zote tatu zilizo Wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napenda nisisitize kuwa utaratibu unaotumika sasa hauna budi utumike katika mazao mengine yote ili kuzuia wafanyabiashara wasiozingatia ubora wa mazao na hatimaye kuharibu sifa ya mazao yetu katika masoko ya nje, kitu kinachopelekea kushuka kwa bei za mazao hayo na hivyo kuendelea kufanya wakulima wetu kushindwa kuondokana na umaskini.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mpaka sasa tumepiga marufuku kuuza mahindi nje, kwa mfano, Zambia na kwingineko; na kwa kuwa kuna kitengo cha kununua chakula *(SGR)* ambacho kina uwezo wa kuhifadhi mazao na wale wananchi wanaoambiwa wakae na mazao yao hawana uwezo wa kuhifadhi na mpaka sasa tumenunua tani elfu hamsini na tatu; je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kuwaruhusu hawa wananchi wauze ili waweze kupata fedha na kuondokana na umaskini badala ya kuwaambia watunze chakula wakati wao hawana maghala ya kutunzia?

Mheshimiwa Spika, pili, iwapo tunanunua bidhaa nyingi kutoka Kenya kama vile mafuta ya kupikia na hata maziwa na wananyonya fedha zetu ya Tanzania; je, Serikali haioni sasa ni vizuri kuturuhusu tuuze huko Kenya bidhaa zetu ili na sisi tuweze kunyonya fedha zao kwa sababu wao hawana nafaka nyingi kama vyakula? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyokuwa nimesema ni kwamba, Serikali haijapiga marufuku uuzaji wa mazao ya chakula hasa hayo mahindi anayoyasema Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, kinachofanyika ni kuweka utaratibu tu wa kuhakikisha kwamba, hatuuzi mahindi yote ili kuhifadhi chakula chetu cha hapa ndani. Kwa hiyo, endapo Serikali kwa utaratibu ule wa kusimamia na kudhibiti upatikanaji wa chakula nchini, ikiridhika kwamba tutakuwa na chakula cha kutosha nchini, hakuna kizuizi chochote ambacho kinaweza kikawekwa kwa mwananchi ambaye ana mazao yake ya ziada ambayo anaweza kuyauza nchi za nje au nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, pili, kama nilivyokuwa nimeeleza katika kujibu swali la msingi ni kwamba, biashara katika nchi za Afrika Mashariki imewekewa utaratibu ambapo kutakuwa na uhuru wa kuuziana bidhaa zetu katika nchi zote za Afrika Mashariki, ikiwemo na sisi wenyewe kuuza katika nchi za wenzetu Kenya na Uganda.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, bei ya mazao ya *SGR* haiwapi moyo wakulima kuiuzia Serikali mazao yao; je, Serikali itakuwa tayari angalau kuweka bei nzuri kuliko ya walanguzi ili ipate mazao ya kutosha katika mfuko huu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, bei ambayo inatumiwa na Serikali ukilinganisha na ile ya walanguzi, kwa vyovyote vile walanguzi wanaweka bei ambayo ni

kubwa zaidi ya kuweza kuvutia ili waweze kupata hayo mahindi, wakati mwingine kusema kweli bei hizi ambazo zinawekwa na walanguzi, ni wale wanunuzi ambao wanapita katika njia ambazo si rasmi. Lakini kwa vyovyote vile kama ambavyo taratibu zimewekwa kwa kupitia katika masoko rasmi, bei zinazotakiwa zitumike ni hizo hizo ambazo zitakuwa zimezingatiwa na Serikali na kuzingatia vigezo vyote vya gharama za uzalishaji wa mazao hayo kwa mkulima.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Nilipenda niongezee mambo mawili madogo kwenye majibu ya nyongeza ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni suala la ulanguzi. Nadhani hawa mnaotaka kuwaita walanguzi wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana, hao ni wafanyabiashara wa mazao. Kwa hiyo, nilikuwa nataka kusema kwamba, tusiendelee kuwaita walanguzi kwa sababu wanafanya biashara za mazao na ndiyo maana katika siku za karibuni kumekuwa na ongezeko la bei kwa sababu hao wafanyabiashara wamekuwa wakitoa mazao katika sehemu za uzalishaji ili kupeleka katika sehemu za masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, ni suala la *SGR*, *SGR* si chombo cha biashara, tangu kilipoundwa lengo lake si kufanya biashara na wakati kilipoundwa tulielezwa wazi kabisa kwamba, wafanyabiashara watanunua mazao na pale ambapo sasa mazao hayakuweza kununuliwa ndipo *SGR* itakapoingia. Kwa hiyo, kwa kweli *SGR* si chombo cha biashara ila ni Chombo cha Hifadhi ya Chakula cha Taifa. Kama *SGR* itanunua kwa bei kubwa sana, ni kweli mkulima atapata faida, lakini yule ambaye anatarajiwa kununua yale mazao ambapo lengo la Serikali ni kupeleka yale mazao kwa wale ambao wana shida kabisa na wao watakwama kabisa kuyanunua yale mazao. Nilitaka kutoa ufafanuzi huo. *(Makofi)*

Na. 37

**Wanunuzi wa Zao la Kahawa**

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya Serikali kuruhusu soko huria la mazao ya wakulima, wanunuzi binafsi wa zao la kahawa waliweza kuwa na leseni zaidi ya moja ya biashara ya kahawa yaani kununua kwa wakulima na kuinunua tena kahawa yao wenyewe mnadani kwa bei ile ile waliyonunulia kutoka kwa wakulima kwa lengo la kulipa kodi na ushuru mbalimbali; na kwa kuwa utaratibu huu wa mnunuzi kuwa na leseni zaidi ya moja sasa umesitishwa na hivyo mnunuzi kuruhusiwa kuwa na aina moja tu ya leseni ikizingatiwa kwamba gharama za kusafirisha kahawa kutoka Mbinga hadi mnadani ni kubwa:-

(a) Je, ipo mantiki gani ya kuendeleza ukiritimba wa kupeleka kahawa ya Mbinga kwenye mnada wa Moshi badala ya mnada kufanyika Mbinga ambako uzalishaji wa kahawa aina ya Arabika ni mkubwa kuliko ule wa Kilimanjaro?

(b) Kwa kuwa zao la kahawa lina makato mengi yanayomsababishia mkulima kupata malipo kidogo kuliko gharama za kuhudumia zao lenyewe; je, Serikali ipo tayari kupunguza au kuondoa kabisa kodi na makato mengine ili kutoa nafasi na muda wa kutosha wa kufufua zao hilo?

(c) Je, Serikali ipo tayari kuruhusu mkulima mmoja mmoja, vikundi au vyama vya msingi vya ushirika kuuza kahawa yao nje bila kupitia Bodi ya Kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mbunge wa Mbinga Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mnada wa kahawa unaofanyika Moshi siyo ukiritimba bali ni moja ya jitihada za Serikali katika kuendeleza soko la zao la kahawa na kuhakikisha kuwa soko hilo linakuwa la ushindani na wakulima wanapata faida kutokana na zao lao. Mnada huo unapofanyika Moshi hukutanisha wanunuzi wengi na hivyo kuleta ushindani zaidi kama ilivyokusudiwa. Aidha, mahali ambapo mnada huo

hufanyika hivi sasa tayari kumewekwa miundombinu ambayo inawezesha kuendesha shughuli za mnada kwa ufanisi zaidi. Miundombinu hiyo ni pamoja na *Electronic Auction Machine* na vifaa vya kukaanga na kuonjea ubora wa kahawa yaani *liquoring facilities*. Vile vile ni rahisi zaidi kwa wanunuzi kufika katika mnada wa Moshi hasa kwa wale wanaotoka moja kwa moja nchi za nje kwa sababu ya kuwepo kwa njia rahisi za usafiri, pamoja na miundombinu mingine.

Hata hivyo, kahawa inayozalishwa Mbinga husafirishwa hadi Makambako ambako huhifadhiwa na sampuli za kahawa hiyo ndizo hupelekwa mnadani Moshi, ambako wanunuzi hununua kahawa hiyo kama kahawa iliyopo Makambako *(Ex-Makambako)* na hivyo hivyo kahawa kutoka Kagera hunadiwa kama kahawa iliyohifadhiwa katika Bandari ya Kemondo *(Ex-Kemondo)*. Kwa utaratibu huu, uuzaji wa kahawa katika mnada wa Moshi hauhitaji kusafirisha kahawa yote hadi mnadani.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imekwishaanza kutekeleza dhamira yake ya kupunguza au kuondoa kabisa kodi na makato mengine ambayo ni kero kwa wananchi ili kutoa nafasi na muda wa kutosha wa kufufua mazao ya kilimo, likiwemo zao la kahawa. Katika kutekeleza azma hii, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tayari ilikwishatoa mwongozo wa uwianishaji na ufutaji wa kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Serikali za Mitaa ambao umegundulika kuwa hauleti tija kwa wananchi. Kwa mfano, kutokana na mwongozo huo Serikali imeagiza kuwa makato yote ya ushuru unaotozwa na Halmashauri katika mazao yasizidi asilimia tano ya bei anayolipwa mkulima. Pamoja na hatua hiyo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, kama ilivyotangazwa kwenye hotuba ya Bajeti, imekwishachukua uamuzi wa kuondoa kodi zote na ushuru ambao unaleta kero kwa wananchi kuanzia msimu wa mwaka wa fedha wa 2003/2004 ikiwemo kodi na ushuru unaohusiana na mazao ya kilimo.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaandaa kanuni na taratibu ambazo zitawezesha mkulima, kikundi au Chama cha Ushirika cha Msingi, kuuza kahawa yenye ubora wa hali ya juu *(Specialty Coffee)*, kwa utaratibu maalum. Ili kuhakiki ubora wa kahawa itakayouzwa katika utaratibu huu, Bodi ya Kahawa imeandaa vigezo ambavyo lazima vitimizwe na mkulima, kikundi au Chama cha Ushirika husika. Baada ya kutimiza vigezo hivyo, mkulima, kikundi au Chama cha Msingi watapewa Hati ya Uthibitisho *(Certificate)* kabla kahawa hiyo kuuzwa kwa utaratibu maalum. Aidha, kutakuwa na mkataba kati ya mnunuzi na muuzaji utakaosimamiwa na Bodi ya Kahawa utakaohakikisha kwamba muuzaji anapata bei nzuri zaidi ambayo inalingana na ubora wa hali ya juu wa kahawa itakayouzwa.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Bodi ya Kahawa ipo pale kwa ajili ya kusimamia na siyo kuendesha shughuli za kiutendaji kama vile kutoa leseni, kujiingiza moja kwa moja kwenye mnada, wakati mwingine pamoja na kutoa leseni hata kwa Wajumbe wa Bodi; je, Sheria iliyopitishwa katika Bunge hili tena kwa mbinde itaanza kutekelezwa lini ili kuweka ufanisi zaidi katika suala la biashara ya kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Ngwatura, katika kuuliza swali hili ni kwamba, Bodi ya Kahawa kusema kweli iko pale kwa ajili ya kusimamia taratibu na Sheria na ndiyo maana hiyo Sheria ambayo anaiulizia kwamba itaanza kutumika lini, itatungwa ili kuhakikisha kwamba kazi ya Bodi ya Kahawa ni kusimamia hizo taratibu ambazo zimewekwa. Kwa hiyo, katika kutekeleza wajibu wake suala la kutoa leseni ni sehemu ya usimamizi wa taratibu.

Mheshimiwa Spika, Sheria hii itaanza kutumika mara tu taratibu zitakapokuwa zimekamilika Sheria itaanza kutumika ili Bodi ya Kahawa iweze kusimamia kazi zake kama ilivyokuwa imekusudiwa.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kutokana na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba ameeleza vizuri kuhusu kuondolewa kwa *VAT* kwenye mazao kama ya kahawa lakini bado wakulima hao hao huwa na migogoro

wanapokuwa wamebeba mazao yao kwenye mabehewa ya *TRC* ambapo *TRC* hulipa *VAT;* je, kutokana na maelezo hayo, yuko tayari wale wakulima watakaokuwa wamebeba mazao yao hayo, endapo itakuwa imetambulika kwamba yamebebwa kwenye mabehewa, yale mabehewa yasiwe *charged VAT* ili kuwasaidia hawa wakulima; je, hilo linaweza likajibika? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Sijui kama Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ushirika na Masoko, anaweza kujibu hilo, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha anaweza. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza kwenye hotuba yangu ya Bajeti na vile vile kwenye hotuba ya mwaka 2002/03 kwamba, wakulima wanaotaka kusamehewa *VAT* ni lazima wajiunge na chombo fulani, *Association* ya wakulima au Chama cha Msingi, kwa sababu mkulima mmoja mmoja hawezi kuandikishwa kama ni mlipa kodi ya *VAT*, ni lazima awe kwenye chombo ambacho kimeandikishwa rasmi na *TRA* kwamba wanaweza wakasamehewa *VAT* hiyo. Kwa hiyo, mkulima asiyekuwa na chombo, Chama cha Ushirika, Kampuni fulani au *Association*, hawezi kusamehewa *VAT* hiyo.

Na. 38

**Sheria ya Uzururaji kwa Mkoa wa Dar es Salaam**

**MHE. PETER KABISA** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania inakubali na kuheshimu haki za binadamu ukiwemo uhuru wa kwenda mahali popote na saa yoyote ili mradi mtu havunji Sheria za nchi; na kwa kuwa baadhi ya Askari Polisi walio wahalifu wa Mkoa wa Dar es Salaam huitumia vibaya Sheria ya Uzururaji kwa kuwakamata vijana saa za jioni bila kosa lolote na wakati mwingine *operation* kamata kamata hufanywa nyakati za usiku ambapo Askari Polisi hao huwasingizia vijana hao watuhumiwa wa makosa ya jinai:-

(a) Kwa vile kuna tatizo la Kitaifa la ukosefu wa ajira kwa vijana wetu; je, Serikali haioni kwamba Sheria hiyo ya Uzururaji kama ilivyo hivi sasa imepitwa na wakati na inatumiwa vibaya na Askari Polisi wahalifu?

(b) Kwa kuwa Sheria hiyo ni ya udhalilishaji na uonevu kwa kumnyima mwananchi uhuru na haki zake za Kikatiba; na kwa vile kamata kamata hiyo ni haramu kwa vile hali ya kutotembea usiku haipo na wala haijatangazwa na Serikali; je, ni kwa nini Sheria hiyo haifutwi?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Peter Kabisa, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Peter Kabisa kwamba, Sheria na Kanuni za Adhabu inayokataza vitendo vya ukahaba, kucheza kamari za karata tatu, pata potea na kadhalika na kuzuia tabia ya uzembe na uzururaji, kamwe havikiuki ibara ya 17 ya Katiba inayomruhusu kila mtu kwenda atakako kwa sababu ibara hiyo hiyo, inahalalisha Sheria zozote zinazotungwa kwa ajili ya kuwalazimisha wananchi kutimiza wajibu wao au kulinda manufaa ya umma au kuhifadhi maslahi mahsusi au ya sehemu fulani ya umma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Peter Kabisa, atakumbuka kwamba, Sheria hii ilipotungwa, Serikali ilifanya jitihada za makusudi kuwapa wananchi mashamba na msaada wa kuanzisha mashamba yao. Hivyo, naamini Mheshimiwa Peter Kabisa, atakubaliana na mimi kwamba, hiyo Sheria iliyotajwa haijapitwa na wakati kwa sababu inalinda maslahi ya jamii yetu dhidi ya vitendo vya watu wazembe na wale wanaojihusisha na vitendo ambavyo havifanani na maadili mema ya jamii yetu. Lakini vile vile nakubaliana na Mheshimiwa Peter Kabisa kwamba, Sheria hii inahitaji kutekelezwa na Polisi kwa uangalifu ili kuepuka kuwabughudhi wananchi waadilifu. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, Sheria hii ilitungwa kwa madhumuni ya kuhakikisha kila Mtanzania anaishi kwa amani, utulivu na kuheshimiana na kuwaondolea hofu wananchi waadilifu na sio kuwaendekeza watu wazembe, wasiotaka kujituma kufanya kazi. Sheria ya namna hii haiwezi kupitwa na wakati.

**MHE. PETER KABISA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anaelewa kwamba kwa mpangilio wa sasa hivi wa kuwakamata vijana kwenye majumba yao unakiuka utaratibu mzima wa haki za binadamu; lakini pia Serikali ya Tanzania haija-*declare confine* kwa maana kwamba watoto wawe wamelala saa 12.00 au saa 2.00. Kwa hiyo, ni kusema kwamba kuna haja ya ku-*revisit* Sheria hii, tuondokane nayo ili kuhakikisha kwamba ule uhuru wa mwananchi uko pale pale lakini akivunja Sheria basi atadhibitiwa kwa maana hiyo lakini kwa kweli Sheria hii inatakiwa iondolewe moja kwa moja? Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tunayo haya matatizo na matatizo haya yametokana na hali ya kiuchumi, kwa miaka mingi tumekuwa katika *reform programs* mbalimbali, ubinafsishaji, kulegeza masharti ya kiuchumi na kwa kiwango fulani hii imeleta ajira kupotea na hivyo vijana kutokuwa na ajira na hivyo kutembeatembea. Kwa hiyo, nakubaliana na hoja yake lakini tukumbuke pia tunayo matatizo ya ujambazi hasa katika mji wetu wa Dar es Salaam na wageni ambao ni majambazi. Lakini pia nasema inabidi tutazame hizi sheria kuona kwamba zinalingana na hali ilivyo kwa wakati huu maana sheria isije kuwa ina-*frustrate interest of the people.* Ni lazima tuyatazame haya. Sheria lazima iwe na *common sense.* Mathalani juzi kulikuwa na tetemeko hapa sasa huwezi ukatunga sheria ukasema kwamba, kila mtu alale na pajama kuhofia kwamba watu wanaweza kukimbia uchi asubuhi. *(Kicheko)*

Na. 39

**Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo**

**MHE. ARIDI M. ULEDI** aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Nanyumbu linakabiliwa na tatizo la uhaba wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo; na kwa kuwa Jimbo hilo lina eneo kubwa sana kumfanya Hakimu mmoja aliyepo kukabiliana na kazi nyingi hivyo kesi kuchelewa kusikilizwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika Jimbo la Nanyumbu?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuirudisha Mahakama ya Mwanzo kwenye Kata ya Nanyumbu ili wananchi waweze kupatiwa huduma hapo kuliko ilivyo sasa?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aridi M. Uledi, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo haulikabili Jimbo la Nanyumbu pekee bali ni tatizo linalozikabili Mahakama nyingi za Mwanzo nchi nzima. Tunazo Mahakama za Mwanzo 1,277 wakati Mahakimu waliopo ni 630 tu. Hivyo, upungufu ni mkubwa. Hivi karibuni tumepata kibali cha kuajiri Mahakimu 74 wa Mahakama za Mwanzo na tayari usaili wa walioomba nafasi hizo umefanyika. Wale watakaoajiriwa, watasambazwa kwenye vituo mbalimbali nchini kwa kuzingatia Wilaya ambazo zina uhaba mkubwa zaidi wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

(b) Mahakama ya Mwanzo ya Nanyumbu haijafungwa. Inaendelea kufanya kazi kama kituo cha kutembelewa na Hakimu kutokea Mahakama ya Mwanzo Mangaka. Hivyo, hadi sasa wananchi wa Nanyumbu wanaendelea kupatiwa huduma hapo hapo.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Michiga alihamishiwa Masasi Mjini mwanzoni mwa mwaka 2002 na kwa kuwa Hakimu pekee aliyeko Mangaka ndiye anayelazimika kutembelea Mahakama ya Michiga kusikiliza kesi ambazo zimerundikana huko. Je, ni lini basi Serikali itapeleka Hakimu Michiga?

(b) Kwa wakati huu ambapo Hakimu aliyeko Mangaka ndiye anayewajibika kutembelea Mahakama ya Michiga na kusikiliza kesi na kwa sababu kutoka Mangaka kwenda Michiga ni masafa marefu ni jinsi gani basi Hakimu huyo anafidiwa kwa usumbufu ambao anaupata? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, tunalo tatizo kubwa la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo lakini jitihada zinafanywa kwa kuwasiliana na Idara ya Utumishi ili tuweze kuendelea kupata vibali na kuongeza idadi ya Mahakimu hapa nchini. Aidha, juhudi zinafanywa kuweza kukipanua Chuo chetu cha Lushoto ili tuweze kuhitimisha Mahakimu wengi zaidi na kuweza kuchukua nafasi katika Mahakama zetu ambazo hazina Mahakimu.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha tunaendelea na *Order Paper*.

Niseme tu kwamba jumla ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wameshaomba kuchangia katika hoja hizi mbili sasa idadi yao imefikia 73, nadhani wote watapata nafasi tunao muda wa kutosha. *(Makofi)*

Pili, kuna masahihisho ambayo yatagawiwa sasa hivi yaliyotolewa na mtoa hoja ile ya kwanza ya Hali ya Uchumi ya maneno madogo madogo lakini vile vile kuna karatasi ya pili ya masahihisho ya fedha kwa Mkoa wa Manyara. Kwa hiyo, yatagawiwa sasa hivi ili tuweze kujadili kitu ambacho ni sahihi. Tunaendelea na *Order Paper*, Katibu endelea.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2002 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2003/2004 na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2003/2004

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa ya Kamati ya Fedha na Uchumi, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 43(5)(b) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2003, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Sera za Uchumi na bajeti ya mwaka 2002/2003 na mwelekeo wa mpango wa maendeleo na mpango wa bajeti kwa mwaka wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa hotuba zao nzuri zenye kuleta matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matumaini hayo yanaletwa na ukweli kwamba, uchumi wa Tanzania unakua kwa kiwango kikubwa kuliko hata baadhi ya nchi jirani zetu, mfumuko wa bei umeshuka sana na uwekezaji unapanuka kwa haraka. Kuongezeka kwa mauzo nchi za nje, kukua kwa sekta ya viwanda, ujenzi, utalii na kupanuka kwa sekta ya elimu, ni mambo yanayoashiria hali bora ya nchi yetu siku zijazo

kama mambo haya yatasimamiwa na kuendelezwa. Ni matumaini ya Kamati yangu kwamba, Serikali itaendelea kuimarisha uchumi jumla na kuhakikisha kwamba misingi bora ya uchumi iliyowekwa katika miaka michache haivurugwi tena.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga mazingira ya kiuchumi ambayo yamewezesha uchumi kukua mfululizo toka asilimia 4 mwaka 1998 hadi asilimia 6.2 mwaka 2002. Mafaniko haya sio madogo hasa ikizingatiwa misingi dhaifu ya uchumi wa Tanzania. Aidha, Kamati inapongeza juhudi za Serikali katika kupanua na kuimarisha sekta ya elimu na hasa Elimu ya Msingi, kama ilivyojionyesha katika ujenzi wa madarasa mapya na ongezeko la uandikishaji watoto wa darasa la kwanza.

Mheshimiwa Spika, hapa Kamati inapenda kutahadharisha kuwa Elimu ya Msingi peke yake haitoshi kwa maendeleo ya nchi. Maendeleo ya sekta mbalimbali kama vile viwanda, sayansi na teknolojia, madini, biashara na kilimo cha kisasa, vinahitaji elimu inayoanzia Sekondari na kuendelea ili kuwezesha nchi yetu kushindana na Mataifa mengine katika nyanja mbalimbali. Kwa hiyo, mkakati wa aina ya Shule za Msingi unahitajika kwa Shule za Sekondari, Vyuo na Vyuo Vikuu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inapenda kukumbusha kuwa pamoja na mafanikio ya mpango wa MMEM wa kujenga madarasa 15,991, hali ya madarasa ya Shule nyingi za Msingi na hata Sekondari na nyumba za Walimu ni mbaya sana. Kuna hatari ya kuendelea kujipongeza na kusahau hali halisi ya Shule za Msingi ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa nchi kubwa kama Tanzania mabadiliko yaliyoletwa na madarasa mazuri 15,991 ni kidogo sana. Kuna haja ya kuwa na mkakati mpana wa kuboresha majengo ya Shule za Msingi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Kamati inapenda kuishauri Serikali ni ongezeko la akiba ya fedha za kigeni kufikia uwezo wa kuagiza bidhaa kwa kipindi cha takriban miezi nane. Kinachotia wasiwasi ni kwamba, fedha hizi halitokani na ongezeko la mauzo ya bidhaa za Tanzania nchi za nje bali linatokana na fedha za wahisani ambazo Serikali haikuzitumia kwa wakati wake. Kwa hiyo, ongezeko hili halina uhusiano sana na uchumi kuimarika na inaweza kutoweka mara wahisani wakiacha kutoa misaada yao.

Mheshimiwa Spika, ingawa mauzo ya bidhaa nje ya nchi katika mwaka 2002 yalifikia Dola za Kimarekani 902.55 milioni kutokana na kuuza mazao ya kilimo, samaki na bidhaa za viwandani, mchango wa mauzo ya dhahabu katika mapato hayo bado una utata. Katika mauzo ya dhahabu Kamati iliambiwa kuwa Tanzania hupata mrahaba wa asilimia 3 tu na kiasi kingine kinachorudi nchini ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi na manunuzi ya bidhaa hapa nchini na misaada inayotoa Makampuni kwa wananchi wa maeneo ya jirani na migodi. Kamati inashauri uchunguzi wa kina ufanywe na taratibu za mikataba katika sekta ya madini iangaliwe upya ili maslahi ya nchi yazingatiwe. Madini humalizika hivyo kuna hatari ya Tanzania kubaki na mashimo na mazingira yaliyoharibika kwa fedha kidogo inayopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine linaloleta wasiwasi ni matumizi madogo chini ya asilimia 50 ya fedha za maendeleo katika bajeti ya 2002/2003. Kamati ilielezwa kuwa hali hiyo kwa kiwango kikubwa ilitokana na usimamizi hafifu wa watendaji Serikalini na uelewa mdogo wa Sheria ya Fedha za Serikali ya mwaka 2001 na Sheria ya Manunuzi ya Serikali ya mwaka 2001. Aidha, uwezo mdogo wa Watendaji Serikalini umetajwa kama moja ya sababu za kushindwa kutumia fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, sababu hizi Kamati haikubaliani nazo kusema Tanzania yenye umri wa miaka 40 tangu ipate uhuru haina Watendaji wenye uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo, ni hali ya hatari. Kamati inaamini hali hii imesababishwa na usimamizi dhaifu wa viongozi wa kisiasa unaoshindwa kuwachukulia hatua Watendaji wabovu au wanaokwamisha utekelezaji wa miradi kwa uzembe. Kamati inashauri kuwa na utaratibu wa kugawa madaraka kamili kwa Watendaji waweze kuamua na kutekeleza, wasimamiwe na kila mmoja awajibike kwa matendo yake. Kuendelea tu kutoa taarifa kama hizi hakulisaidii Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukuaji wa sekta ya kilimo mwaka 2002 ulishuka kutoka 5.5% mwaka 2001 na kufikia 5%. Kushuka huko hakushangazi, ikizingatiwa kuwa huduma za ugani ni hafifu sana, utafiti katika mazao mengi ni kama haupo, upatikanaji wa pembejeo ni mgumu na bei ya pembejeo ni kubwa sana kwa mkulima mdogo, mikopo ya uzalishaji mazao hakuna na masoko ya mazao hayana uhakika, jambo linalochangia bei ya mazao kuwa ndogo. Kwa kifupi hali ilivyo kwenye sekta ya kilimo ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kulikuwa na taarifa za kuleta matumaini, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa Kuendeleza Kilimo *(Agricultural Sector Development Program)* na Mpango Kamambe wa Kilimo cha Umwagiliaji imeandaliwa na fedha iliyotengwa kwa sekta ya kilimo imeongezwa sana. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo lakini inasisitiza utekelezaji madhubuti wa programu na usimamizi imara. Kamati pia inaipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku ya mbolea kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika bajeti ya 2003/2004. Natumaini wakulima wa Mikoa hiyo watatumia fursa hii kwa kuongeza uzalishaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo inayobeba 80% ya Watanzania na inayochangia 50% ya Pato la Taifa ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Kamati inashauri Serikali kuipa umuhimu wa kipekee sekta hii kwa vile ni dhahiri mkakati wa kuondoa umaskini hautafanikiwa iwapo kilimo hakitaendelezwa. Kwa mujibu wa *House Hold Budget Survey* ya 2000, idadi ya watu maskini kabisa vijijini imeongezeka na matokeo haya yanaendana na kushuka kwa uzalishaji katika kilimo. Aidha, Kamati inashauri Serikali kuimarisha kilimo cha mazao asilia na kuhakikisha ubora wake umekuwa wa kiwango cha juu kushindana katika soko la dunia. Katika mfumo wa utandawazi, jambo muhimu ni ubora wa zao na sio wingi wake, halikadhalika kuanzisha mazao mapya sio kazi rahisi, imarisheni yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa mikopo ya muda wa kati na muda mrefu kumekuwa ni kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya sekta ya kilimo na viwanda. Tunashukuru kuona kwamba, ushauri wa muda mrefu wa Wabunge kuitaka Serikali ianzishe Benki ya Maendeleo sasa umekubaliwa na Serikali. Serikali katika bajeti hii imetamka wazi kuwa Benki ya Maendeleo ya Viwanda na Benki ya Kilimo zitaanzishwa. Kutokana na umuhimu wake Kamati inashauri kuwa kuanzishwa kwa vyombo hivi vya fedha kufanywe mapema kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002 sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 8 na ni sekta iliyovutia wawekezaji wengi katika kipindi hicho. Hii ni taarifa nzuri na ya kuleta matumaini ya uchumi kuimarika. Kamati inashauri Serikali kuisaidia sekta hii kuweza kuongeza uzalishaji na kuvutia wawekezaji wengi zaidi. Kukua kwa sekta ya viwanda na biashara ndivyo vitakavyoimarisha uchumi wa Tanzania. Popote duniani uchumi imara na endelevu ni uchumi ambao msingi wake ni viwanda.

Mheshimiwa Spika, katika nchi changa kama Tanzania, viwanda vingi katika hatua za mwanzo vitakuwa ni vile vinavyosindika mazao ya kilimo. Kwa hiyo, kupanuka kwa sekta ya viwanda kutapanua pia soko la mazao ya kilimo na hivyo kuongeza uzalishaji katika kilimo. Kutokana na uhusiano huo, Kamati inaishauri Serikali kuandaa sera nzuri ya kuainisha sekta ya viwanda na kilimo ili kilimo kiweze kufaidika na kupanuka kwa sekta ya viwanda. Aidha, Serikali ibuni mbinu za kusaidia viwanda vya ndani vizalishe bidhaa bora kwa gharama ndogo viweze kushindana katika Soko la Afrika Mashariki na Soko la Jumuiya ya *SADC*. Viwanda vinavyoweza kuingia kwenye masoko kama haya kwa sasa ni viwanda vya nguo na mafuta ya kupikia. Tunapendekeza viwanda vya mafuta vifanyiwe uchambuzi ili ipatikane njia bora ya kuvisaidia. Gharama ya umeme bado ni kubwa sana kwa maendeleo ya sekta ya viwanda na kwa kuwa sasa Kenya imepunguza kodi ya *VAT* viwanda vya Tanzania vitakuwa na wakati mgumu kushindana katika soko la Afrika Mashariki. Serikali ichunguze suala hili kwa makini sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kikao cha bajeti kuanza, Kamati ilitembelea viwanda vilivyobinafsishwa na visivyobinafsishwa katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya. Tunaishukuru Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma kwa kufanikisha ziara hiyo. Wakati wa ziara tuliona mafanikio ya ubinafsishaji kwa baadhi ya makampuni na matatizo ya taratibu za ubinafsishaji kwa baadhi ya makampuni.

Mheshimiwa Spika, ili Bunge hili liweze kufanya kazi nzuri ya kusimamia na kushauri Serikali baadhi ya mambo yaliyojitokeza yanafaa kufuatiliwa na kuchunguzwa. Aidha zoezi la ubinafsishaji ambalo

limedumu kwa miaka 10 linafaa kufanyiwa tathmini kubaini mafanikio, matatizo na mapungufu na kushauri njia bora za kuendelea na zoezi hilo. Matatizo ya programu ya ubinafsishaji ni mengi sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kauli zinazosema kwamba, kuhoji namna ubinafsishaji unavyotekelezwa ni kupinga sera. Katika hoja hii, napenda kusema kuwa baada ya Sera ya Serikali ya kujiondoa kwenye shughuli za uzalishaji na biashara na kujenga sekta binafsi kukubaliwa yalifanyika maamuzi muhimu. Kwa kuwa utaratibu wa kushirikisha wadau ulikuwa haujaanza kutumika kikamilifu enzi hizo, Serikali yenyewe ilifanya maamuzi yafuatayo: Ilisitisha uanzishaji wa mashirika mapya, iliamua mashirika gani yauzwe, mashirika gani yaingizwe kwenye ubia au kukodishwa, mashirika gani yafungwe na mashirika gani yabaki mikononi mwa Serikali. Kadhalika Serikali iliendelea na ujenzi wa sekta binafsi ingawa hakukuwa na muafaka Kitaifa sekta binafsi ijengwe vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutamka hapa kuwa Kamati ya Fedha na Uchumi haipingi Serikali kujiondoa kwenye shughuli za uzalishaji na biashara. Kamati haipingi programu ya Serikali ya kuondokana na mashirika yenye mwelekeo wa uzalishaji na biashara. Aidha, Kamati haipingi baadhi ya mashirika machache kubaki mikononi mwa Serikali. Hali kadhalika Kamati inaunga mkono programu ya Serikali kujenga uchumi unaoongozwa na sekta binafsi. Kwa maelezo haya, ni dhahiri hakuna anayepinga sera au programu ya Serikali kuondokana na mashirika ambayo kwa mazingira ya sasa yanawezwa kuendelezwa vizuri zaidi na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya ili kuondoa dhana iliyokuwa inajengeka kwamba, kuna Wabunge wanapinga Sera ya Serikali kujiondoa kwenye shughuli za uzalishaji na biashara, hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuamua shirika gani liuzwe tunaweza tukatofautiana kadhalika kuamua sekta binafsi ijengwe namna gani kwa kuwa na programu kamambe ya kushirikisha wananchi au iachwe huria kwa yeyote mwenye uwezo ni eneo tunaloweza kutofautiana. Kwa mfano, Serikali imeshataja mashirika ya kubaki Serikalini kuwa ni pamoja na Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* na Shirika la Viwanda Vidogo *(SIDO).* Lakini kama ingeshirikisha Wabunge, uamuzi kama huo wangesema na *National Micro-finance Bank* nayo ibaki mikononi mwa Serikali kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza tu kwamba, tofauti hizi ni za kiutekelezaji na sio za kisera na hazilengi kubomoa bali kuboresha. Aidha, napendekeza kuwe na mjadala Kitaifa wa namna ya kujenga sekta binafsi. Lazima tukubaliane tunawashirikisha vipi Watanzania katika ujenzi wa uchumi unaoongozwa na sekta binafsi. Kuwaacha Watanzania hivi hivi tu wajitumbukize kwenye utandawazi hawatafika mbali, ushindani ni mkali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti ya mwaka 2002/2003 ilitegemea misaada toka nje kwa 47% na bajeti ya 2003/2004 ni tegemezi kwa msaada toka kwa wahisani kwa 45%. Hali hii ni hatari kwa maendeleo na uhuru wa nchi. Hata wafadhili wenyewe wamesikika wakisema Tanzania ipunguze utegemezi wa misaada katika bajeti yake. Kamati inashauri Serikali kuwa na mpango thabiti katika sekta za kilimo na viwanda ili kuongeza mapato ya ndani. Aidha, Serikali iimarishe mbinu za kukusanya mapato ili kuziba kabisa mianya ya ukwepaji kodi, uzembe na wizi. Hadi sasa mapato ya ndani yamesimama kwenye kiwango cha 12.3% ya Pato la Taifa. Misamaha ya kodi ni eneo lingine linalopunguza mapato ya Serikali. Tunaipongeza Serikali kuanzisha mpango wa *Treasury Voucher System,* ambao umeonesha mafanikio makubwa lakini inashangaza kuona katika bajeti hii fedha nyingi zimetengwa kwenye fungu hilo tena.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Waziri wa Fedha kwamba, aliahidi kutafuta njia nzuri ya kuweka fedha za Mfuko wa Pembejeo mahali ambapo ni rahisi kwa wananchi toka sehemu mbalimbali za nchi kupafikia. Katika hotuba yake ya bajeti hajalitaja hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuzingatia ushauri wa Kamati yangu na maoni ya Wabunge na hatimaye kuja na bajeti ambayo kwa kiwango kikubwa inapunguza mzigo wa kodi na kuondoa kero kwa wananchi wa kawaida. Bajeti hii ni nzuri na ikisimamiwa vizuri itakuwa na matokeo mazuri kwa uchumi wa Tanzania. Naiona bajeti hii kama ni mwanzo wa utekelezaji wa kauli ya Rais wakati akichukua madaraka

kwa mara ya pili mwaka 2000 ya kuitaka Serikali kufikisha matunda ya mafanikio ya uchumi jumla kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaamini fedha zinazotengwa kila mwaka katika bajeti zinatosha kuleta mabadiliko makubwa katika uchumi na maendeleo ya nchi hii. Lakini hilo linawezekana tu iwapo fedha hizo zitasimamiwa vizuri kuzuia matumizi mabaya, ubadhirifu, wizi na uzembe. Ingawa mapato yameongezeka, bado kuna Idara ambazo hazipati bajeti ya kutosha kutokana na Serikali kupanua matumizi yake na kushindwa kudhibiti matumizi ya fedha zikishatoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha na hususan Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa hatua inazochukua kufuatilia fedha za Serikali katika Wizara na Idara mbalimbali. Kamati inashauri Idara ipewe kila aina ya msaada ili ifanikishe malengo yake. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuwawajibisha Maafisa Wahasibu wanaotumia fedha bila kufuata taratibu zilizowekwa na Serikali. Mfumo wa kusimamia fedha za Serikali umekuwa unabadilikabadilika mara kwa mara kuwakwepa wabadhirifu badala ya kuwachukulia hatua. Sasa mnapeleka fedha za Wilaya moja kwa moja Wilayani kuwakwepa Ma-*RAS*, fedha zitakapoliwa Wilayani mtapeleka vijijini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuondoa kodi na kero kwa wananchi ni jambo lingine na kuhamasisha uzalishaji katika uchumi ni jambo tofauti. Kujenga uchumi haraka kunahitaji usimamizi wa karibu, nidhamu na uwajibikaji. Tukumbuke msemo wa wahenga usemao: "Maneno makali peke yake hayavunji mfupa". Nawashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri na kwa ushirikiano wao. Pia nawashukuru Maafisa mbalimbali waliofika mbele ya Kamati kwa msaada na ushirikiano walioipatia Kamati yangu. Naomba ushirikiano huu uendelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED) - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI NA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Namba 43(b)(c), Toleo la 2003, naomba kwa ruhusa yako, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kuwasilisha maoni yetu juu ya Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa na Mapendekezo ya Mpango wa muda wa kati na mfumo wa matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, pamoja na makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha za Serikali kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote 15 kutoka Chama cha *CUF*, ambao awali waliachishwa Bungeni na wananchi wakaamua kuwachagua tena na wanne wa *CUF* waliorudishwa na Mahakama na wanne wa CCM waliochaguliwa hivi karibuni. Wote tunawapongeza na kuwaomba kuwa tushirikiane katika kuwatumikia Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nitumie fursa hii kuipongeza Timu ya *Simba Sports Club* kwa ushindi walioupata na kufikia katika mechi ya robo fainali. Michezo katika Dunia ya leo ni Kitega Uchumi kizuri, ni chombo cha kuleta maelewano ndani ya jamii na ndio maana *UN* wanataka kuitumia michezo kusuluhisha migogoro. Hivyo, kujenga kiwanja ni muhimu sana lakini zaidi ni maandalizi ya vijana wetu kuichukulia michezo kama sehemu ya ajira yao, ndio jambo linalotakiwa hivyo tuwasaidie. Pia ni vizuri bajeti ya michezo iwe nono na ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba niwapongeze Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa mawasilisho yao ya mipango na bajeti kwa kugusa kwa kiwango kikubwa yale yaliyokuwa yakisemwa na Wabunge wa Kambi ya Upinzani, pamoja na Wabunge wa Chama Tawala hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, kama mwaka 2002 tulivyogusia, juu ya Muafaka, naomba kusema kuwa, matokeo ya Uchaguzi Mdogo Pemba yametoa somo jipya kwa wana demokrasia kwamba, wananchi wanajua wanachokitaka. Pili, kama tukiwa na Tume huru tunaweza kufanya chaguzi zetu kwa amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo Kambi ya Upinzani inawaomba Mheshimiwa Rais Mkapa na Mheshimiwa Rais Amani Karume, watimize ahadi yao waliyotoa kwa Watanzania na Dunia kwa jumla kutekeleza Muafaka kikamilifu. Hadi sasa Mheshimiwa Karume, hajachagua wajumbe wawili kutoka *CUF* kuingia katika Baraza la Wawakilishi.

Mheshimiwa Spika, kati ya mambo 29 yaliyomo ndani ya Muafaka ni asilimia 30 tu ndio baadhi yake yametekelezwa angalau nusu. Taarifa za Tume zilizoundwa kuchunguza mauaji ya tarehe 26 na 27 bado kufanyiwa kazi na wahusika kulipwa kifuta machozi kama walivyoahidiwa.

Aidha, Tume alizounda Mheshimiwa Rais Karume, kutathmini watu waliofukuzwa kazi kutokana na sababu za kisiasa na ile ya watu waliovunjiwa nyumba zao pia haijaelezwa chochote. Hata marekebisho ya Mahakama hayajafanyiwa kazi bado. Ni matumaini ya Watanzania wote kwamba, viongozi wetu wataheshimu kauli zao na ahadi zao hivyo tunaomba kuwakumbusha kuwa watimize wajibu wao. Muafaka umeijengea heshima kubwa nchi yetu, ni muhimu kuulinda na kuuendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kichocheo kikubwa cha wawekezaji kuja nchini kwetu kuwekeza ni amani na utulivu uliopo lakini tuelewe kuwa raslimali hii ni ile inayoondosheka hivyo inahitaji kutunzwa kama yai jeteta ili iwe endelevu.

Mheshimiwa Spika, moja katika mambo yanayovuruga amani na utulivu ni chaguzi za nchi. Kutokana na uzoefu tulioupata katika chaguzi za Pemba, kama Tume kwa kiwango fulani ikiwa huru, uwezekano wa kuwa na uchaguzi ulio huru na haki ni mkubwa mno.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kifungu cha 5(3) kimeelezea kuwepo kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura. Sheria ya Uchaguzi ya 1985 Kifungu cha 12 kama ilivyorekebishwa kinaelezea kuwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura litaanza kutumika baada ya uchaguzi wa mwaka 2000. Kitu cha kushangaza ni kuwa bajeti ya Tume ya Uchaguzi ya mwaka 2002/03 ni shilingi 1.7 bilioni, bajeti ya 2003/2004 ni shilingi 1.83 bilioni wakati gharama ya Daftari la Kudumu ni shilingi 16 bilioni kama ilivyoombwa na Tume yenyewe. Lakini Serikali katika bajeti tuliyonayo yaani 2003/2004 imetoa kiasi cha Sh.1.3 bilioni tu hiki ni kichekesho ukilinganisha na kiwango halisi kilichoombwa na Tume. Pamoja na hayo, Serikali wakati imetenga kiasi hicho kidogo sana, chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, imetenga Sh. 3 bilioni kwa kitu kinachoitwa kutengeneza vitambulisho. Tunavyofahamu vitambulisho viko chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kama vinahusiana na uchaguzi vinatakiwa viwe chini ya Tume ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, inaelekea Serikali haina nia ya kuanzisha Daftari la Kudumu na Waswahili wanasema: "Usipoziba Ufa Utajenga Ukuta." Namwomba Mheshimiwa Rais wetu, ambaye karibuni atatuaga, atutayarishie mazingira mazuri ya kuwa na uchaguzi ulio huru na haki ili matunda ya kazi yake yawe endelevu na ya kuheshimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia Serikali kuchukua hatua mbalimbali ilizozichukua katika kutekeleza Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa 2000 ambazo naomba kuzinukuu baadhi yake:-

(i) Mashirika ambayo ni ya msingi na nyeti kama vile Bandari, Reli, Posta, Simu, Mabenki ya Umma na Nishati kwa maendeleo ya Taifa yanaendelea kumilikiwa na Dola;

(ii) Sera ya Kurekebisha Mashirika ya Umma itakwenda sambamba na hatua za kuwalinda wafanyakazi wa mashirika yatakayohusika, CCM itaona kuwa ajira ya wafanyakazi inalindwa kwa kadri itakavyowezekana na fidia za haki kwa wafanyakazi watakaoachishwa kazi zinatolewa; na

(iii) Wafanyakazi wanaoachishwa kazi wanasaidiwa na waingie katika sekta ya wananchi wanaojiajiri.

Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM, Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, ilipanga mkakati wa kutekeleza Sera za Uchumi kama ifuatavyo:-

(i) Kuona kuwa uchumi unakua kwa viwango na kasi kubwa ukilinganisha na mwaka uliopita;
(ii) Mikakati ya kupunguza umaskini hasa usio wa kipato; na

(iii) Kuratibu mipango Kitaifa, uwekezaji na ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, je, misingi hii imeheshimiwa na Serikali? Sote ni mashahidi wa wafanyakazi wetu waliotumikia Taifa hili kwa maagizo na miongozo ya Serikali yao wanavyosumbuka na kutaabishwa katika kudai haki zao zilizotokana na ahadi za Serikali. Wapo waliokufa bila ya kupata haki zao, wapo waliokwenda Mahakamani na wapo waliowajia Waheshimiwa Wabunge kuomba msaada wao.

Ndio maana tunaomba uhakiki wa kina wa *PSRC* kwani kwa mujibu wa taarifa ya *IMF* ni kwamba Serikali haijanufaika na ubinafsishaji kwa maana ya faida kutokana na mauzo. Fedha zilizopatikana ni kidogo mno ikilinganishwa na madeni. Kwa mfano, *IMF* inasema kuwa Serikali haijapata hata senti moja kutokana na ubinafsishaji wa *TTCL* wa asilimia 35 wa hisa za Kampuni ya *TTCL*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM kudai kuwa katika kuendeleza, kuufufua na kuujenga uchumi wa Taifa, Serikali ya CCM itaongozwa na Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, inayolingana na wakati tulionao. Shabaha ya Ujamaa katika kipindi hiki ni kuwafanya wananchi wenyewe kuwa ndio wamilikaji wakuu wa uchumi wa dola, kuwa mhimili zaidi wa uchumi wa Taifa. Je, ubinafsishaji umewafanya wananchi wa Tanzania ku wa wamilikaji wakuu wa uchumi kwa sasa?

Mheshimiwa Spika, mashirika 134, asilimia 100 yamenunuliwa na Watanzania, mashirika 16 wawakezaji wa nje wamenunua kwa asilimia 100 na mashirika 116 yamebinafsishwa kwa ubia kati ya Serikali, wabia wa nje na wabia wa ndani.

Mheshimiwa Spika, tunaomba tupatiwe thamani ya mashirika hayo ili tuone kama ubinafsishaji umewafanya wananchi kuwa wamiliki wakuu, kama ilivyotaka Ilani ya Uchaguzi. Aidha, Serikali ieleze ni wananchi wangapi walipoteza ajira. Tuna taarifa kuwa thamani ya mashirika hayo 134 yanayomilikiwa asilimia mia moja na Watanzania haifiki hata nusu ya thamani ya mashirika 16 yanayomilikiwa na wawekezaji wa nje. Tunaitaka Serikali itoe taarifa rasmi ili hisia hizi ziondoke na tuwe na uhakika kama umiliki huo kweli umewanufaisha Watanzania ukiacha ule wa wachache walionunua hisa, kwenye mnada wa hisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hii, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi mkubwa wa kufikiwa malengo yaliyowekwa na Dira ya Taifa kwamba uchumi ukue kwa asilimia nane au zaidi.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imekadiria Pato la Taifa litakua kwa asilimia 7.4 mwaka 2003 hadi 2007. Kwa miaka sita iliyopita uchumi umekua kwa wastani wa asilimia 4.3, je, lengo la kukuza uchumi kwa asilimia nane litawezekana?

Mheshimiwa Spika, tunamwomba Waziri atupe mchecheto wa kutuonyesha namna ya ukuaji unavyoweza kukua kwa kiasi hicho, wakati katika miradi ya maendeleo katika mwaka wa 2002/2003 utekelezaji ni asilimia 52.8 tu. Kwa hiyo upo wasi wasi kuwa hata mwaka huu ongezeko lililopo la miradi ya maendeleo linaweza kuwa chini ya hapo. Lakini Waziri anaweza kutupa kwa undani vigezo vilivyotumika ili kufikia lengo hilo.

Mheshimiwa Spika, mpango uliotangazwa na Serikali wa kuwa na Mikoa itakayopangiwa aina ya mazao ya kuzalisha ya chakula na biashara, utakuwa mzuri tu ukitekelezwa vizuri. Sambamba na hatua hiyo basi tunashauri wazalishaji wa bidhaa za viwandani zinazotokana na malighafi za kilimo washauriwe kuwa na Mikataba na wakulima ili malengo hayo yawe na manufaa kwa wananchi na kwa Taifa kwa ujumla. Mikakati hiyo ilenge:-

(i) Kuwahakikishia wakulima soko ambalo kwa sasa ni kero kubwa kwa wakulima; na

(ii) Upatikanaji wa Pembejeo wa uhakika. Kwa mfano, wazalishaji wa unga wa ngano ambao wanaagizia ngano kutoka nje, washauriwe wakae na wakulima wa ngano wa Singida na Arusha ili waweke mikakati na mipango ya kupata ngano ya kutosheleza viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo umeainisha Mradi wa Minazi na wa Chai. Hakuna mradi wa kuendeleza uzalishaji wa mahindi na mpunga. Aidha, Serikali ya Japan imeahidi kusaidia katika Mradi wa Umwagiliaji Maji lakini Serikali haikutenga hata senti moja katika mradi huu. Waziri tunaomba atupe ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua nyingi zinazochukuliwa ili uchumi wetu uweze kuingia kwenye ushindani wa kiuchumi, bado hatua madhubuti hazijachukuliwa za kupunguza ughali wa uchumi wetu. Gharama za kuendeshea uchumi wetu ni kubwa kutokana na gharama kubwa za sekta ya nishati hasa umeme, usafiri na usafirishaji na mawasiliano. Kambi ya Upinzani inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Tathmini ya kina ifanyike juu ya kuendelea kulipa shilingi bilioni 3.5 kila mwezi kwa *IPTL*. Aidha, tathmini ya Mradi wa Songosongo namna utakavyosaidia kuongeza au kupunguza ughali wa uchumi wetu;

(ii) Mkataba na *IPTL* unasema wazi kukiwa na mgogoro Mahakamani Serikali inaweza kuvunja Mkataba na *IPTL*. Ni vizuri Serikali itoe taarifa rasmi kwa nini hadi sasa haijachukua hatua hiyo baada ya *IPTL Directors* kupelekana Mahakamani wao kwa wao; *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mawasiliano tunashauri ushuru ulioongezwa wa asilimia 5.7 kwenye mawasiliano ya simu *(Air Time)* utaongeza ughali wa uchumi, hivyo utazamwe upya. Tathmini ifanywe namna tunavyoweza kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji.; *(Makofi)*

(iv) Utumiaji wa *Microwave* ambayo *infrastructure* yake haichukui muda mrefu na inaongeza gharama, tunashauri tutumie *Fiber Optic* ambayo *life span* yake ni zaidi ya miaka 20; na

(v) Kuwa na *coordination* katika uwekezaji wa raslimali za mawasiliano kwa mfano, hivi sasa *TANESCO, TRC* na *TTCL,* wote wanaweka *Long Distance Fiber Optic Transmission*. Mradi huu unaweza

kufanywa na Shirika moja tu na wengine wakaweza kununua huduma hiyo, hasa kwa vile *Fiber Optic* inatoa *lines* nyingi hivyo kuwezesha kuwa na uwezo wa kutumiwa na watumiaji wengi wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi zinazopendekezwa zitapunguza mzigo wa madeni na utumiaji mbaya wa raslimali ndogo tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, tumefurahishwa na Serikali kuitazama sekta ya uvuvi. Sekta ya maliasili ilikuwa kwa asilimia 5.4. Sekta hii inaweza kukua maradufu kwani sehemu kubwa ni uvunaji hasa wa samaki.

Mheshimiwa Spika, uvuvi ulikua kwa asilimia 6.5 pungufu kwa 0.5 ikilinganishwa na mwaka 2001, hadi sasa samaki wanaosafirishwa kwa wingi ni wale wa kwenye Maziwa. Lakini wa Baharini ukiacha kamba, samaki wengine bado hawajavunwa vya kutosha. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa:-

- Miradi ya uvuvi wa Bahari Kuu *(Deep Sea Fishing)* ipewe kipaumbele ili kuongeza uuzaji wa samaki nje na kuongeza lishe kwa Taifa; na

- Mayai ya samaki yana wastani wa Dola 30 - 40 kwa kilo, eneo hili linaweza kutuingizia mapato na kutoa ajira kwa wavuzi wetu iwapo litatiliwa mkazo.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mifugo iliongezeka kutoka asilimia 3.3. mpaka 3.5 mwaka 2002. Sekta hii inaweza kukua kwa haraka zaidi kama ile ya uvuvi kama mkakati madhubuti wa kuuza bidhaa za mifugo yenyewe na zinazotokana na mifugo zitaandaliwa vizuri. Sisi Watanzania tumekuwa na mazoea ya kuuza bidhaa zetu zaidi Ulaya, lakini kuna masoko mazuri zaidi nchi za Ghuba na Mashariki ya mbali.

Mheshimiwa Spika, tunashauri kuwa tutumie uzoefu wa baadhi ya Wabunge na wananchi kwa ujumla, kutafuta masoko mapya ya bidhaa zinazotokana na mifugo nchi za Ghuba na Mashariki ya Mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuwa wazi juu ya suala la umaskini. Kukiri kwa Serikali kuwa hali ya umaskini wa kipato na maendeleo ya jamii haijabadilika sana ni jambo zuri. Utafiti unaonyesha kuwa umaskini wa kukosa mahitaji muhimu umepungua kutoka asilimia 39 mwaka 1991/92 na kufikia asilimia 36 mwaka 2000/2001.

Mheshimiwa Spika, kigezo kilichotumiwa kupima umaskini ni kuwa mkazi wa Dar es Salaam, mtu mzima, anahesabiwa kuwa maskini ikiwa anatumia chini ya shilingi 330/= kwa siku. Mkazi wa Dodoma shilingi 275/= na wa Vijijini shilingi 250/= kwa siku.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea Serikali ingelitumia vigezo vya Kimataifa vya kutumia angalau dola moja kwa siku. Kwa kutumia vigezo hivyo, umaskini umeongezeka toka asilimia 48 mwaka 1991/92 mpaka kufikia asilimia 75 mwaka 2001. Kwa kubadilisha takwimu hizi, Serikali haikuonyesha taarifa sahihi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kupunguza umaskini, kuna maeneo ambayo Kambi ya Upinzani inaona Serikali imependa na imefanya makusudi watu wawe maskini. Maeneo hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuacha kuwashirikisha wananchi katika madini ya dhahabu na almasi na angalau hata kwa kuyashauri Makampuni ya Dhahabu na Almasi kujiunga na *Stock Exchange* ili wananchi wanunue hisa hizo; na

(ii) Kutokuwa na uendelevu katika vyombo tunavyovianzisha vya kupambana na ajira na kupunguza umaskini. Mfano ulio hai ni *National Income Generation Programme (NIGP),* ambayo japo ilianzishwa kwa kishindo, lakini hivi leo hatma yake haijulikani. Mfuko huu ulianzishwa na Serikali, pamoja na wahisani, kwa madhumuni ya kutekeleza Sera ya Taifa ya Ajira *(National Employment Policy)*

iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais na madhumuni makubwa ni kuondoa umaskini katika makundi ya vijana, wanawake na watumishi pamoja na walemavu.

Mheshimiwa Spika, hadi Machi 2003 miradi 26 imetekelezwa kwa thamani ya Dola 25 milioni katika sekta mbalimbali na wananchi wapatao 23,892 wamepata ajira na kujiongezea kipato. Ni wachache sana lakini ni vizuri Mfuko huu ukafufuliwa kama mkakati mmojawapo wa kupiga vita umaskini na usimamiwe vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo wa 2003/2004, yaani *Framework for Poverty Eradication,* kuna fedha za nje Sh. 800,000,000/=, ambazo tuna mashaka huenda zisipatikane kwa wakati hasa kwa vile Serikali haikutenga fedha za ndani kama inavyoonekana kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, tunaishauri Serikali iiendeleze miradi iliyoanzishwa na *NIGP* na mipya minane ikiwemo Mradi wa Uzalishaji Chumvi Pemba na Unguja, Mradi wa Kukopesha Ng'ombe wa Maziwa Unguja na Pemba, Arusha, Manyara, Mara, Mwanza, Pwani, Iringa, Mbeya, Morogoro, Rukwa na Ruvuma, pamoja na miradi mingine iliyokwishaandaliwa. Mahitaji ya miradi hii ni Sh. 314,000,000 tu. Hivyo, Serikali ikiwa na nia ina uwezo kabisa wa kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti la 2002/2003, tulielezea uvunjwaji wa Katiba Ibara ya 24 (1), juu ya Haki ya Kumiliki Mali. Mbali na kuvunja Katiba, Serikali kwa makusudi inawafanya raia wao wa Zanzibar wawe maskini kwa kuwazuia wasiuze bidhaa zao za biashara hasa karafuu kwenye soko wanaloona wao lina manufaa kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wananchi wa Zanzibar hasa Pemba wanazo karafuu zao ndani kwa sababu ya bei ndogo wanayopewa na Serikali na wao kuzuiwa wasiuze kwenye bei inayowafaa. Hii ndiyo Serikali ambayo inajali Sheria na Katiba na huu ndiyo Utawala Bora? Pia ni kweli Serikali ina nia ya dhati kuondoa umaskini?

Mheshimiwa Spika, umaskini utaweza kupungua kwa haraka kama tutaongeza kwa kasi kiwango cha elimu cha vijana wetu. Tunashauri Serikali iendelee kuchota sera za Wapinzani za kuwa na elimu ya lazima ya darasa la kumi na mbili, ili mtoto amalize shule akiwa na umri wa miaka 18 ili aweze kuingia kwenye soko la ajira. Aidha, elimu ya walimu iboreshwe ili tusije tukarudia matatizo tuliyokumbana nayo kwa walimu wa *UPE*. Aidha, tunashauri kuwa hatimaye Serikali itoe elimu bure hadi Chuo Kikuu ili tuwe na hakika kwamba, vijana wetu wataweza kuingia kwenye soko la ushindani la ajira na au kujiajiri kama mpango mahsusi wa kupiga vita adui yetu umaskini kama walivyofanya wenzetu wa Asia.

Mheshimiwa Spika, tumezipokea takwimu za nguvu kazi na ajira, ila nafikiri Waziri ni vizuri azitolee tafsiri pana zaidi, kwani ni vigumu kuelewa kwamba, watu 15.5 milioni wawe kweli wanafanya kazi na bado ukuaji wa uchumi wetu uwe chini ya asilimia saba. Je, ni kweli watu 15.5 wana ajira na ni ajira gani? Vijana wetu wengi huonekana vijiweni siyo tu Mijini bali hata Vijijini kwa kukosa ajira, ardhi inayoaminika na mitaji.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali, asasi binafsi na madhehebu ya dini, tatizo la Ukimwi linaendelea kuwa tatizo ambalo hatimaye litatuathiri katika ukuaji wa uchumi wetu. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa tathmini ifanywe ili itusaidie kutupa mbinu mpya za kupambana na janga hili, kwani baada ya semina na warsha nyingi zenye kutumia fedha nyingi, bado maambukizi yanazidi kuongezeka kwa kasi. Aidha, Serikali bado haijaweka mkazo wa kutosha kwa watu walioathirika na mayatima ambao Kambi ya Upinzani inaona wana haki ya kupata huduma za lazima kutoka Mfuko wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Taifa ni chombo muhimu pekee cha kutafsiri na kutekeleza Sera za Chama Tawala kwa vitendo. Katika bajeti Serikali inapata fursa ya kupanga matumizi ya fedha kidogo zilizopo katika maeneo na sekta zinazohitaji kupewa kipaumbele ili malengo makuu ya Serikali yatekelezeke. Hivyo basi, matumizi ya Serikali yalingane na uwezo wa mapato ya Serikali na matumizi ya Serikali yawe endelevu, pasiwe na nakisi kubwa ya bajeti inayojazwa kwa kuchapisha fedha, kukopa ndani

au nje. Bajeti ya Serikali lazima ilenge katika kupunguza kutegemea misaada na mikopo. Mikopo ielekezwe zaidi kwenye maendeleo na kukuza uchumi na si uendeshaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali igawanywe kwa uwiano katika sekta mbalimbali, kwa lengo la kuongeza ufanisi na kutoa kipaumbele katika maeneo yanayokuwa chachu katika kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za Serikali katika sekta zilizopewa fedha hizo yaendeshwe kwa ufanisi na kwa kuongeza tija. Darasa linalogharimu shilingi milioni moja lisijengwe kwa gharama kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya Serikali, kodi ndiyo njia pekee ya uhakika ya kupata fedha za kugharamia shughuli za Serikali kama vile kuelimisha watoto, kutoa huduma za afya na kujenga barabara.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzuri wa kodi ni ule unaoikusanyia Serikali mapato ya kutosha bila kuiingiza Serikali katika mzigo wa madeni na bila kuathiri shughuli za kiuchumi na kibiashara kwa kupunguza motisha kwa wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara na wenye viwanda. Sera bora ya kodi inazingatia uwezo wa kulipa kodi. Viwango vya kodi viwe nafuu, lakini wenye uwezo walipe kodi. Misamaha holela ya kodi inaendeleza rushwa na utawala mbovu. Katika nchi nyingi, matajiri wana nguvu za kisiasa na wanatumia nguvu hizo kupunguza mzigo wao wa kodi na kuuhamishia kwa walala hoi.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzuri wa kodi ni ule ambao unaeleweka vizuri, uko wazi, mwepesi kuuendesha, unapunguza tofauti au angalau hauongezi tofauti za vipato. Sasa hivi tatizo ni tofauti za vipato katika nchi yetu. Viwango vya kodi viwe vinaeleweka na kutabirika na visiwe vinabadilika mara kwa mara. Kwa hiyo, tunaamini mabadiliko ya Sheria za Kodi yatazingatia hayo.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya 2003/2004 bado ni tegemezi. Asilimia 45 ya matumizi ya Serikali yanategemea misaada na mikopo ya nje. Hata hivyo, Serikali inaonekana kubana matumizi yake ya jumla yalingane na mapato ya ndani na misaada ya kutoka nje. Utaratibu wa kuziba nakisi ya bajeti kwa kuchapa noti nyingi umeepukwa. Utaratibu wa *cash budget* umetumiwa kubana jumla ya matumizi yalingane na makadirio ya bajeti. Hata hivyo, Serikali itambue kuwa na salio mwisho wa mwaka wa fedha sio utaratibu mzuri na hasa kwa bajeti ya maendeleo kama ilivyotahadharishwa na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mpango wa bajeti ya fedha taslim ulipaswa kuwa wa muda wa mpito wa kurejesha nidhamu ya matumizi. Katika utaratibu wa *Cash Budget*, matumizi halisi hayafanani na bajeti inayopitishwa na Bunge katika kikao cha bajeti. Wakati umefika sasa wa kuacha utaratibu wa *Cash Budget* na kuwa na bajeti ya kweli ambayo Serikali itaiheshimu. Wizara ya fedha imekuwa na madaraka na mamlaka makubwa ya maamuzi ya sekta gani zinazopata fedha katika utaratibu huu wa *Cash Budget*. Miradi ya maendeleo imeathirika zaidi katika utaratibu huu wa *Cash Budget*. Ni sekta zile ambazo zinaungwa mkono na wafadhili katika mpango wa msamaha wa madeni na zinazopata *Basket Funding* ya wafadhili, ambazo zimenusurika na matumizi yake yanalingana kwa kiasi kikubwa na bajeti. Usimamizi wa matumizi ni muhimu lakini ufanisi wa matumizi ya Serikali utapatikana ikiwa Wizara nyingine zina motisha ya kufanya kazi zao vizuri. Katibu Mkuu ambaye hana uhakika wa bajeti yake, hawezi kuwa Kiongozi shupavu katika kuongeza ufanisi na tija katika Wizara yake. Ndiyo maana tumeshindwa kujenga *capacity* ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003, Serikali ilitenga bajeti ya maendeleo kuwa asilimia 34 ya matumizi yote. Katika kipindi cha Julai 2002 mpaka Machi 2003, bajeti ya maendeleo imetumia asilimia 19 ya matumizi yake yote. Mipango ya bajeti na matumizi halisi havioani. Mwaka 2003/2004, Serikali imetenga asilimia 31 ya matumizi yote yaende katika bajeti ya maendeleo. Matumizi halisi yatakuwa chini ya hapo. Serikali ijenge uwezo wa kusimamia miradi ya maendeleo. Uwezo huo bado tunaamini ni mdogo na unaathiriwa na utaratibu wa *Cash Budget*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kukusanya mapato yanayotokana na madini, lakini sekta hii bado haijawashirikisha wananchi katika kuwapatia mapato yatokanayo na madini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2001 uzalishaji wa almasi ulipungua kwa asilimia 16 na kusababisha mauzo kupungua kwa asilimia 7.9. Serikali haielezi upungufu huu mkubwa umetokana na nini na wala haisemi ni vipi Watanzania wenye ardhi inayochimbwa almasi au dhahabu watafaidika na umiliki wao wa ardhi utakuwaje. *(Makofi)*

Katika hotuba ya Waziri wa Fedha, ameelezea *Tanzanite* ambayo haijakatwa, haitasafirishwa nje, haijakatwa lakini hasemi chochote kuhusu madini mengine. Isitoshe katika Gazeti la *SAA*, ambalo linawekwa kwenye ndege ya *ATC*, wawekezaji wanasema wazi kuwa wanavuna na kuuza haraka haraka kwa sababu *Tanzanite* itamalizika katika miaka 25 ijayo.

Mheshimiwa Spika, kama kuna eneo ambalo lingetujengea uchumi endelevu ni la dhahabu, almasi na madini mengine, lakini eneo hili Serikali inalionea haya kuligusa. Hatuelewi ni kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuweke viwango nafuu vya kodi lakini Makampuni makubwa pia yalipe kodi. Hakuna mantiki ya kufuta ushuru wa forodha wa vifaa maalum vya mawasiliano kwa njia ya radio, *walkie talkies,* kwani hizi zaidi zinatumiwa na makampuni ya madini na wawindaji wakubwa na baadhi ya Makampuni ya usafirishaji ambao wana uwezo wa kulipia tofauti na simu za mkono ambazo hata mitaani watu wa kawaida wameanza kuzitumia na tungeshauri waendelee kuzitumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa:-

(a) Viwango vya *royalties* vinavyotozwa kwa dhahabu 3% viangaliwe upya kwa sababu dhahabu Tanzania haitafutwi ipo na tunaijua ilipo, mwekezaji anakuja kuvuna tu sio kutafuta, hivyo Mikataba yake huwa tofauti na wanaotafuta. Sisi Mikataba yetu imekuwa ya aina moja tu hivyo, hiyo sio sahihi;

(b) Kuondoshewa kodi *Subcontractors* ambao wanatoa huduma kwa wawekezaji wa madini si sahihi, kwani tutakuwa kwa mradi mmoja tunasamehe kodi kwa zaidi ya kampuni moja, hii nayo ni hatari sana;

(c) Utaratibu wa kusamehe kodi ya *capital investment* kwa kutegemea taarifa zinazotolewa na mwekezaji tu, bila ya kufanya ukaguzi na uchunguzi nayo hiyo pia sio sahihi;

(d) Uchimbaji wa Madini unaharibu sana mazingira, ni vizuri tukaelewa hatua zinazochuliwa kudhibiti uchafuzi wa mazingira;

(e) Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi ni vipi wawekezaji wa madini wanaruhusiwa kuzalisha umeme wao na kusamehewa kodi hata ya mafuta wanayotumia, lakini wazalishaji wa umeme unaotokana na makaa ya mawe wanalazimika kuiuzia *TANESCO* ambao huuza kwa bei kubwa. Kwa nini Kiwira wasiruhusiwe kuuza umeme moja kwa moja Kiwanda cha Saruji na kwa wananchi kama walivyoruhusiwa wawekezaji wa dhahabu? Hiyo itafanya saruji kuwa na bei ndogo; na

(f) Kambi ya Upinzani kwa mara nyingine tena inashauri asilimia 20 ya *VAT* ipunguzwe kama Waziri alivyowahi kuahidi ndani ya Bunge hili ili kumpunguzia mlaji ughali wa maisha, hasa kwa vile nchi jirani zimepunguza chini ya kiwango hicho.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Waziri wa Fedha kuwa Tume hii ambayo itafanya kazi chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kwa kuongezea Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambayo ni sehemu ya Katiba ya Muungano, itasaidia sana katika kutatua matatizo Sugu ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa wa 44, Mheshimiwa Waziri anasema kuwa, Bajeti ya 2003/2004 imezingatia mgawo wa asilimia 4.5 ya misaada nafuu ya nje isiyo ya miradi kwa ajili ya kusaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ni vizuri Waziri akatuelezea:-

- Mwaka wa Fedha uliokwisha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa utaratibu huu ilipata kiasi gani? Pia kwa nini haionekani katika mafungu ya matumizi halisi ya mwaka uliokwisha? (Makofi)

- Ni kasma gani inayotumika kutoa fedha hizi na makisio yake ni kiasi gani mwaka huu 2003/2004?

- Ni sababu zipi za msingi zinazoifanya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar isifaidike na Msamaha wa *HIPC* wakati suala la msaada na mikopo ni suala la Muungano? *(Makofi)*

- Pia Mheshimiwa Waziri atueleze wamiliki wa hisa za *BOT*, ambao ni Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ambayo mchango wake ulitokana na *East African Currency Board* na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kila mwaka wanapata mgao wa kiasi gani unaotokana na faida inayopata *BOT*? Uwiano huo ukoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti haionyeshi fedha zilizotengwa kushughulikia tatizo la njaa. Shilingi bilioni 2.2 zimetengwa kununulia chakula cha hifadhi. Ikiwa kilo moja ya mahindi itagharimu 100/= kuinunua na kuisafirisha na kuihifadhi, fungu hili litanunua kama tani 22,000 tu. Fedha zilizotengwa kwa tahadhari zote ni bilioni 8.7, ikiwa fedha ya tahadhari itatumiwa kuagizia mahindi kwa wastani wa dola 200 kwa tani, basi Serikali itaweza kuagiza tani 43,000 lakini uzoefu unaonyesha miaka yote tumenunua chakula kwa kiwango cha tani 250,000. Isitoshe Bajeti haikutenga fedha za kugawa chakula kwa njia ya msaada hivyo suala hilo tunaomba liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhitimisha uwasilishaji huu kwa kuipongeza kwa dhati Serikali kwa mambo yafuatayo:-

(a) Kukubali ushauri mbalimbali wa wananchi kupitia Vyama vyao vya Siasa, Sera ya *CUF* na CHADEMA, kwa mfano, juu ya kufuta kodi ya maendeleo na wale walioitwa Profesa Uchwara .....

**WABUNGE FULANI:** Ohooo!

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI NA WIZARA YA FEDHA):** Mnaweza kuzomea tu lakini wale walioitwa Profesa Uchwara, sasa wamebadilika sio Uchwara tena. Mwenye kutaka kujua atazame Sera na Ilani ya Vyama hivyo na kulinganisha na ya CCM. Tusiandikie mate wakati wino upo. Hata hivyo, kikubwa si nani kasema au kubuni bali mwananchi anufaike; *(Makofi)*

(b) Kukubali ushauri wa Kambi hii ya Upinzani na Wabunge kwa jumla; na

(c) Kuwashirikisha wadau wote kwa pamoja.

Hata hivyo, kwa kawaida aliyeiga hatekelezi kama yule aliyebuni na ndiyo maana utekelezaji wa mipango kama MMEM umekumbwa na matatizo mengi. Kwa mfano, ahadi ya Serikali ya kutoa dola 10 kwa kila kichwa, kwa kila mwaka iliyotolewa mwaka 2001, hadi leo zimetolewa chini ya dola sita baada ya dola 30 kwa miaka mitatu (2001 hadi 2003). Inawezekana hata Waheshimiwa Wabunge humu bado hatuifahamu hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru na tutaunga mkono iwapo hoja hizi zitapewa maelezo kamili. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa ili niweze kutoa mchango wangu katika hizi hoja mbili ambazo zipo mbele ya Bunge lako Tukufu. Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hoja ya Waziri wa Fedha.

Kwa sababu najua muda wetu ni mfupi, naomba tu kwa haraka haraka kwanza kabisa, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote, ambao wamechaguliwa katika chaguzi ndogo zilizoendeshwa kote nchini hivi karibuni ili kuingia hapa Bungeni. Tunawakaribisha sana ili tushirikiane kufanya haya ambayo tumekabidhiwa na wananchi katika Bunge hili Tukufu. *(Makofi)*

Pili, Mheshimiwa Spika, ningependa kuwapongeza sana Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, kwa hoja hizi nzuri sana na niwapongeze wataalam wote katika Wizara hizo walioshiriki katika kuandaa hoja hizi ambazo ni nzuri na za aina yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hasa hasa kwa madhumuni ya kuipongeza bajeti ya mwaka huu 2003/2004. Baada ya mafanikio makubwa ambayo tumeyapata kwenye uchumi mpana *(Micro Level)*, nafikiri sasa ni wakati muafaka kabisa wa mafanikio hayo kuelekezwa kwa wananchi walio wengi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hao ni hao asilimia 16 ambao mpaka leo hawawezi kumudu milo mitatu kwa siku na hao asilimia 36 ambao hawawezi kumudu mahitaji muhimu kwa maisha ya binadamu yeyote yule na hiki ndicho ambacho bajeti hii imejielekeza kukifanya. Kwa maoni yangu kama bajeti hii ikisimamiwa vizuri, basi kwa kiwango kikubwa sana tutafanikiwa kupunguza umaskini uliokithiri huko Vijijini.

Nasema bajeti hii imejielekeza kufanya hivyo kwa sababu katika maeneo yote unaona dhahiri kabisa hicho ambacho Waziri amekisema kwamba, wametoa upendeleo maalum katika maeneo yote yanayolenga kuondoa umaskini huko Vijijini. Kwa hiyo, mimi naipongeza sana Serikali kwa bajeti hii nzuri sana na hayo nitakayochangia kwa muda huu mfupi nilionao kwa kweli yatakuwa na lengo la kuboresha maeneo machache katika bajeti hii ambayo kama itafanya hivyo, tutapata ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba niipongeze Serikali kwa kupunguza milolongo ya kodi na ada zilizokuwa zinatozwa na Halmashauri za Wilaya na Miji katika sehemu mbalimbali. Ni kweli kabisa kwamba, ufuatiliaji wa baadhi ya kodi hizi ulikuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi na kwa kiwango kikubwa sana ulikuwa unavuruga utulivu Vijijini na kwa hiyo kuharibu mazingira ya uzalishaji ya wananchi. Ningependa kutoa pongezi maalum kabisa kwa Serikali kwa uamuzi wa kufuta kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama imetokana na kauli za Upinzani au Chama cha Mapinduzi, nadhani tutamwachia Waziri, atalieleza hilo mbele ya safari. Lakini naamini hii ni hoja ambayo tumekuwa nayo katika Chama cha Mapinduzi kwa muda mrefu na Wabunge wa Chama cha Mapinduzi hapa Bungeni mara nyingi katika michango yao wameililia Serikali kuhusu suala hili ambalo tulikuwa tunaliona dhahiri Vijijini kwamba, lilikuwa ni kero kwa wananchi wetu. Mimi naamini ni hoja ambayo imejengwa ndani ya CCM na Serikali imeamua kuitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ambayo ni ya pongezi, naomba sasa nijielekeze katika maeneo mawili kwa lengo tu nilivyosema la kuboresha., eneo la kilimo na eneo la mifugo. Haya ni maeneo mawili ambayo Serikali imeyapa kipaumbele katika bajeti hii na imetoa upendeleo maalum katika bajeti hii kwa lengo la kuyaboresha kutokana na umuhimu wake. Nimefurahi sana kwa uamuzi ambao umechukuliwa na Serikali wa kuzitaka Wilaya kuteua mazao, zao moja la biashara na zao moja la chakula. Kwa kweli mimi hii ndiyo imekuwa ndoto yangu ya muda mrefu na ninafurahi sana Serikali hivi sasa imeiona na kwamba uamuzi huo ndiyo unaweza kutuletea ufumbuzi wa tatizo tulilonalo katika kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ni kubwa, tunalo eneo la karibu kilomita za mraba milioni moja na huwezi kutegemea hata siku moja kwamba, eti hali ya mazingira na hali ya hewa katika maeneo yote haya itakuwa ni sawa. Tunatofautiana kwa hali ya hewa, kuna tofauti za udongo na mazingira mengine ya kilimo. Kwa hiyo, kila Wilaya kutokana na mazingira yake ya kilimo italima zao linaloendana na hali ya mazingira hayo. Kwa bahati mbaya sana tulikuwa tumefikia mahali ambapo karibu wote tulikuwa wakulima wa mahindi na mimi nafikiri hili ni tatizo moja ambalo limetusababishia tatizo kubwa la upungufu wa chakula hapa nchini, ambapo wote tulikuwa tumeamua kuwa wakulima wa mahindi kwa sababu tu wote tumependa ugali wa mahindi, lakini si kweli kwamba zao la mahindi linastawi katika kila Wilaya au kila Mkoa. Kwa hiyo, nasema uamuzi huu wa kuzitaka Wilaya kila moja iteue zao la chakula na zao la biashara ambalo linaendana na mazingira ya Wilaya ile ni uamuzi muafaka sana na utatusaidia sana kama ukisimamiwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili uamuzi huu uwe na mafanikio ninapendekeza kwamba, uamuzi huu usimamiwe kisheria. Kwa hiyo, kila Wilaya itunge sheria ndogo ya kutekeleza azma hii kwa sababu naamini kabisa kama itakuwa ni kutamka hivyo tukaishia hapo, utekelezaji wake unaweza kuwa ni wa matatizo.

Mheshimiwa Spika, mapinuduzi ya kilimo katika nchi zilizoendelea zote hayakufanywa tu kwa kuhamasisha, yalifanywa kwa kutumiwa nguvu kidogo na sehemu nyingine nguvu zilitumika sana tu. Mimi uamuzi huu wa Serikali nauona ni uamuzi wenye lengo la kuleta mapinduzi ya kilimo katika Taifa letu. Kama tunataka tufanikiwe kwa kweli lazima tusaidiwe na nguvu ya kisheria na viongozi wa Wilaya zinazohusika zikishatungwa sheria ndogo hizo basi wahakikishe zinasimamiwa kikamilifu ili uamuzi huu uweze kuzaa matunda ambayo yanategemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi sana kuona kwamba fedha kwa ajili hiyo zimetengwa na ninaamini kwamba, kweli zitafika huko zinakotegemewa zifike. Kwa hiyo, kama tukilisimamia suala hili vizuri, ninaamini kabisa kwamba, linaweza kutuvusha kutoka hapa tulipo. Katika sheria hizo ndogo napendekeza vilevile suala la nguvu kazi vijijini nalo liwe miongoni mwa hayo masuala ambayo yatasimamiwa na sheria hiyo.

Kuhakikisha kwamba, kila mwenye uwezo wa kufanya kazi, anafanya kazi. Sasa hivi tunasema asilimia 80 ya wananchi wetu wako vijijini na fursa pekee waliyonayo huko ni kilimo ili kuwaondoa katika suala la umaskini. Mimi sielewi, Msemaji wa Upinzani aliposema kwamba, kuna tatizo la ardhi halali. Mimi sikuelewa. Kwa sababu bado hatuna tatizo la ardhi, kama yapo maeneo tu ambayo yana tatizo la ardhi ni machache.

Lakini labda unaweza ukafanyika utaratibu na wananchi hao wakaenda kulima maeneo mengine. Lakini mimi ninavyoelewa ni kwamba, katika ardhi inayofaa kwa kilimo katika nchi hii, tunatumia kidogo tu na iliyobaki bado iko *idle*. Kwa hiyo, hatuna tatizo la ardhi ni suala tu la kuitumia. Kwa hiyo, suala la nguvu kazi lihusishwe katika sheria hizi na vilevile suala la huduma za ugani liingizwe katika sheria hizi ili Maofisa wetu wa Ugani katika vijiji wafanye kazi ambayo inakusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ningependa kugusia suala la mifugo. Tunayo mifugo mingi katika Taifa hili, lakini nafikiri taratibu za kuihudumia mifugo hii bado ni tatizo. Tuna tatizo kubwa sana la uzururaji wa mifugo kwa sababu ya kukosa huduma muhimu katika maeneo yanayohusika. Sasa ili mifugo isiwe balaa kwa Taifa hili na kusababisha uharibifu wa ardhi katika maeneo mbalimbali, basi tuhakikishe kwamba, tunajielekeza katika kutoa huduma za mifugo ili wasizurure ovyo nchi nzima. Kwa hiyo, uchimbaji wa mabwawa na suala la nyanda za malisho vilevile lipewe umuhimu unaostahili.

Mheshimiwa Spika, ningelipenda nigusie mambo mawili tu katika bajeti hii. Suala la kuongeza ushuru wa dawa za mbu na vyandarua kutoka nje, mimi nafikiri uamuzi huo utazamwe upya. Kama uzalishaji wa bidhaa hizo nchini hapa unatosheleza mahitaji yetu, basi hilo litakuwa halina tatizo. Lakini mimi sina hakika. Kama uzalishaji hapa nchini hautoshelezi mahitaji yetu, basi hili suala inabidi liangaliwe na ikiwezekana libadilishwe, kwa sababu bado tuna tatizo kubwa sana la mbu nchini. Sasa kuongeza ushuru wa dawa hizi za mbu na vyandarua nadhani linaweza likaathiri sana jitihada za kupambana na malaria.

Vilevile kuna kipengele ambacho kimeongeza viwango vya ushuru kwa mvinyo inayotengenzwa kwa asilimia 75 ya zabibu za hapa nchini. Nalo vilevile mimi ningelipenda litazamwe upya. Kilimo cha zabibu hapa Dodoma kilikufa kwa kiwango kikubwa sana kwa sababu ya kukosa soko na ni hivi karibuni tu wamejitokeza watu binafsi wameanza kutengeneza mvinyo na hiyo imeleta soko kwa zabibu na kilimo hiki kinaanza kufufuka tena. Sasa kuongeza ushuru kama ilivyopendekezwa hapa, nadhani inaweza kuwa na athari katika hali ambayo imeanza kujitokeza ya kilimo cha zabibu kufufuka tena hapa Dodoma na sehemu nyingine ambazo wanalima zabibu. Kwa hiyo, naomba vilevile uamuzi huo utazamwe upya.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nashukuru kwamba, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya tatizo la njaa tulilonalo mwaka huu. Katika bajeti yametajwa maeneo, sasa ningelipenda niseme au

nitamke kwamba na sisi hapa Dodoma tunategemea kuwa na tatizo hilo. Kwa hiyo Serikali inapolishughulikia suala hili, basi ielewe na hapa Dodoma vilevile.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nitamke kwamba, naunga mkono hoja zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Naomba nianze kwa kuwapongeza wote waliochaguliwa hivi karibuni kuingia katika Bunge hili Tukufu. Lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini na nitamke rasmi kwamba, kazi ya kulilea Jimbo hilo nimeikamilisha na kama nilivyosema Bungeni kwamba, nitakuja na Mbunge wa CCM kwa mbwembwe, naomba niseme kazi hiyo nimeikamilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kutuletea bajeti nzuri na kusema kweli ukiangalia vigezo vya kuangalia uchumi unavyokwenda tunaona kwamba, uchumi umekua angalau kwa asilimia 6 na tunaona sasa tuna fedha nyingi za kigeni za akiba ambazo hata tukisema tumeacha biashara yoyote leo hii, tunaweza kuishi kwa miezi 7. Lakini vilevile tunaona mapato ya Serikali yameongeza kwa zaidi ya shilingi bilioni 100 kwa mwezi na ni kwa sababu ya mafanikio haya ndiyo maana kwa mbwembwe tumeamua kufuta kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo watu ambao wangependa ikiwezekana tufute kodi zote. Lakini tunasema huwezi kufuta kodi kabla hujajua utaziba vipi pengo hilo. Kwa hiyo, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi tunatambua kabisa kwamba, tunaanza kwa kuwa na uwezo wa kuweza kuziba pengo na ukishakuwa nao ndiyo unaweza ukaongelea kufuta kodi na ndiyo maana tulianza na sera ya kuongeza mapato ya Serikali na Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi tumeisimamia vizuri na sasa ndiyo maana tumeweza kufuta kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze wenzetu wa Benki Kuu, kwa sababu mwaka 2002 nilijaribu kuwatahadharisha kutoleta takwimu zinazotofautiana na za Serikali na mwaka huu nilifuatilia kwa karibu sana ile *Statement* ya Benki Kuu, nimefurahishwa sana kukuta kwamba, kwa mara ya kwanza sasa wamehakikisha wameandika yale ambayo yapo katika Bajeti ya Serikali na kwa sababu hiyo Gavana hana mgogoro tena na mimi na nawapongeza kwa kusikiliza maoni ya Waheshimiwa Wabunge na kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo ukiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, imeongelea kwamba shilingi yetu inashuka na ametoa sababu mbili. Moja ni kwamba, kasi ndogo ya mauzo ya nje na ya pili ni kushuka kwa bei za mazao asilia, iko ukurasa wa 12. Lakini ukitazama kitabu hicho hicho ukurasa wa 60 ukiangalia kwa mwaka 2000, kwa sababu mwaka 2001 mpaka mwaka 2002 shilingi yetu ilishuka kwa asilimia 7 na Mheshimiwa Waziri, akatueleza kwamba, sababu ni kupungua kwa mauzo ya nje kumechangia. Lakini ukiangalia mauzo ya nje kwa mwaka 2001 tuliuza dola milioni 776.4 na mwaka 2002 tumeuza nje dola milioni 877. Kwa sababu alizozitoa Mheshimiwa Waziri, tulitarajia fedha yetu ipate nguvu zaidi kwa sababu mauzo yameongezeka. Kwa hiyo, sababu hiyo si kweli ila kuna tatizo ambalo lazima tulitafute tatizo hilo liko wapi.

Mimi ningependa tu nishauri kidogo hapa kwamba, tunalo tatizo kwamba, baadhi ya Mabenki yanatorosha nje fedha za kigeni na kwa sababu hiyo hata uchumi wetu tukijitahidi namna gani bila kudhibiti hali hiyo fedha za kigeni zitaendelea kuwa pungufu katika soko la ndani ya nchi na kwa hiyo fedha yetu itaendelea kupoteza thamani. Kwa hiyo, nashauri wahusika walitizame jambo hilo kwa makini kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini ushauri mwingine ambao ningependa niutoe ni kwamba, tuna tatizo kwamba tunatumia fedha za kigeni kununua hata bidhaa ambazo zingeweza kupatikana ndani ya nchi. Kwa mfano, tunatumia fedha za kigeni kuagiza nyanya, tunatumia fedha za kigeni kuagiza *juice* za machungwa, tunatumia fedha za kigeni kuagiza vitunguu, tunatumia fedha za kigeni kuagiza vitu vidogo vidogo tu na hii yote maana yake ni kwamba, lazima shilingi yako itayumba.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nitoe ushauri kwamba, yapo mambo ya kutazama kwa makini kabisa na ndiyo maana hata Mheshimiwa Waziri katika jitihada za kujaribu kutueleza kwa nini shilingi inashuka, sababu alizozitumia zinapingana na hotuba yake hiyo hiyo. Kwa sababu jedwali linaonyesha mauzo ya nje yaliongezeka na sababu hizi nilizozitoa na ushauri nilioutoa, nashauri tuutazame na tuuangalie kwa makini, vinginevyo tutaendelea kuimba hapa na fedha yetu itaendelea kushuka siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yetu katika bajeti ya mwaka 2002, Mheshimiwa Waziri alisema anaondoa kodi ya *VAT* katika usafirishaji wa mazao ya biashara, pamoja na magunia na vitu vingine. Kwa hiyo, tulimpigia makofi sana ndani ya Bunge hili. Lakini baada ya kufuatilia nimegundua alichosema Mheshimiwa Waziri, sicho kilichotekelezwa. Kilichotekelezwa wataalam walisema waliosamehewa *VAT* ni wale wanaouza mazao nje ya nchi moja kwa moja, kwa hiyo, Chama cha Msingi na Chama cha Ushirika kama *KCU* hawajasamehewa *VAT* yoyote. Sasa nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, alikuwa na nia nzuri kabisa, aliwasilisha hapa na sisi tukapiga makofi, lakini watekelezaji na wasaidizi wake hawayajui hayo. Sasa hili ni jambo la hatari kabisa kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, anasema hivi, lakini watekelezaji wanatekeleza mambo mengine. Sasa ningependa katika bajeti hii basi Mheshimiwa Waziri, alifuatilie kwa karibu. Kwa mfano, ningefurahi kama akiweza kunieleza kwamba, *KCU* Chama ambacho ni cha Ushirika kinastahili kusamehewa hiyo *VAT* kwa mwaka huu tunaoumaliza kimesamehewa shilingi ngapi, akinieleza hilo nitajua kwamba imetekelezeka. Lakini ukweli ni kwamba, hilo halijatekelezwa na wataalam wake wao wanatafsiri tofauti kabisa na aliyonayo Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo naomba alifuatilie kwa karibu suala hilo.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo mengi yameelezwa kuhusu kilimo na kusema kweli kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa hili na napongeza mikakati mbalimbali iliyoonyeshwa kwamba itatekelezwa. Ukiangalia ukurasa wa 29 ni kwamba, kuwawezesha wananchi kufanya biashara zao bila vikwazo kwa kuruhusiwa kuuza mazao yao nje ya Wilaya au Mkoa hata nje ya nchi kwa taratibu rahisi na zilizo wazi. Kwa kweli hii ndiyo maana halisi ya utandawazi. Tunaposema utandawazi ni pamoja na mwananchi kuwa na uwezo wa kuuza mazao yake kokote kule anakoweza kupata soko. Swali ambalo huwa naulizwa sana kwenye mikutano yangu na wananchi ni kwa nini Mganda atoe bei kubwa na sisi ndani tunatoa bei ndogo. Swali hili huwa nalijibu, lakini naomba nikiri kwamba huwa nalijibu kisiasa mno kuliko kiuchumi. Ukiamua kulijibu kisiasa litajibika. Lakini roho yangu huwa inasema Mheshimiwa Kamala hapa pamoja na majibu haya, hapa umefanya sana siasa kuliko hali halisi.

Mheshimiwa Spika, sasa si vizuri kuendelea kuwafanyia siasa wapiga kura, ni vizuri ifike mahali tuelezane kama kuna tatizo na tulisahihishe. Sasa nimefurahishwa kwamba sasa Serikali imesema yakiwemo mazao ya biashara wananchi wanaweza kuuza kokote kule. Sasa ningependa uwekwe utaratibu mzuri kama Waganda wanaweza kupata soko zuri la kahawa, basi tuwawezeshe waje kwa taratibu nzuri waweze kununua kahawa yetu na tuweze kupata bei nzuri. Tatizo ni kwamba, unapozuia ukatumia polisi, ukatumia askari ukafanya hivyo, lakini kama kweli yule anayekuja anatoa bei nzuri hata ufanye vipi hiyo itakuwa ni kazi bure na utakachokuwa unafanya ni kutumia gharama nyingi ambazo zingeweza kutumika kufanya mambo mengine. Kwa hiyo, nimefurahi kwamba Serikali imeliona hilo na hiyo hasa ndiyo maana ya utandawazi. Tuboreshe mfumo wetu wa ndani, lakini tujaribu kufungua milango na wananchi hasa wakulima waweze kunufaika zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimefurahishwa kwamba, Serikali sasa imeongeza mara mbili fedha zilizotengwa kwa ajili ya kudhamini Vyama vya Ushirika na mpango huu ni mzuri na kwa hivi sasa ninavyoongea huko Mkoani Kagera hakuna tatizo tena la wakulima kupeleka mazao yao kwenye Vyama vya Msingi na wakashindwa kulipwa pale pale. Hii imetokana na utaratibu mzuri wa kudhamini Vyama vya Ushirika, kwa hiyo, huo mpango uendelee.

Mheshimiwa Spika, lakini ninatoa tahadhari kidogo huu Mfuko mpya wa kudhamini wakulima wadogo wadogo, wenye viwanda na wafanyabiashara wadogo wadogo, mimi nikilitazama hili naomba katika utekelezaji wake tupunguze *bureaucracy* na kweli tunaposema mkulima mdogo mdogo na mfanyabiashara mdogo mdogo awe mfanyabiashara mdogo kweli na isije ikawa vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile kuna wazo kwamba, Serikali itaanzisha Benki mpya ya kuhudumia wavuvi, wafugaji na wakulima. Sasa mimi nashauri tu kama Serikali bado inaona umuhimu wa kuanzisha benki, basi ni vizuri badala ya kuanzisha benki mpya tukachagua benki yoyote tunayoiona ipo na inafanya kazi vizuri. Sitaki kutaja Benki ipi ili nisilete mgogoro wa malumbano yasiyo na sababu. Ni vizuri basi Serikali ikatazama benki zetu tulizonazo, ikaona benki iliyo karibu na wananchi na inayoweza kufanya shughuli ikaboreshwa kuliko kuanzisha benki nyingine, halafu baadaye ikaja hoja ya kwamba, hiyo benki iliyoanzishwa haina leseni. Nilikuwa natoa ushauri tu, tunaweza tukalitazama kwa ajili ya kupunguza kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee kwa haraka suala la pensheni. Namshukuru Waziri wa Fedha, kwa kuongeza pensheni mpaka shilingi 20,000/= na vilevile kusema kwamba sasa malipo ya mkupuo hayatakuwepo, lakini akasema hakuna mabadiliko ya sheria. Ningependa nimshauri tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kuwa malipo ya mkupuo yaliwekwa na sheria, mimi nadhani haiwezekani ukayabadilisha bila sheria. Nia ni nzuri kabisa, lakini ni vizuri sheria ikaletwa hapa Bungeni ili tuifanyie marekebisho. Ningependa kumwambia tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kama ataleta sheria hiyo, basi mimi mapenzi yangu yananituma kwamba, hata wale waliolipwa kwa mkupuo wa miaka kumi na mbili na nusu, lakini kwa bahati mbaya bado wanaishi, basi wakati tunaleta sheria hiyo nitashauri vizuri tu kwamba, tuwarejeshe na wale ambao bado wanaishi kwenye daftari la pensheni. Lakini nadhani ili lisituletee mgogoro, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ataleta sheria hiyo na lazima sheria ije kwa sababu kama kitu kiliwekwa kwa sheria huwezi ukakibadilisha bila sheria. Labda nimhakikishie Mheshimiwa Waziri wa Fedha, asiwe na wasiwasi, alete tu hapa tutajadiliana na tutapata muafaka, asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tu nimalizie kwa kusisitiza jambo moja. Katika bajeti ya mwaka 2002/2003, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliongelea ubadhirifu kwenye Ushirika. Lakini siyo hiyo tu vilevile Mheshimiwa Rais, huko nyuma aliunda Tume ya *Sir George Kahama* na hiyo Tume ilitoa ripoti nzuri tu na ni kati ya ripoti nzuri kuliko zote na mimi huwa nazunguka nayo kila sehemu. Ndani ya ripoti ile inaonyesha kwamba, kufikia tarehe fulani wabadhirifu waliosababisha ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika, wangekuwa wamefikishwa katika vyombo vya sheria na kilicho kizuri zaidi katika ripoti hiyo anaonyesha ni nani mhusika anayetakiwa kufanya kazi hiyo. Sasa nisingependa kusema sana ila napenda Serikali itoe msimamo hapa.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi niihakikishie Serikali, sitapenda kuwa mtu wa fadhila kwa kuhurumia waliosababisha ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika, katika hilo mimi sipo. Ambacho nasisitiza ni kwamba, maamuzi ya kimsingi yakishachukuliwa tusiwe na tabia ya kurudi nyuma na kuanza kuwa waoga waoga, mambo magumu lazima yasimamiwe na Serikali imara na ndiyo maana tunayo Serikali imara isiyoyumba na ndiyo maana hata Mheshimiwa Waziri Mkuu, alishaagiza kwamba, wale wanaotakiwa kuwashughulikia waliosababisha ubadhirifu, basi wafanye kazi yao nilimsikia na kwa kweli sidhani kama leo atarudi nyuma na kusema sikusema. Katika bajeti ya mwaka 2002/2003, nilitoa mwaka mmoja kwa Serikali na mwaka huu ndiyo sasa unaisha. Sasa wananchi wamenituma kwamba, kama Serikali haifanyi kazi yake sasa unafanyaje. Sasa sijui nifanye nini. Lakini ningependa kurudia tena kwa sababu ninasema na watu wana masikio kwamba, tujifunze kila mtu kufanya kazi yake na tuache ubabaishaji wa maneno na kujaribu kutaka fadhila kwa kuhurumia waliosababisha ubadhirifu katika Vyama vya Ushirika, hilo sitaki kabisa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie tu kwa kuipongeza Serikali, kwa kuona haja ya kufanya mabadiliko katika sheria ya mapato na Mheshimiwa Waziri amesema ataleta sheria mpya. Labda nimkumbushe tu kwamba, kuna mapato ambayo yanapotea bila sababu ya msingi. Kwa mfano, kuna sheria moja ya kukusanya ushuru wa kwenye meli kule, sasa ile sheria ilisema watakaosafiri kwenye *vessel* watatoa shilingi 500/= na watakaosafiri kwenye *ferry* hawatoi. Lakini unakuta *ferry* inatoka Mwanza inaenda mpaka Bukoba, lakini kwa sababu imeitwa *ferry* basi hao hawalipi shilingi 500/=. Sasa namshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, hapo kuna mamilioni ya fedha yanapotea na akilifanyia kazi hilo anaweza akapata fedha. Lakini hapo hapo nimshauri vilevile Sheria ya Mapato ilikuwa ni mbaya kwa upande mwingine kwa sababu ule Mfuko wa Wakulima wa Mkoa Kagera, walioanzisha kwa kukata fedha zao kidogo kidogo na wenyewe umekuwa ukiwajibishwa kutozwa kodi. Sasa ukifanya hivyo unakuwa haumsaidii mkulima. Kwa sababu Mheshimiwa Waziri nimemsaidia hapa kumpa mapato kwa

kuonyesha mwanya wa mapato yanayopotea, nadhani vilevile atanipa fadhila sasa kwa kurekebisha sheria hiyo ili ule Mfuko wa Mazao usiendelee kukatwa kodi ambazo si za msingi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na napenda niseme kwamba, bajeti hii ni nzuri kabisa na nimalizie kwa kusema, naomba yale ambayo nimeshauri, Serikali iyafanyie kazi na hasa hili la ubadhirifu kwenye Vyama vya Ushirika. Kama Serikali inaona kazi hiyo ni ya wakulima wenyewe, itamke waziwazi na tujue huo ndiyo msimamo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie machache tu kuhusu hotuba hizo mbili za Mawaziri wetu Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kwanza kabisa, nadhani niwape hongera nyingi sana kwa *speech* ambazo wamezitoa wiki iliyopita, ni nzuri, zimetuelimisha, licha ya kutoa elimu zimechanganua pia mambo ya kitaalam na ya kiutekelezaji. Hotuba zote zimekuwa safi sana.

Pili, mimi kwa niaba ya watu waishio Songea au Jimbo letu la Peramiho na hasa Wilaya ya Songea, tunatoa shukrani za dhati kuhusu zile shilingi bilioni 4 ambazo na sisi tumepangiwa kwa wale *Big Four*, tulikuwa siku hizi tukiitwa *Big Fools*, lakini sasa tutarudi tena kuwa *Big Four*, kwa msaada huo ambao Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ametupa Mikoa ile minne kwa kuanzia na baadaye wengine pia watapata kama alivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, nina machache tu ya kuchangia kwenye hotuba hizo mbili. La kwanza kabisa, ni lile la kuwa na *planning*, sina hakika kama *planning* bado ipo, *planning* ile tuliyoipitisha siku hizo au *planning* sasa imekuwa kama Idara tu, siyo Wizara kama ilivyokuwa. Nasema hivyo, kwa sababu kulikuwa na *Commissioners* wa kudumu kule ndani, waliokuwa wanaongelea miradi na programu, ambapo Rais mwenyewe alikuwa *Chairman*, lakini wale *Commissioners* nadhani wote wameshaondoka amebaki mmoja tu, nadhani Dr. Mbogolo, hata yeye hakubaki kwenye *line* ile ambayo aliyoendea pale, naye wamemsogeza yuko kwenye kuhesabu watu. Kwa hiyo, hatuna wale *Commissioners* sasa sijui kama hiyo *planning* ipo?

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kusisitiza kuwa *planning* lazima iwepo la sivyo tutayumba baadaye hata kama tunakwenda kwenye *Private Sector*, ndiyo chombo cha maendeleo, lakini bado kitahitaji *planning* ya Serikali. Hata Marekani ambako uchumi wao ni wazi zaidi, ambao ni wa demokrasi, lakini bado wanafanya *planning* yao kupitia Ofisi yao ya Rais kule, huwa wana-*plan* hata hiyo *Private Sector*. Kwa hiyo, nadhani tufanye juhudi, tufikirie kuwa *planning* irudi kuwa *planning* kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, maana kama tutapewa mradi au programu itakayotekelezwa na Wizara mbili, tatu, nne, bila *coordinator* pale, inakuwa vigumu, huwa mara nyingi miradi kama hiyo hufa kabla haijaanza. Kwa Miradi kama hiyo, nasema kuwa mradi ule wa *Mtwara Development Corridor*, ambao ulikuwa utekelezwe na Wizara kama tatu, nne, tano hivi, Mheshimiwa Rais aliupeleka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Mkuu akautengenezea Kamati, *Interministerial Committee* ikaja na *Interstate Committee* kwa kuwa mradi wenyewe unahusisha Zambia, Malawi, Msumbiji na sisi.

Kwa hiyo, kama hizo mbili zilikuwepo *Interministerial* ya kwetu na Waziri Mkuu waliichagua Wizara ya Ujenzi kuwa ndiyo iwe Wizara itakayo-*coordinate* hiyo, lakini mpaka leo tunapofikia hapa lililofanyika tulikwenda mpaka kufikia kusaini *Memorundum of Intent* mwaka 2001 na pale ndiyo ilikuwa mwisho na haijasikika tena kama Kamati hizo zinaendelea au haziendelei. Kwa kuwa mimi nipo katika Kamati zote mbili, sijaitwa hata siku moja, yaani imekuwa mradi umeachwa tu hauna mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema kama ingekuwepo *Planning Commission* ipo kama zamani, ingelikuwa inafanya kazi ile ya kuunganisha hawa wote waliohusika na mradi huo na *Chairman* kwa kuwa ni Mheshimiwa Rais mwenyewe, angejua mapema sana kuwa mradi huo unasinzia wapi na kuwatikisa wale ambao walikuwa wanasinzia.

Kwa hiyo, Tume ya Mipango nawashauri irudishwe, wairudishe kwa nguvu zaidi na ifanye kazi ile iliyopangiwa kufanya, hata kama wakifanya *modification*, siyo lazima wawe Makamishna kule katika Wizara, lakini irudi kuwa Wizara ya Mipango, pamoja na kazi hizo nyingine ilizopewa. Nadhani hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka kuongelea habari ya barabara na madaraja. Sasa barabara na madaraja yametajwa vizuri sana katika *paragraph* ya 43 kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ametaja Mikoa yote, zote hizo ni barabara nzuri tu na nyingi zinapita Tanzania na Tanzania tunaweza kufaidi zaidi ikiwa tukipanga miradi yetu ya barabara kwa mfumo wa *East African Community*.

Lakini tunaona kama tuna aibu aibu hivi, tunaacha tu tunataja tu zile za kupitia *Western part of country* kuanzia Uganda kwenda mpaka Zimbabwe. Halafu tumebaki na zile tu ambazo tulikuwa nazo tangu wakati wa *concept of sense road*.

Lakini mimi nataka niongeze pale kwenye orodha ile ya barabara, niongeze tatu nyingine, nazo ni barabara ya Pwani kuanzia Horohoro kuja Tanga, Saadani, Bagamoyo, halafu tuje Dar es Salaam twende Lindi, Mtwara, twende Pemba, ya Mozambique ili barabara hiyo ihudumie nchi zote za *Southern Africa* na *South Africa* mpaka itokee Durban na Capetown.

Hivyo barabara kubwa sana, lakini pale nimeona iko kimya kabisa. Wakati mmoja ilitajwa tajwa lakini katika *plan* zetu tunaona iko kimya. Ningependa hiyo iwepo.

Halafu ya pili ile ambayo ni Cesil Rhodes ya kutoka Cairo hadi *Cape Town or Cape Town to Cairo*. Na *link* hiyo ilikuwa itoke Nairobi na ije ya Arusha, Dodoma, Iringa na Makambako. Kutoka pale ile ya kwenda Kusini ya *traditional* iwepo lakini *I will suggest* pia ile iendelee kutoka Makambako iende Songea. Halafu Songea, Lichinga iingie *Maputo Corridors*. Na itakuwa na barabara ya pili hapo kutoka *North* kwenda *South*. *Corridors* hiyo tu zitoke Mashariki kwenda Magharibi, zinaweza kutoka Kaskazini kwenda Kusini.

Barabara ya tatu nilidhani kuwa nayo muhimu sana ni ile ya kutoka Musoma kuja Mwanza, Tabora, Sikonge, Chunya ikaingia Mbeya na Mbeya ikakutana na ile barabara kuu inayokwenda huko Kusini. Nako pia pale Mbeya kuna barabara muhimu ya kwenda Malawi ambayo tumeiacha tu ipo lakini hatuitunzi sana kama vile ni barabara kubwa kwa ajili ya Afrika ya Mashariki na Kusini. Kwa hiyo, ninayotaka kuhimiza hapa kuwa barabara ya kwetu sisi na baadaye reli kwetu sisi itakuwa ni kitu cha kutilia mkazo kwa sababu kwetu sisi ni daraja kwa nchi za Afrika Mashariki na Kusini, *SADC* na *East African Community* zitakuwa. Kwa hiyo, njia hizo za kutoka Kaskazini kwenda Kusini pamoja na barabara na reli zake lazima tuzifikirie kwa makini na kwa mahiri zaidi kusudi tuweze kwenda huko. *(Makofi)*

Sekta ya tatu ambayo nilitaka kuiongelea ni sekta ya nishati iko kwenye para ya 47 ambapo tumejaribu kuongelea. Nishati mbadala kuna maneno mengine hata sielewi ni kitu gani lakini yote hiyo katika harakati za kutafuta nishati ya kutosheleza. Mimi nadhani katika firka zetu ni vizuri kufuata urahisi au kukimbilia pale ulipo umeme na kuuleta. Lakini hatujaweka nguvu ili kutengeneza umeme wetu na sisi ikawa ni zao pia la kupeleka nchi jirani. Kwa hiyo, tukiona matatizo yanatokea Kagera tunasema tutaleta umeme kutoka Uganda. Matatizo yakitokea Mkoa wa Kigoma tunasema tutaleta umeme kutoka Burundi ingawa hata Burundi yenyewe sijui kama umeme wao unawaka au wako *busy doing other things*.

Tatu, ni kuwa Sumbawanga tutaleta umeme kutoka Zambia na tumeleta, lakini sisi wenyewe tunavyo vyanzo vya umeme ambavyo tungetilia mkazo tungekuwa na nafasi kubwa ya kuwa na hilo. Pia sisi tuta-export. Kama M-*South Africa* anataka kupitia Tanzania kwenda Kenya kuuza umeme, sisi tuko hapa kwa nini tusiwe wa kwanza kusema kuwa kwanza tutengeneze wa kwetu ili tuweze kupeleka Kenya kama peke yetu au pamoja na Wa-*South Africa*. Kwa hiyo, nilitaka kwa mfano mkaa wa Mchuchuma *(Mchuchuma Project)* maana nisingetoa *speech* bila kutaja Mchuchuma. Mchuchuma ikiwepo inaweza

kwenda na kuendeshwa ikawa na *megawatts* zaidi ya 2,000 kwa mkaa uliopo Mchuchuma wenyewe na jirani yake.

Halafu *Stigler's Gorge* walishatufanyia kazi nadhani Denmark miaka 20 iliyopita. Nao walisema 1600 sasa 2000 na 1600 *megawatts* nadhani Wa-*South Africa* walifurahi sana kufanya *Inter-connector* wao wenyewe kuliko kupitia mgongo wa Zambia. Sisi tungeweza kuwa na umeme wa kuwapelekea wazito kama Zambia, Nairobi ambao wanahitaji umeme kwa sasa hivi. Kwa hiyo, nilidhani kuwa jambo la umeme tulifanyie bidii na juhudi maalum katika kulipanga na kulitekeleza, tusiache tu kama ilivyo sasa. Kwa kuwa gesi ndio zao unaweza kutengeneza kitu kingine *fertilizer chemicals,* zaidi *fertilizers* na kadhalika kuliko kuunguza. Nadhani kuunguza ule mkaa ambao uko zaidi ya tani bilioni moja hapa nchini nina hakika zaidi. Lakini gesi kwanza sina uhakika na wale tunaowaita wahisani maana wao wamebadili wameuziana ile sehemu yao kule Wacanada waliwauzia Wamerikani na Wamerikani waliwauzia Kampuni moja sasa nasikia Kampuni hiyo nayo sasa imeuza. Sasa hatujui *partner* wetu ni nani au tuna-*keep take* ya mauzo hayo yote itakuwa Waziri bila shaka atasema anajua anafuatilia na ana-*change* kila siku. Nadhani hilo niliseme kwa upande wa nishati.

Kuhusu Wizara ya Fedha hilo nitalitilia mkazo kwa kuwa shida yetu hasa ni umeme katika mikoa ile ya Kusini na Kusini Magharibi halafu na *West Kigoma*, Kagera nadhani utiliwe mkazo kwa Wizara ya Fedha na Nishati ambao wote wananukia kifedha maana huyo wa Nishati ametokea Fedha wanaweza kupata msaada fulani kutoka nje au mikopo laini ya kuweza kufanya umeme upatikane sehemu zile ambako hamna umeme. Kweli ukienda Kusini mwa Dar es Salaam na Morogoro ni giza tu hamna umeme toka Lindi, Mtwara na Ruvuma na ukienda zaidi ya Mbeya upande wa Sumbawanga kwenda Kigoma mpaka Kagera hamna umeme ni giza tu. Ingekuwa tuwashe tungeona giza tu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, hawa wawili wakae pamoja, wataalamu wao wafikirie kazi hiyo iwe kubwa na nene kusudi sisi pia tupate umeme maana bila umeme teknolojia tunayoiongelea leo *Commerce, Government* na *people* haitakuwepo, hatuwezi. Kwa hiyo, nafuu tupate umeme na viwanda hivyo tunavyosema ni vidogo vya kati na vikubwa. Kule tutakuwa wa mwisho kupata maendeleo hayo ya viwanda na suala la *IT* ya siku hizi hatutapata mpaka tupate huo umeme. Kwa vitu hivyo viwili umeme ni kama barabara. Siku hizi ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu pamoja na sehemu hizo nzito nilizozitaja hazina umeme. Kwa hiyo, namalizia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia. Ahsante sana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani nyingi sana kwa kunipa nafasi nianze kuchangia hizi hoja mbili ya Mipango pamoja na Bajeti ya Serikali.

Kwanza nianze kwa kumpongeza Waziri wa Mipango, Waziri wa Fedha na wasaidizi wake pamoja na Watendaji wote kwa kuandaa Bajeti nzuri ambayo kwa kiasi kikubwa ikifuatwa na kutekelezwa itaondoa kero nyingi sana kwa wakulima, wafanyakazi na hata wafanyabiashara. Vile vile niipongeze Serikali kwa kuwa na akiba ya fedha za kuweza kununulia vitu kutoka nje kwa miezi sita ijayo, lakini hicho ni kiasi kidogo tujitahidi kukusanya fedha nyingi zaidi tuwe na akiba ya kununua hata kwa miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, nimeipitia kwa undani sana Bajeti hii, mimi naomba nianze kuongelea sekta ya kilimo. Bajeti imeonyesha wazi kwamba inataka kuwasaidia wakulima na kama tunavyosema Kilimo ndio uti wa mgongo hapa nchini kwetu. Lakini ningependa kumwambia Mheshimiwa Waziri wa Fedha sasa hivi kuna njaa maeneo mengi hapa Tanzania na hii njaa haikuja kwa sababu wananchi wetu walizembea kulima, la hasha. Hii ni hali ya hewa. Chakula kinunuliwe kuanzia sasa kipelekwe karibu na wakulima katika maeneo yote ambayo yana njaa tusisubiri mpaka watu waanze kuhangaika na kuitukana Serikali. Chakula kisogezwe kwenye Wilaya zote zile ambazo zina njaa ili wananchi waweze kukinunua. Mimi nina imani wengi wana uwezo wa kujinunulia chakula chao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Kilimo, Mheshimiwa Waziri vile vile nimpongeze kwa Serikali kutoa misaada kwa hii mikoa minne kupeleka pembejeo, mbolea na mambo mengine kwa ajili ya kuzalisha mazao ya kutosha ili kulisha nchi yetu. Mimi najua mwaka huu Mikoa hiyo imepewa kwa kuanzia tu, mwaka unaokuja mikoa mingine itaongezwa ili mikoa itumie vizuri zile mbolea na mahitaji mengine itakayopewa. Serikali ina kugeuka mwakani wasitegemee watapewa kama mwaka huu. Kwa hiyo, mimi nawaomba watumie vizuri na walime chakula cha kutosha ili tuepukane na njaa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri amezungumzia mengi sana kusaidia Kilimo chetu. Kwa kweli wakulima wetu wako tayari kulima mazao ya biashara, mazao ya chakula lakini ni lazima Serikali ishikilie agizo lake. Mheshimiwa Waziri ametuambia kwamba kila Wilaya itafute zao moja la biashara ambalo litawekekewa mkazo. Mimi naunga mkono hata kwa Wilaya zingine zina mazao mawili au matatu lazima kuna moja watalipa kipaumbele. Mimi nikiongea mikoa hii ya kati mkoa ninaotoka mimi Singida, Dodoma, Iringa, Morogoro, Shinyanga sasa hivi wengi tunalima zao la alizeti na wananchi wamejitoa kulima kweli kweli.

Mwaka huu pamoja na hali mbaya ya ukame lakini wananchi watavuna alizeti nyingi sana. Tatizo la mikoa yetu hii ushirika bado kuanzisha vyama vya ushirika vipya. Naiomba Serikali iweke mkazo, ipeleke Maafisa Ushirika kule na isaidie kutafuta soko la mazao haya. Mimi nashukuru Serikali mwaka jana wananchi wetu waliuza, ingawaje walikuwa wanauza moja moja, lakini bei haikuwa mbaya sana. Lakini sasa hivi kuna mdudu ameingia, kuna watu ambapo hawapendi wakulima wetu wanaozalisha mazao yanayotoa mafuta kama vile alizeti, pamba na mengine bado wanaibana Serikali, wanaizungukia Serikali ipunguze kodi kwa mafuta yanayoagizwa kutoka nje kwa ajili ya chakula. Sisi tunaomba Serikali kwa sababu imeamua kuwasaidia wakulima wake isikubaliane na hao watu wachache. Kama kuna baadhi ya Wabunge wenzetu ambao wanaungana mkono na hao watu, tunaomba wakome mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tunataka kumjenga mkulima wetu ili aweze kujitegemea, auze mazao yake na hatimaye tuondokane na umaskini. Kwa hiyo, mimi naomba Serikali isikubali kulegeza masharti waende kwa wakulima wanunue mazao kutoka kwao. Hali ya hewa ya nchi yetu si nzuri. Mimi nashukuru Serikali hata kwenye Bajeti hii wameandika kwamba wataanzisha na kusaidia umwagiliaji hasa ule umwagiliaji wa asili. Sisi tunaomba sana kuna maeneo mengi ambayo yanaweza yakafaa kwa umwagiliaji. Mimi niipongeze Serikali kwa sababu *IFAD* imeenea mahali pengi na hata Wilayani kwetu imefika. Kwa hiyo, tunaomba Kilimo cha umwagiliaji kiwekewe mkazo zaidi.

Mheshimiwa Spika, upande ule ule wa Kilimo kuna mifuko ambayo ilianzishwa na Serikali kwa nia njema ya kusaidia wakulima. Nikianza na mfuko wa *Import Support* sasa hivi Watanzania wengi hawafaidiki. Ule mfuko bado unatumiwa na matajiri na wafanyabiashara wakubwa hauendi kule kwa walengwa. Hauendi kule kwa sababu ya masharti yake magumu. Mwanzo ule mfuko ulikuwa na masharti kidogo nafuu, lakini sasa hivi hali ni mbaya sana. Mkulima alipe asilimia 30 ya mkopo anaopewa na aweke dhamana atatoa wapi? Mimi napendekeza Waziri wa Fedha akae na watu wake afikirie hiyo badala ya asilimia 30 tulipe asilimia 10. na badala ya dhamana hiyo mali inayoagizwa ndiyo iwe dhamana. Watu wanaagiza matrekta, wanaagiza malori kusaidia wakulima hizo ndio ziwe dhamana. Mimi ningeiomba tukitaka kujikomboa kwa kweli ni lazima tufanye hivyo. Sasa hivi vibali vinatoka lakini vinaishia kwenye mikono ya matajiri sitaki kutaja matajiri wa aina gani, lakini matajiri ambao hata hawaendi kule vijijini kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mfuko mwingine huu wa Japan na Tanzania unaohusu chakula. Huu mfuko umekuwa unasaidia sana na mimi nasikitika sana kuona mchele umeshaagizwa kwa ajili ya uzembe wa watu wachache huo mchele mpaka sasa uko bandarini na ukitoka utakuwa umeharibika. Mimi ningeiomba wale watoa tenda wanaosimamia huu mfuko waangalie. Hivi haya yanayotokea, kesi ziko Mahakamani si ajabu kuna harufu ya rushwa ilitembea mle. Kwa hiyo, sisi tunaomba usirudie tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema juu ya mfuko huu kwa sababu huu ndio mfuko pekee ambao unasaidia wananchi kule kwenye Wilaya zetu. Unatoa fedha kwa ajili ya kuchimba mabwawa, maji, kujenga mashule na kuendeleza Kilimo. Huu ni mfuko ambao hauna mizengwe kabisa na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na hasa wale walioko kwenye huu mfuko. Kazi inayofanya inaonekana na tunaomba waendelee nayo.

Mheshimiwa Spika, nikiendelea na kuchangia humu kwenye hotuba ya Waziri ameongelea juu ya balaa ya UKIMWI lakini hakuongelea kwa undani zaidi. Kwa kweli sasa hivi nguvu kazi yetu inakwisha. Mimi bahati nzuri niko kwenye Kamati ya *LAAC* Wilaya zote tunaziuliza kama wametenga fedha za UKIMWI, hakuna Wilaya hata moja. Wanategemea wapate fedha kutoka Serikali Kuu. Kwa hiyo, mimi ningeiomba Serikali iweke umuhimu wa kupambana na hili gonjwa la sivyo baada ya muda mfupi

hatutakuwa na nguvu kazi. Niwapongeze *TACAIDS* wanatoa fedha lakini kule Wilayani hata sasa haieleweki zile fedha zinatumikaje. Kwa hiyo, Serikali inapotoa fedha ihakikishe inafuatilia na matumiziyake ili yaende kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika vile vile niipongeze Serikali kwa uamuzi wake kwa kutumia fedha zetu wenyewe kujenga barabara zetu. Sasa hivi barabara ya Dodoma hadi Manyoni imeshaanza, Manyoni hadi Singida imeshaanza, Shelui hadi Nzega imeshaanza, Singida hadi Shelui itapata fedha hivi karibuni na itaanza. Barabara za Kusini Somanga kwenda Mnazi nazo zimeanza kwa kweli mimi niipongeze sana Serikali kwa hilo. Aidha tuweke mkazo na hii ndiyo njia pekee yake itakayotukomboa sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mengi ambayo Bajeti hii imeelezea na hasa kwa watumishi wetu. Waheshimiwa waliopita wamezungumza juu ya kuondoa kero za watumishi hasa weale wanaopata pensheni. Bado mpaka leo watu wana shida kweli kweli. Kila mwaka tumekuwa tunaomba hizi pensheni zilipwe kikanda. Wananchi wetu bado wanaumia sana. Mtu anatoka Kigoma anakwenda Dar es Salaam ambapo angetoka Kigoma akaenda Tabora au Mwanza au hata akaja Dodoma inarahisisha zaidi. Mimi naiomba Serikali isichoke juu ya hili iendelee kusaidia ili wastaafu wetu wasiendelee kuipaka matope au kuisema vibaya Serikali. Hili jambo linawezekana kabisa na sasa hivi mmeanzisha mtandao wa kompyuta, mambo yote yangeweza kufanyika huko huko tuliko.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Bajeti hii sasa ndiyo ya ukombozi na ndiyo inatimiza Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi (CCM). Kwa sababu inatimiza Ilani ya Uchaguzi mimi nitaiunga mkono mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nianze kwanza kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hizi mbili zilizotolewa na Waheshimiwa Mawaziri wetu wawili inayohusu Mipango na Fedha katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo.

Msemaji aliyepita yeye amemalizia kwa kuiunga mkono Bajeti hii akisisitiza umuhimu wa utekelezaji wa sera za Chama cha Mapinduzi ambacho ndicho kinachoongoza Serikali ya Tanzania. Sasa mimi ninaanza kwa kuiunga mkono Bajeti hii asilimia mia kwa mia. Baada ya kuiunga mkono Bajeti hii ninaomba pia nichukue nafasi ya pekee kuwapongeza Wabunge wote wapya waliojiunga pamoja nasi katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nina imani tutashirikiana nao vizuri na hasa wale wa Chama cha Mapinduzi ambapo wamepita na kuja kushirikiana pamoja nasi. Pamoja na pongezi hizo ninaomba nichukue nafasi nyingine ya pekee kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni historia katika nchi ya Tanzania Bajeti ya mwaka huu kwa kweli imeonyesha historia ya ajabu na inaonyesha kabisa kwamba majukumu ya Serikali yetu sasa yanaanza kuonekana wazi katika dhana ya utekelezaji na sio maneno. *(Makofi)*

Baada ya kupongeza juhudi za Serikali yetu basi sasa ninaomba nijiingize katika suala zima la kutoa michango yangu kuhusiana na Bajeti yenyewe. Namna ilivyowekwa Bajeti yetu kwa kweli imeanza kuonyesha ni kwa kiasi gani tunaelekea sasa kutambua maeneo ambayo ni maeneo husika kabisa yenye kuweza kutoa mchango wa moja kwa moja wa kusaidia kuongeza pato la Taifa na hivyo basi kusaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza adha ya umaskini ambayo imekuwa ndiyo sera kubwa ama wimbo wetu mkubwa wa kujinasua kutoka katika uchumi tegemezi.

Mheshimiwa Spika, nikifuatilia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango amejaribu kulinganisha juhudi za sekta mbalimbali katika kupambana ama kuleta maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania, lakini nilivutiwa zaidi katika kipengele alichokuwa anajaribu kutolea taarifa kuhusu sekta ya uzalishaji na katika hasa sekta ya Kilimo inaonekana kabisa ni kama vile kwa kiasi kidogo juhudi zetu zilionekana kushuka kwa sababu katika mwaka uliopita, mwaka 2002, sekta hiyo ilikua kwa asilimia 5.0, ikiwa ni pungufu kidogo ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 wa mwaka 2001. Lakini mimi nasema kwamba hili si tatizo na sasa hivi Bajeti yetu imejielekeza zaidi katika sekta ya Kilimo ninaamini kabisa uko uwezekano mkubwa wa uchumi wa nchi yetu kuongezeka kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninapozungumza uchumi na hasa katika sekta ya kilimo pia ninaomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na hasa

Wanawake ambao ni wazalishaji wakuu wa sekta ya Kilimo kwa kuweza kupewa ruzuku ya pembejeo ili kuinua kiwango cha uzalishaji wa mazao. Suala la umaskini linagusa kabisa, tumeona kabisa katika viashirio vinawagusa maskini wengi ambao wako vijijini na kwa kuwa ongezeko la watu linaonyesha kabisa kwamba Wanawake ni wengi, hatuna budi kuwazingatia Wanawake maskini na ambao ni wengi na hasa wale wanaoishi katika maeneo ya vijijini. Kitu cha msingi sasa hivi ni kuhakikisha asilimia kubwa ya fedha inayopatikana katika makusanyo mbalimbali inawafikia walengwa wenyewe na wahitaji yao na nimewataja kuwa wengi wao ni wale wanawake walioko vijijini. Walengwa wenyewe ama wahitaji yao, basi ni wale maskini wa kipato na maskini wa hali na wengi ni wale wanaoishi katika maeneo ya vijijini. Basi kama hilo tutaweza kufanikiwa, ina maana tatizo la umaskini litapungua sana na hivyo basi nchi yetu itaendelea kujiongezea pato katika Taifa na hivyo uchumi utazidi kuongezeka siku baada ya siku.

Ukuaji wenye wigo mpana wa sekta zinazogusa umaskini moja kwa moja bado umejionyesha kwamba ni tatizo katika maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu. Kumekuwa na mipango ya ujumla ya Kitaifa ya kuhakikisha kwamba nchi yetu inasimamia suala zima la maendeleo. Lakini kwa kweli ninaunga mkono maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwamba haitoshi kuwa na mipango ya kijumla tu ya kuhakikisha kwamba tunapambana na umaskini na kuleta maendeleo katika nchi yetu. Ni kweli kabisa kwaamba hatuna budi sasa tuanze kuangalia tunawezaje kubadilisha historia na tabia ya maisha ya Mtanzania katika hali ya kawaida iliyozoeleka kwenda katika mabadiliko yatakayomwezesha Mtanzania kutambua ni nini kinachopasa kufanyika ili aweze kujinasua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sana wenzetu wa Mipango wajaribu kuangalia ni namna gani tunaweza kutumia nguvu kazi zinazopotea bila kuratibiwa katika mfumo wa familia na kuziingiza katika uzalishaji ambao utasaidia kupambana na umaskini. Sasa hivi si ajabu ukakuta kwamba familia nyingi ambazo ni maskini na zilizopo katika asilimia hiyo ya kumi na tisa ni zile ambazo hakuna mahusiano bora ya kijinsia kati ya baba na mama na watoto na hivyo kuratibu shughuli zote za uzalishaji na kujipangia Bajeti za kuweza kujinusuru kimaisha na hivyo basi kuondokana na umaskini katika familia hiyo. Umaskini ni ugonjwa na tatizo la ugonjwa wa umaskini ni kwamba unamvaa mgonjwa mwenyewe na hauambukizi kwa jirani wala rafiki. Nyumba yangu ikiwa na ugonjwa wa umaskini wa kula sio kwamba na jirani yangu lazima augue ugonjwa huo. Kwa hiyo, mimi nasema tunayo nafasi nyingine ya kutumia basi wataalamu wetu kuona wanawezaje kutoa mchango wa karibu sana kusaidia majukumu hayo ya kutumia nguvu kazi tulizonazo katika kuboresha uzalishaji ndani ya familia na kuendelea katika vijiji kama tulivyoainishiwa katika hotuba yetu na hatimaye nchi nzima ya Tanzania. *(Makofi)*

Ni ruzuku ya asilimia 100 au ruzuku ya asilimia 20 ni kiasi gani? Ili tusije tukashangalia tu kumbe ruzuku imepewa 1% au 5%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kutakuwa na mpango gani wa kuendeleza katika mikoa mingine kwa mfano, Mkoa wa Tabora ni maarufu sana kwa kilimo cha tumbaku. Tumbaku lazima unapolima uweke mbolea, usipoweka mbolea huwezi kupata mavuno ya kuridhisha. Wakulima wanaweka mbolea ya kiasi cha mifuko 4 kwa ekari moja, bado hujaweka *thiodani* na gharama zingine zote kiasi ambacho katika ekari moja unapata angalau kilo 500. Lakini katika nchi zingine wanapata zaidi ya hapa kwa sababu ya matumizi ya mbolea ya kupandia. Je, Serikali ipo tayari vile vile kusaidia katika mazao makubwa kama hili la Tumbaku ambalo linaingiza pato kubwa katika nchi hii? Vile vile katika Bajeti yake Mheshimiwa Waziri ameongelea sana kodi ya mbolea katika tumbaku. Je, Serikali nayo itakumbuka kusaidia wakulima wa tumbaku lini? Nilikuwa na hilo kwa upande wa mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande mwingine ambao nataka kuchangia ni upande wa mipango. Waziri ameeleza kutokuwa na maeneo maalum kwa ajili ya wawekezaji. Amesema wawekezaji watapewa nafasi ya kumiliki mashamba makubwa, lakini nchi hii ni nchi ya Wakulima na asilimia 80 ni Wakulima. Ni maeneo gani hayo ambayo Serikali imeyatenga ambako hayatawaingilia Wakulima wetu na kuwafanya vibarua? *(Makofi)*

Kwa sababu unaweza ukachukua maeneo yote ambayo ni mazuri mazuri tukawapa wawekezaji, lakini wawekezaji wakubwa katika nchi ni Watanzania wenyewe. Watanzania tumewaweka namna gani kuwawezesha ili waweze kujiwezesha wenyewe kuendeleza nchi yao? Hawa wakulima wakubwa watakaokuja watakuja kwa ajili ya biashara, watalima vizuri, watavuna vizuri, lakini kikubwa kitakachokwenda kitakwenda kwa ajli ya faida yao.

Sasa ni maeneo gani ambayo yametengwa kwa ajili ya wawekezaji na ni vijiji gani hivyo basi ambavyo vimewekwa ili tuweze kujiandaa ili tuweze kuwapokea hao wawekezaji? Lakini nilikuwa nashauri tuwapeleke mahali ambapo bado kabisa hapajamilikiwa na wakulima wetu. Vinginevyo tutaanzisha fujo ya kugombana na wawekezaji na fujo ya kuwafanya wakulima wetu wawe vibarua na manamba na pia kuwafanya watu wanaohangaishwa.

Mheshimiwa Spika, lingine siwezi kabisa nikakaa kimya bila kutaja madini. Tanzania inasifika sana kwa kuwa na raslimali ya madini mengi, ikiwemo dhahabu, almasi na *Tanzanite* kama alivyotaja Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Lakini takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania mwaka jana imeweza ku-*export* Dola za Kimarekani shilingi 400 milioni. Je, katika hizi Tanzania imepata shilingi ngapi? Ukijiuliza hapo Tanzania ilichopata ni mashimo na huruma ya bure, hakuna ambacho tumepata kutokana na madini kwa sababu hata ile huruma tuliyonayo imezidi kiwango. *(Makofi)*

Kwa mfano sisi Tanzania tunapata mrahaba wa asilimia 3%, lakini nchi zingine ambazo zimeendelea katika suala la madini wako mpaka asilimia 6%, 10%. Sasa kwa nini wawekezaji wengi wasije kuvuna kwetu hapa na wakasifia Tanzania ni nzuri ya uwekezaji mzuri, wanasifia hivyo kwa sababu faida yote wanayopata wanaichukua wao, sisi wanatuachia mashimo. Sisi wanatuachia *inflation*, sisi wanatuachia kukosa nguvu katika maeneo yetu ambako madini yanatoka. *(Makofi)*

Zamani tulivyokuwa wachimbaji wadogo wadogo, maeneo yaliyokuwa na uchimbaji wa madini yalikuwa na nguvu ya kiuchumi ya kununua. Lakini walipokuja hawa wawekezaji kwa sababu kila kitu kimebanwa kimekuwa na wawekezaji wakubwa, wale wawekezaji wadogo hatujawaendeleza, hatujawapa mitaji basi maeneo yote yamekaa bila nguvu ya kununua. Nafuu za kodi hizi kwa wawekezaji zinazoendelea kwa muda wa miaka 3 mpaka miaka 5 ni mwanya mkubwa sana ambao ungefanya tungepata uchumi mkubwa. Sasa kwa kuruhusu kufanya hivi wanaanza kuchimbua pale ambapo ni pazuri, ambako pako *concentrated.* Sehemu mbaya wanaacha wanasubiri ruhusa hiyo ya miaka mitano itakapokwisha ndiyo waanze kuchimba ambako ni hafifu ili waanze kulipa kodi kidogo. Hii ni hatari, wanatufanya sisi tuwe waangaliaji tu, tunasema tunaangalia na dhahabu tunayo nyingi, almasi tunayo nyingi ni kazi bure. *(Makofi)*

Naomba hili tulitazame upya Mheshimiwa Waziri kwa sababu baada ya miaka mitano wataondoka. Tutazame upya sheria zetu, ili tuweze kuzibadilisha kulingana na nchi zingine zivyofanya juu ya hawa wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii. Awali ya yote ningependa nichukue nafasi hii kwa kuwapongeza Wabunge wote waliochaguliwa. Pili napenda nichukue nafasi hii vile vile kuwapongeza watoa hoja kwa kutuletea taarifa nzuri sana katika kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda sasa nianze kuchangia kwa ufupi tu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kwanza kabisa naunga mkono hoja hizi moja kwa moja hasa kwa mambo ambayo mimi ninadiriki kusema kabisa kwamba hayawajahi kutokea kabisa katika mtazamo wetu wa Serikali, tangu tuanze mfumo wa vyama vingi. La kwanza kuondoa Kodi ya Maendeleo, pamoja na kodi nyingine ambazo zimekuwa ni kero kubwa sana na ni zinasababisha usumbufu katika ukusanyaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wapinzani wanasema ni sera yao. Mimi nadhani si sahihi kwa sababu mwaka jana Serikali, iliondoa ada za shule ya msingi je, hiyo ilikuwa ni Sera ya Vyama vya Upinzani? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, mimi nadhani huu ni mtiririko wa utekelezaji wa Sera ya Chama cha Mapinduzi, katika kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wetu.

Kwa hiyo, Chama cha Mapinduzi kinaendeleza baada ya kuondoa ada na matokeo yake ambayo hata Wapinzani wameyaona, sasa inafikia hatua ya pili nayo ni muhimu na itakumbukwa kwamba suala la hizi kero Mheshimiwa Rais amewahi kuzungumza katika Bunge hili hili kuhusu kero ambazo zimekuwa zikisababishwa na Watendaji wa Kata na Vijiji na ndiyo kwa sababu hiyo akaamua kutekeleza kwa vitendo, kuwalipa watumishi hao mishahara moja kwa moja. Je, hiyo ni Sera ya Wapinzani? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu hii kwa kweli ni kazi ya Waheshimiwa Wabunge, ambayo iko kwenye Katiba ya kuishauri Serikali. Wabunge wengi humu ndani ni wa Chama cha Mapinduzi na wanaishauri Serikali yao na Serikali yao inakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi naamini kabisa kuna kero nyingi tu. Wenzangu wamezungumzia kero ya nishati na kwa kawaida siwezi kuchangia bila kuzungumzia kero ya nishati katika Bunge hili. Mikoa ya Kusini, Mikoa ya Magharibi na maeneo mengine bado yana matatizo makubwa ya umeme.

Lakini ninafarijika kwamba katika Bunge hili hili tayari Wizara ya Nishati na Madini, imeshaahidi kwamba itakapofika mwaka 2005 miji yote ya Wilaya itakuwa imepata umeme na naamini kabisa ahadi hii, itatekelezwa kwa sababu Chama cha Mapinduzi na Serikali yake wana tabia ya kutekeleza ahadi zao kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kusema hayo ningependa sasa nianze kuchangia jambo lingine ambalo ni zito sana nalo ni kutoa ruzuku kwenye sekta ya Kilimo hususan pembejeo. Suala la kilimo kama ilivyoelezwa katika hotuba hii ni suala la kufa na kupona. Mimi ningependa nichukue nafasi hii, kuipongeza sana Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Mbinga, kwamba ndoto hii ambayo tumelalamika sana sasa imekuwa ni kitu ambacho kimefikiriwa. Lakini rai yangu ni kwamba pembejeo hizi zije kwa wakati muafaka, zije mapema. Nataka niwahakikishie kwamba kwa wananchi wa Mikoa ya nyanda za juu na hasa wa Mbinga, kulima siyo tatizo, watalima na mtashangaa, lakini tatizo letu ni masoko.

Je, Serikali inajiandaa vipi hasa kuhakikisha kwamba tunapata masoko ya uhakika hasa nchi za nje?

Mheshimiwa Spika, juzi nilikuwa nawasiliana na watu wa China, wameniambia kwamba China kuna soko kubwa la kahawa. Waganda wamekwishaingia wamefungua tayari migahawa ili kuwafanya Wachina waanze kunywa kahawa kwa wingi na mwelekeo umekuwa mzuri sana. Je, Wizara ya Ushirika na Masoko italitazama hilo? Ningependa kupata jibu.

Mheshimiwa Spika, lakini suala ambalo pengine linaweza likasumbua sana utekelezaji ni suala la usalama wa nchi yetu. Pamoja na juhudi hizi zote usalama nadhani ndiyo jukumu kubwa sana la Serikali. Hivi sasa kuna wimbi la ujambazi kutoka nchi jirani. Lakini zipo taarifa ambazo kwa kweli sisi wenyewe tunachangia kwa namna moja au nyingine au pengine ni kwa sababu ya jiografia ya nchi yetu.

Lakini zaidi ya hapo zipo taarifa kwamba asilimia zaidi 90 ya watumishi wa ndani Jijini Dar es Salaam na miji mingine nchini wanaofanya kazi hata kwa wakubwa na wafanyabiashara wanatoka nchi jirani na hao siyo raia. Sasa najua hali siyo ya kufurahisha lakini ni vizuri tukasema hapa kwamba kama tutaendeleza mwenendo huu tujue kabisa tunajimaliza sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi rai yangu ni kwamba sasa hivi Dar es Salaam tumeambiwa kuna msako na Mkuu wa Mkoa amekuwa mkali sana. Amekuja na mikakati mizuri, ninampongeza.

Lakini mimi nadhani kama hatapata ushirikiano kutoka kwa viongozi wakubwa na wafanyabiashara, basi juhudi zake zitakuwa ni nguvu za soda. Lakini hazitakuwa nguvu za soda zitakuwa kwa kweli ni kifo. Tutakuwa tunajichimbia kaburi sisi wenyewe. Kwa hiyo, mimi ningeomba kwamba Watanzania kwa kweli tufike mahali tuwe na uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili kuhusiana na usalama. Huko vijijini bahati nzuri mimi naishi kijijini kwa kweli vijana wetu ambao zamani wazazi wao walikuwa ni wakulima hodari, lakini sasa wao wamegeuka ni watu wanaongojea kuwa walanguzi, watu wa kati. Sasa hawa ndiyo wanaotumiwa kuhujumu wakulima. Sasa kilimo kinapoanguka na wao wanaanguka.

Lakini siyo hivyo tu Mheshimiwa Spika, katika maeneo yale ambayo hakuna eneo la kutosha hawa sasa wanageuka ndiyo wasaidizi wa ujambazi na imeonekana wazi kwamba vijana wengi wanaomaliza shule ya msingi, sekondari na hata walioachishwa kazi katika mpango wa kupunguza watumishi hawa ni wale ambao wanashiriki katika vitendo vya ujambazi.

Sasa mimi ningeomba kabisa kwamba suala la vijana liangaliwe kwa makini zaidi kwa sababu kwa hakika hilo naweza kusema kwamba ni *Time bom* ni hii inaweza ikawa ni ya hatari zaidi kwa usalama wa nchi na ikawa ni ya hatari zaidi kwa kuvuruga maendeleo yetu yote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa ningependa niseme suala la nidhamu na uwajibikaji katika kutekeleza Bajeti hii. Ningeshauri kwamba ifanyiwe marekebisho sheria namba 7 na 8 ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inayofanya Kamati ya Fedha na Mipango za Halmashauri baadaye zinageuka kuwa Bodi za Zabuni za Wilaya.

Sasa mfumo huu kwa kweli unajenga mianya ya rushwa. Sasa ningeshauri kabisa sheria ipitiwe upya ili ikiwezekana ile Bodi ya Zabuni iwe wazi na ikiwezekana iongozwe na mtu kama Padri au Sheikh wanaochukia rushwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo alikuwa msemaji aliyepangwa wa mwisho kwa asubuhi hii. Napenda kutoa taarifa kwamba sasa katika orodha ya wachangiaji tumeshapata majina 83. Kwa hiyo, ukizingatia kwamba hatimaye mwishoni Mawaziri husika watahitaji nafasi ya kujibu hoja za Wabunge, nadhani tumeshapata orodha ya kutosha kwa siku tano zilizotengwa kwa ajili ya hoja hizi. Kwa hiyo, orodha hii itawekwa kwenye ubao wa matangazo ili kila mtu aliopo ajue na asiyekuwepo ajue. Sasa kwa wale wasiokuwepo nitaomba wachangie kwa maandishi kwa sababu haitawezekana tena kuwaingiza kwenye orodha, wachangiaji wameshatosha kwa siku zilizotengwa. Hilo moja.

La pili, nataka kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge, tuko viongozi wanne tuliochaguliwa kuongoza Bunge katika Kiti hiki cha Spika. Yuko Spika, yupo Naibu Spika na wako Wenyeviti wawili waliochaguliwa kwa kazi hiyo. Kwa hiyo, kwa kuwa mkutano huu ni mrefu, nitakuwa napanga zamu nani aongoze Bunge lini, ili kusudi kusambaza uzoefu kwa wenzangu na wao wajenge uzoefu wa kuongoza Bunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kuanza mchana huu itakuwa ni zamu na Mheshimiwa Mwenyekiti, Anne Makinda, ndiye atakayeongoza Bunge.

Baada ya kusema maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.50 Mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 Jioni)*

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kwamba, fedha zaidi za misaada zinatakiwa ziingie katika nchi yetu badala ya fedha za mikopo. Hiyo itatusaidia kuondokana na adha ya kufikiria tena kuanza kulipa madeni na hivyo kuendelea kukusanya nguvu zetu za ndani ili kukidhi mahitaji na matumizi yetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la msingi ni kuangalia bei za juu za biashara za ndani za nchi yetu zinazouzwa huko nje. Bado Tumekuwa na tatizo kubwa la masoko na bado bei ya mazao yetu imekuwa ikiyumbayumba kila siku.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa pia kama tunaboresha Kilimo, ni lazima tuangalie viwanda vidogo vidogo na hasa katika maeneo yale ambayo Kilimo kitakuwa kimeboreshwa. Pamoja na kuzalisha kwa wingi kama hatutakuwa na viwanda vidogo vidogo ambavyo vitaanza kubadili malighafi hiyo kwenda katika bidhaa, bado juhudi zetu zitaendelea kuwa ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kuwa kuna kundi kubwa la wafanyakazi wetu waliostaafu. Hawa tungeweza pia kuwachukua na tukawatumia kama wataalam wa mwanzo katika maeneo wanayoishi ili kusaidia kutoa elimu na kusaidia katika suala zima la maendeleo kuliko kuendelea kuwaacha. Ninaipongeza Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, kwa kuwarudisha Mahakimu waliostaafu na wanasaidia sana kutoa michango mbalimbali katika kazi zao za uhakimu. Iweje Serikali yetu isifikirie kuwachukua Mabwana shamba, maafisa maendeleo ya jamii ambao wamestaafu na wako katika mazingira yetu wakatusaidia katika vita hii ya mapambano dhidi ya umaskini na ukuaji wa uchumi wetu katika nchi yetu ya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado tunahitaji Taasisi za Fedha ziendelee kuona umuhimu wa kujiingiza moja kwa moja katika maeneo ya vijijini ya wazalishaji na kutoa huduma hiyo kwa ukamilifu. Tumekuwa na tatizo kubwa si rahisi sana kwa Wananchi kuondoka masafa marefu kutafuta uwezeshwaji wa namna moja ama nyingine. Ninaamini Taasisi hizi zitasaidia sasa kuwabadilisha wakulima wetu kutoka katika kilimo kile cha mkono, cha kutumia jembe la mkono kwenda katika kilimo cha majembe ya kukokotwa na ng'ombe na hata kutumia matrekta na hivyo kuongeza uzalishaji. Si tu suala la pembejeo, lakini pia zana za kutumia katika uzalishaji ni bora ziangaliwe kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kusema kwamba Mkataba wa Huduma Bora kwa Wateja usisitizwe ili jamii iufahamu na kuuelewa vizuri kwani utachangia sana katika suala zima la uzalishaji. Tunapozungumza uzalishaji hatuzungumzii tu suala la Kilimo ama madini, vile vile tunatakiwa kujua ni kwa kiasi gani huduma zitatolewa ili kuwawezesha wazalishaji kumudu kufikia kiwango cha uzalishaji kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niendelee kuishukuru Serikali kwa kuona umuhimu wa kuzingatia suala la jinsia katika Bajeti hii. Ninaamini kabisa usawa wa jinsia kwamba mahusiano bora kati ya wanaume na wanawake yatachangia kuleta mabadiliko makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitoshi kuendelea kusema mwanamke tu aangaliwe, lakini bila kumsaidia mwanamme kuelewa umuhimu wake kama mwenza katika suala zima la mabadiliko, haitasaidia kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninaomba niunge mkono Bajeti hii, kwa asilimia mia moja, lakini ninaomba sana utekelezaji wa Bajeti hii uwe ni yakinifu utakaowezekanika na hivyo utaisaidia sana nchi yetu kuondokana na tatizo kubwa la kiuchumi na kujiongezea pato ambalo litaweza kutusaidia kuleta maendeleo halisi na yanayotakiwa na ambayo yatakuwa ni endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004. Kabla sijafanya hivyo, napenda kwa niaba ya Wananchi wa Kisarawe niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote waliojiunga na Bunge hili kuanzia kikao hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Mawaziri, Dr. Abdallah O Kigoda na Basil P. Mramba, kwa hotuba zao nzuri sana. Bajeti hii ni nzuri kiasi kwamba hata wapinzani wanashindwa kupata hoja, wanabakia kusema kwamba, eti tunatekeleza sera zao! Ni bora

wasome Ilani za Uchaguzi za mwaka 1995 na 2000 wataona kwamba zinazotekelezwa ni sera za Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze na maoni kwenye hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda. Kama nilivyosema, mpango huu ni mzuri, lakini pia ningependa kuipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri katika kipindi cha mwaka uliopita. Maelezo yaliyomo katika ibara za 10 - 16 ya hotuba ya Mipango ni ya kujivunia kwa Chama cha Mapinduzi na Tanzania kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka tunaoumaliza tumefanya vizuri. Kama hotuba zinavyosema, tumepita utekelezaji wa mwaka 2001/2002. Vile vile, malengo yetu ya mwaka huu tumeyapita na kwenye ongezeko la Pato la Taifa kama hotuba zinavyosema, tumepita wastani wa nchi za Kiafrika. Hongera Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, kama anavyosema katika Ibara ya 13 ya hoja yake kwamba: “Kutokana na ongezeko la pato lisiloridhisha Wananchi walio wengi bado hawajaiona kama kweli bei imeshuka”. Kwenye Ibara ya 12 ya hotuba hiyo Mheshimiwa Waziri anatupa matumaini kuwa: “Hali ni nzuri”. Lakini napenda niseme kwamba huko vijijini tunakotoka kwa kweli hali bado haijawa nzuri na kutokana na ukosefu wa mvua za vuli na masika njaa sasa hivi inatunyemelea. Hali halisi ni ile ambayo inaelezwa katika kitabu kile cha Benki Kuu cha *Monetary Policy Statement* kama ilivyowekwa katika *paragraph* za 23 na 39.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuzungumzia kidogo umuhimu wa takwimu. Hapa nitakuwa tofauti kidogo na Mheshimiwa mmoja aliyetangulia asubuhi aliyesema kwamba: “Mwaka huu takwimu zinakubaliana.” Kwenye Ibara ya 16 hotuba hii ya Mipango inatuambia kuwa Dola 1529.9 bilioni zilizofikiwa mwaka 2002 zinatuwezesha kuingiza bidhaa kutoka nje kwa miezi 8.9 au karibu miezi 9. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Ibara ya 8 inatuambia kwamba, fedha hiyo inatuwezesha kuagiza bidhaa kwa miezi 71/2 na kwenye *Monetary Policy Statement,* fedha ambayo ni nyingi kidogo Shilingi 1532.7 milioni, nayo eti inasema kwamba tunaweza kuagiza bidhaa kwa miezi 7.3. Sasa, ipi ni sahihi, miezi 9, miezi 71/2 au miezi 7.3? Nafikiri kuna haja kwa Taasisi hizi tatu ambazo huwa zinashirikiana katika mipango kuhakikisha kwamba takwimu zinakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17 ya Hotuba ya Mipango inasema kuwa, kutoka Juni 2001 hadi Juni 2002, Shilingi yetu ilishuka kwa 7.6%, lakini *Monetary Policy Statement* inasema, kati ya Juni 2001 na Aprili 2002, muda mfupi zaidi, Shilingi ilishuka kwa 9.7%. Kwa hiyo, ama Shilingi katika kipindi cha miezi miwili ilipanda kwa 2.1% au sivyo basi takwimu zinagongana. Niliona nisema haya ili kusudi tuwe na takwimu ambazo zinakubalika.

Mheshimiwa Spika, sasa napenda kuzungumzia Sekta ya Maji. Ibara za 49, 54 - 56 zinaelezea jitihada za Serikali katika kuwapatia Wananchi maji safi na salama. Ninaipongeza sana Serikali kwa jitihada zake, lakini kwa bahati mbaya maeneo mengi nchini kwetu hayafai kwa visima vifupi na suala hili mimi siyo mara ya kwanza kulisema. Kule Kisarawe na Kibaha kwa mfano, utafiti umegundua kwamba visima vifupi havichukui muda kukauka. Hali hiyo hiyo imeonekana katika Mikoa ya Shinyanga, Lindi na Mtwara ambako tulipata misaada ya Waholanzi na Wafini. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kwa mara nyingine tena iweke mkazo kwenye visima virefu, malambo na uvunaji maji ya mvua. Nafikiri huko tutakuwa na mategemeo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kukamilika kwa ubinafsishaji wa *DAWASA* ninaishauri Serikali imsisitizie huyo mtoa huduma mpya, kwamba kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa wale Wananchi wa Mkoa wa Pwani linapopita bomba kutoka Ruvu kwenda Dar es Salaam wanapata maji, wasiendelee kuwa watazamaji tu wa kuyaona maji yakienda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la elimu, ninaipongeza Serikali kwa kutenga fedha za kulipia ada za baadhi ya wanafunzi ambao wazazi wao hawana uwezo. Katika suala hili, ninaishauri Serikali iyape kipaumbele maeneo ambayo yapo nyuma sana kielimu na wengi wa wakazi wao kipato chao ni duni. Kisarawe na Mkoa wa Pwani unaingia moja kwa moja katika orodha hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nina matatizo kidogo juu ya uzito uliopewa Sekta ya Kilimo. Nitoe mfano tu, katika mgao nimechagua Sekta chache. Deni la Taifa limepewa Shilingi bilioni 4 na milioni 5, Ulinzi Shilingi bilioni126, Wizara ya Fedha Shilingi milioni 123.5, Afya Shilingi milioni 86, Elimu ya Juu Shilingi milioni 69, Wizara ya Mambo ya Ndani, Polisi tu peke yao Shilingi milioni 65 na Mhasibu Mkuu Shilingi bilioni 62.5 Kilimo kimepewa Shilingi bilioni 22.6 tu. Ni kweli fedha za kilimo zimeongezeka kwa Shilingi bilioni 6 kutoka mwaka jana, lakini bado sijapata mantiki kwa nini Bajeti ya Wizara ya Fedha niliyoitaja imeongezeka kwa Shilingi bilioni 80 wakati Kilimo kimeongezeka kwa Shilingi bilioni 6 tu kati ya mwaka jana na mwaka huu? Kwa maana hiyo basi, bado tusijigambe kusema kwamba tunakipa umuhimu mkubwa kilimo kama uti wa mgongo. Sina ugomvi na Sekta yoyote, lakini nafikiri kuna haja ya kuhakikisha kwamba kweli kilimo ni uti wa mgongo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningeomba basi Serikali iangalie sana suala hili kusudi tunaposema kwamba tunatia uzito, basi uwe ni uzito wa kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inastahili kupongezwa katika bajeti hii kwa mambo mengi, lakini nitataja machache. Kwa sababu ya muda sitaweza kuyataja yote kwa sababu mengine yametajwa na Waheshimiwa walionitangulia.

Kwanza, ni ukusanyaji mzuri wa kodi. Tunaambiwa kwamba tumevuka lengo kwa 4.5% hongera sana, lakini haieleweki ni kwa nini ushuru wa forodha ushuke wakati manunuzi yetu kutoka nje yameongezeka! Nafikiri hili suala itabidi Waziri wa Fedha alitafakari.

Mheshimiwa Spika, pili, ni ufutaji wa baadhi ya kodi. Ninaipongeza sana Serikali kwa kufuta kodi ya maendeleo ambayo imekuwa kero kwa Wananchi na pia azma yao ya kutaka kupunguza mlolongo wa kodi za Halmashauri. Lakini kwa kuwa hatua hii itapunguza mapato ya Halmashauri nyingi, ninaishauri Serikali kubuni mbinu za kuongeza mapato ya Halmashauri ikiwemo kuongeza gawio kwa Halmashauri hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, kutambuliwa kwa Watendaji wa Vijiji na Kata. Hatua hii kwa kweli itawahamasisha sana Watendaji hao ili waweze kusimamia vizuri katika utekelezaji wa mipango yetu katika maeneo yao. Awali sikuelewa kwa nini mishahara ianze kulipwa kuanzia Januari 2004 na siyo Julai mwaka huu wa 2003, lakini baada ya kupata maelezo ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utumishi kwenye Kamati yetu, nimeridhika kabisa kwamba, matayarisho yanahitajika kabla mishahara haijaanza kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, kufidia bei za pambejeo. Hatua hii itakuwa kichocheo kwa wakulima wazalishe zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tano, kuanzisha mifuko ya kuwasaidia wafanyabiashara pamoja na wanaosafirisha bidhaa nje. Kwa kuwa mtaji ni moja ya matatizo makubwa ya Wafanyabiashara ndogo ndogo, hatua hii itakuwa kichocheo kikubwa cha uzalishaji utakaosaidia ongezeko katika Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, sita, kutenga fedha za kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya. Hili ni jambo zuri, lakini kuna mambo mawili. Jambo la kwanza kama walivyosema Waheshimiwa walionitangulia ni kwamba, pana haja ya kusimamia vizuri sana matumizi ya fedha hizi zisije zikatumika isivyotakiwa. Lakini jambo la pili ni kwamba, nimeangalia katika Bajeti ya Maendeleo, sijaweza kuona kasma hii. Inawezekana sikusoma vizuri, lakini kwenye Wilaya zote sijaiona, labda Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia tutaiona wapi kasma hiyo.

Mheshimiwa Spika, saba, utengaji wa fedha kwa ununuzi wa chakula cha njaa. Huu ni uamuzi wa busara wakati huu ambao maeneo mengi hapa nchini yamekosa mvua za masika na vuli. Lakini ninamwomba Mheshimiwa Waziri, kwenye orodha ya Wilaya zile alizozitaja, zenye njaa, basi aiunganishe Kisarawe. Maana kama tulivyosikia katika Vyombo vya Habari wiki iliyopita, baadhi ya Kata za Wilaya yangu watu sasa wanakula nyasi!

Mheshimiwa Spika, nane, uanzishwaji wa mfuko wa kuwasaidia baadhi ya wanafunzi wanaojinga na Shule za Sekondari. Tunaipongeza sana Serikali, lakini nashauri kuwa mkazo mkubwa uwekwe kwenye maeneo ambayo yako nyuma kielimu na kipato cha wakazi wao ni cha chini. Kama nilivyosema mwanzo Wilaya ya Kisarawe na Mkoa wa Pwani unaingia katika orodha hii.

Mheshimiwa Spika, tisa, Taifa kujiondoa pole pole kwenye bajeti tegemezi ingawa Mheshimiwa Waziri wa Fedha anasikitika kidogo kusema kwamba bajeti hii ni tegemezi na baada ya Serikali kufuta kodi ya maendeleo wenzetu wapinzani wanatafuta hoja na kwa mujibu wa vyombo vya habari, hoja waliyoishika ni kwamba: "Aah, bajeti hii ni tegemezi!" Napenda kusema kwamba hatuna sababu ya kulalamika na hili kwa sababu ukiangalia bajeti ya mwaka huu ni karibu mara nne ya bajeti ya mwaka 1995. Kwa hiyo, imeongezeka. Lakini pamoja na hayo utegemezi wake ni 45% tu, wakati bajeti za nyuma tulikuwa na utegemezi unaopita asilimia 50%. Kwa hiyo, tunaenda vizuri, wapinzani walie tu, Chama cha Mapinduzi kinasonga mbele. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa bajeti nzuri, yapo maeneo ambayo ningependa kushauri yafanyiwe masahihisho. Kwanza, utozaji kodi wa dawa za mbu na vyandarua sikubaliani nao. Kwa sababu kwanza mapato yatakayopatikana ni madogo. Pili, hizi ndiyo nyenzo peke yake za mtu mnyonge za kuweza kupambana na mbu anayeeneza ugonjwa ambao sasa hivi ndiyo muuaji mkubwa hata kupita UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, pia, utozaji wa kodi kwenye ada za Wakurugenzi wasiokuwa na Ukurugenzi wa kudumu sikubaliani nao. Kwanza hawa ni watu wachache, wengi wao ni watu wastaafu, wanataka wapate mahali ambapo wanaoweza kufidia kidogo ile *pension* wanayopata ambayo hairidhishi. Sasa Serikali itapata nini katika kuwatoza watu hawa kodi hii?*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimeangalia *Monetary Policy Statement* ya Benki Kuu, nimeona kuwa Serikali bado inakopa sana! Imeondoka kukopa kutoka kwenye Mabenki, inakwenda kukopa kutoka kwa Wananchi, kwa maana ya kutoa *Treasure Bonds.* Sababu iliyotolewa ni kwamba kuna fedha nyingi katika *circulation.* Lakini unapokuwa na hali hiyo, aidha unapunguza pesa au unaongeza uzalishaji.

Sasa, kwa kuwa Serikali siyo mwekezaji tena, fedha hizi kuziondoa mikononi badala ya kuziweka kwa wazalishaji zikikaa kule Benki Kuu bado hujauongeza uzalishaji. Kwa hiyo, bado kutakuwa na *too few goods chasing too much money*.

Mheshimiwa Spika, sipendi kugongewa kengele ya pili, lakini nadhani maoni yangu Serikali imeyasikia na ningeomba hasa zile kodi iweze kuzipunguza na kuzifuta ambazo zinastahili, lakini bado tunabaki kwamba Bajeti hii ni nzuri sana na ninaamini kabisa Bajeti zijazo ule utegemezi wa 45% utashuka mpaka 30% na pengine 20%.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Leo hii nitazungumza kwa ufupi sana, isipokuwa nimepanga nizungumze kwa aina mbili. Kwanza nitazungumza kwa utangulizi na baadaye mchango wangu kwa ufupi.

Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutangulia kuwapongeza sana timu ya Simba. Ninaipongeza timu hiyo siyo kwa sababu imeifunga timu ya Zamalek, bali kwa sababu imevunja mwiko wa timu za Misri kuwa zinaifunga timu za Tanzania. Kwa hilo ninawapongeza sana timu ya Simba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuwapongeza Mawaziri, lakini napenda kuipongeza Serikali kwa ujumla kwa mambo yafuatayo: Kwanza, kwa kuondoa Kodi ya Maendeleo ya kuziainisha kodi nyingine zote za Halmashauri. Pili, nawapongeza kwa kuainisha kodi ya mapato ambayo ilikuwa ni kero. Kodi ya mapato kwa mwaka imewekwa katika viwango mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, naipongeza *TRA* kwa juhudi wanazozifanya katikakukusanya mapato. Katika suala hili napenda kushauri kwamba, iundwe Tume ya kufuatilia matumizi yaliyomo/yaliyokubalika katika bajeti kwamba zimepatikana fedha kiasi gani, zimekwenda wapi na zimefanya nini, kuliko ilivyo hivi sasa tunakusanya fedha nyingi lakini matumizi yake bado hayajawa mazuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, napenda kuwapongeza Serikali kwa kupunguza mfumuko wa bei. Napenda kuwashauri kwamba waweze kuangalia ni namna gani thamani ya Shilingi yetu inashuka kila siku. Mfumuko wa bei uko chini, lakini thamani ya Shilingi inaporomoka mara kwa mara na hapo hapo waangalie ni kwa nini uwezo wa Wananchi wa kununua nao unapungua.

Mheshimiwa Spika, tano, napenda kuipongeza Serikali kwa jinsi ambavyo wameimarisha Mfuko maalum wa Elimu ya Msingi na kusaidia Watoto Yatima. Lakini napenda kushauri kwamba hapa mwelekeo tuuweke katika kuimarisha Shule za Sekondari na Elimu ya Juu ili angalau tuweze kufanana na wenzetu wa Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, napenda kuipongeza sana Serikali kwa namna ya kipekee kwa kuanzisha ujenzi wa barabara kuu za Mwanza - Dar es Salaam na Dar es Salaam - Lindi - Mingoyo. Ujenzi huu tumeanza, napenda kushauri kwamba sasa tufikirie namna ya kujenga barabara za kuinua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizo ni barabara ya kutoka Kigoma - Itigi, Nzega -Tabora - Ipole - Rungwa - Mbeya. Barabara hii nasisitiza isipite Itigi - Rungwa, ipite Tabora - Ipole - Rungwa, kwa maana ya kuunganisha kwenda Mpanda Mkoa wa Rukwa. Barabara nyingine ni ile ya Arusha - Dodoma - Iringa. Tutakapojenga barabara hizi tunaweza kuinua uchumi kwa sababu maeneo haya yana uchumi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwapongeza Wabunge wote ambao wamechaguliwa kuingia katika Bunge letu hili Tukufu na ninachowaomba kwa kuwa wameingia katika Bunge hili la Wananchi wawatumikie Wananchi kwa moyo na kwa nguvu zao zote. Mambo ya malumbano, mambo ya udini, mambo ya chuki na fitna ...

**MBUNGE FULANI:** Na maruhani!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Na mambo ya maruhani, wayaache huko huko, hapa ni katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo ilikuwa ni sehemu yangu ya kwanza ya utangulizi na ninaamini Serikali hii ni makini ambayo inaongozwa na Chama cha Mapinduzi itayazingatia haya ambayo nimeyasema katika utangulizi.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo ambacho kimetolewa na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ukurasa wa 73 kuna fedha za ndani na fedha za Mikoa. Katika fedha za ndani kuna Mikoa ambayo haipati kabisa fedha za nje! Fedha za ndani zipo jumla ya Sh.25,633,210,100/= . Kuna Mikoa mitano ukiwepo Mkoa wa Dar es Salaam haipati kabisa fedha za nje, Mikoa hiyo ni Rukwa, Kigoma, Shinyanga na Tabora. Nimeangalia katika mfululizo wa kuanzia mwaka 1999/2000, 2000/2001, 2001/2002, 2002/2003 na sasa 2003/2004, mgawanyo wa hizi fedha kigezo chake ni nini? Mikoa mengine ambayo sijaitaja yote imepata fedha za nje na bado imepata fedha nyingine za ndani. Lakini cha ajabu katika hizi fedha za ndani iko Mikoa ambayo imepata fedha za nje imeongezewa tena nyingi zaidi kuliko Mikoa hii! Kwa mfano, Mkoa wa Tabora umepata fedha za ndani jumla ya Shilingi milioni 621, Mkoa wa Shinyanga umepata jumla ya Shilingi milioni 527, Mkoa wa Kigoma umepata jumla ya Shilingi 372, Mkoa wa Rukwa umepata Shilingi milioni 318. Mkoa mwingine ambao umepata fedha za nje ni Mkoa wa Singida, lakini Mkoa huo umepangiwa jumla ya Shilingi milioni 280 tu za ndani.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, hivi mgawanyo huu unafuata vigezo gani? Ni vigezo vya wingi wa watu, vigezo vya wingi wa Wilaya au ni vigezo vya tabia za watu wa kule? Kwa sababu ukiangalia Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma na Rukwa kwa asili ni Mkoa mmoja ambao ulikuwa

unaitwa *Western Province.* Sasa inakuwaje Mikoa hii haipati fedha nyingi za nje, lakini vile vile, bado inapewa kidogo fedha za ndani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu bajeti ni yetu na mapato ndiyo hayo tunayoyapata basi angalau kwa ile Mikoa ambayo haipati fedha za nje kwa mfano Mkoa wa Rukwa au Singida zingepata angalau kufikia Shilingi milioni 500 za ndani ili kufidia zile ambazo hazipatikani kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninapenda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha basi ajaribu kufafanua suala hili, juu ya vigezo ambavyo vimetumika kugawa bajeti katika Mikoa hii, hasa Mikoa ambayo wafadhili hawaipendelei. Mara nyingi Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kuna Mikoa ambayo inapendelewa na wafadhili, lakini ukiangalia kuna Mkoa mwingine umeanza juzi tu umepewa fedha nyingi sana za nje na umepewa fedha nyingi za ndani. Hivi sisi ambao tuko huko ambako wafadhili hawapendi hata Serikali yetu nayo haitupendi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nina hilo tu juu ya mgao katika Bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba, kwanza, ninaipongeza sana Serikali kwa kukumbuka kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wetu wa nyanda za juu, Mikoa ya Iringa, Rukwa, Ruvuma na Mbeya, ambayo ni *the big four.* Ni kweli itawasaidia katika kupunguza njaa kwa ulimaji wa zao la mahindi. Lakini ninajiuliza kwamba ruzuku katika Mikoa hii ni ya kudumu au ni ya muda! Iwapo ni ya kudumu, itadumu kwa muda gani na ni kiasi gani cha fedha ambacho kinatolewa katika mfuko mmoja wa mbolea?

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaahirisha Kikao asubuhi, tulikuwa tumepata wachangiaji kama nane hivi na sasa tunaanza. Mkitaka kutambua majina yenu, yako kule kwenye ubao. Kwa hiyo, sasa nitamwita Mheshimiwa Michael Lekule Laizer. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja ya Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha na ningependa tu kusema kwamba nawapongeza Mawaziri wote wawili na napongeza Baraza la Mawaziri na Kamati ya Fedha na Mipango kwa mchango mzuri waliochangia na kuboresha Bajeti hii na kupendwa na kila mtu. Ningependa kuungana na Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa wa Mbeya waliosema CCM iendelee kuongoza Taifa hili. Mimi kwa kweli naungana nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kusema kwamba Serikali ya Awamu ya Tatu imetengeneza njia ya ushindi wa kushinda Awamu ya Nne. Nadhani hata wapinzani leo wamekubali kwamba bajeti ni nzuri hii ni sera ya Chama chake, lakini waliotekeleza ni CCM, kwa hiyo ni sera ya CCM. *(Makofi)*

Lakini ningependa tu kusema kwamba Bajeti hii ni ahadi ambayo tumetoa kwamba tutatekeleza na ili tutekeleze ni lazima tukusanye mapato. Mapato yote yaliyokadiriwa ni lazima yakusanywe na bila kukusanya hatuwezi kutekeleza.

Ya pili, ni lazima kuziba mianya yote ya matumizi mabaya ya fedha pamoja na *over expenditure,* kama hatutafanya hivyo, mapato yatakwenda kiholela na hatutatekeleza yote yaliyosemwa katika Bajeti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Wabunge waliochangia na watakaochangia wote wataunga mkono Bajeti hii, hakuna atakayekosoa. Lakini ningependa na mimi nichangie kwa kuboresha. *(Makofi)*

Kwanza nashukuru kwa kodi ya maendeleo iliyofutwa. Lakini ningeiomba Serikali ifidie hizi kodi kwa sababu hizi kodi ndizo zinazotumiwa na Halmashauri nyingi, ndio mapato makubwa sana katika

Halmashauri zetu na msipozifidia Halmashauri nyingi zitaanguka. Zitafutwa kwa sababu hazina mapato na bila mapato hakuna Halmashauri. Nadhani mmeona kwamba mnaweza mkafidia kodi za wananchi. Kwa hiyo, naomba zifidiwe haraka sana ili mipango ya Halmashauri zetu zisife.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuzungumzia tena madini. Mheshimiwa Waziri alisema kwamba madini yote hayatapelekwa nchi za nje bila kukatwa. Sasa sina hakika kama kuna mashine hapa nchini zinazoweza kukata madini. Kama zipo sijui ni za nani, inawezekana zikawa ni za Wafanyabiashara wakubwa wa madini na hapo Wafanyabiashara Wadogo watanyanyasika kwa sababu ni biashara ya ushindani. Hawa Wafanyabiashara wakubwa wenye mashine wanaweza kuwanyonga hawa Wafanyabiashara Wadogo. Hii itasababisha magendo ya madini kwenda Kenya na nchi nyingine kwa sababu mfanyabiashara mdogo asipopata mashine atatafuta namna yoyote ya kusafirisha madini auze. Kwa hiyo, anaweza akapeleka Kenya ambao wao wanaruhusu kupeleka madini bila kukatwa. Kwa hiyo, ningeomba Serikali iangalie jambo hili zaidi kwa sababu inaweza kuleta kero kwa wachimbaji wadogo wadogo au Wafanyabiashara ambao sio wachimbaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la huu Mfuko mpya wa mikopo. Kwanza tunashukuru sana kwa kuweka Mfuko huu ambao umesema kwamba ni Mfuko wa Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa hiyo, nasema imegusa kabisa wale watu wa hali ya chini walioko Vijijini. Lakini ningependa kupata maelezo zaidi tuelewe hata katika Bunge hili ili tukiondoka na sisi tuweze kuyaeleza makundi hayo yote yaliyotajwa kwamba utaratibu wa Mfuko huu ni upi, namna ya kuzipata hizi fedha. Tunapenda sana tuelewe Mfuko huu ni muhimu kama nilivyosema, lakini ulenge watu waliotajwa isiwe kama Mfuko wa Pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Pembejeo, mimi nasema huo Mfuko unatumika vibaya sana na mimi nasema Mfuko huo ni vigumu kabisa kupatikana kwa mkulima wa hali ya chini wa Vijijini. Ni vigumu sana! Napenda kusema tu kwamba huo Mfuko ni Mfuko wa matajiri. Watu wachache sana kule Vijijini ndio wamepata hizo fedha. Wakubwa tu ndio wanapata hizi fedha na Mfuko huu uwe tofauti na Mfuko huo. Mimi bado nalaani kabisa kwamba huo Mfuko haukulenga watu wanyonge, ni Mfuko ambao ungeangaliwa sana na kama umepangiwa bajeti mwaka huu uangalie vigezo vilivyowekwa. Tunaweka masharti makubwa sana ambayo mtu akisikia, anakata tamaa hata ya kwenda kutafuta hizo fedha.

Kwa hiyo, tufahamu kwamba watu Vijijini hawawezi kukopa katika Mabenki, wanakimbilia katika mifuko iliyowekwa na Serikali yao, lakini tukiwapa masharti tena watashindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la masoko kwa ajili ya mifugo. Serikali yetu inafahamu kabisa kwamba Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa mifugo. Lakini katika kila Bajeti ya kila mwaka mnaipapasa tu na kuiruka, hamjaweka mikakati. Katika Bajeti hii nitazungumzia tu suala la masoko, suala la malambo nitazungumzia katika Bajeti ya Waziri anayehusika. Lakini tunazungumza kila siku na maswali ya masoko ya yanayojibiwa na Serikali ni maswali ya masoko ya korosho, pamba, kahawa lakini hakuna masoko ya mifugo yanayozungumzwa. Lakini mifugo inategemewa na wananchi wengi sana katika Taifa letu, hata wasiotegemea wanapenda kula nyama ya mifugo. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa nashangaa kwamba hatutafuti masoko kwa ajili ya mifugo, hakuna viwanda kwa ajili ya mifugo. Wawekezaji tunawataja kila siku, wawekezaji wa mambo mengine tu, kwa nini wasitafutwe wawekezaji wa kuja kujenga viwanda vya kusindika nyama katika Mikoa ya wafugaji? Shinyanga, Mwanza, Arusha, wana mifugo mingi inayotosheleza kabisa viwanda. Morogoro, kuna ndugu zangu walioko hapo Morogoro wanahangaika kila siku. Kwa hiyo, Serikali kama inataka kuondoa umaskini iwasaidie wafugaji kuwapatia masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niongee kwa haraka kwa sababu kengele imelia. Ningependa kuzungumzia tena suala la matatizo tunayopata watu wa mipakani. Sijui kuna nini! Tunanyanyaswa sana na Wafanyabiashara wa huko Kenya na tatizo letu ni kushuka kwa thamani ya fedha. Wafanyabiashara wa Kenya, kwanza ukiwa na Sh.1,000/= ya Kenya ni Sh.14,000/= za Tanzania ndio unabadilisha upate Sh.14,000/=. Kwa hiyo, Wafanyabiashara wa Tanzania hawawezi kabisa kufanya biashara na

Wafanyabiashara wa Kenya kwa ajili ya kushuka kwa fedha ya nchi yetu. Kwa hiyo, liangaliwe na hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kuzungumzia ubinafsishaji. Nimeona ekari milioni nne zilizowekwa kwa ajili ya ubinafsishaji. Kwanza sijui hizo ekari ziko wapi. Ingetajwa kwamba hizo ekari milioni nne ziko Mkoa fulani, Mkoa fulani na Mkoa fulani na zinafanyiwa nini. Vile vile naomba ikifika wakati wa kutumika wananchi walioko pale wahusishwe, sio kwenda tu kusema kwamba hii ardhi ni ya Serikali. Hakuna ardhi ambayo haitumiki na wananchi na hakuna ardhi ambayo iko mbali na wananchi. Kwa hiyo, wananchi walioko pale wahusishwe na wajue kwamba inatumika kivipi na wapate fidia endapo wawekezaji ndio watapewa eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni mafuta yanayotoka nje kwamba wakulima walioko Mikoa ya mpakani kama vile Rombo, Longido, Mwanga na kwingineko, wanatumia mafuta kutoka Kenya wakati wa Kilimo. Sasa huu utaratibu wa kufuata mafuta kutoka Kenya, wakulima wanapata matatizo uamuzi wa mafuta ya huko kwa ajili ya kudaiwa ushuru. Ningependa Serikali yetu iwasaidie wananchi walioko mipakani ambao wako mbali vilio vya na mafuta vyetu, yatolewe ushuru kabisa wakati wa kilimo ili wananchi waweze kufaidika na Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni fedha za UKIMWI. Hizi fedha hazina mradi. Matumizi ni vikao, semina na kadhalika. Ningependa kusema kwamba hizi fedha ziwasomeshe watoto yatima na watoto wa waathirika ambao hawawezi kuwasomesha watoto wao kwa sababu wamekwishaathirika. Hivi ukienda semina kila siku na watoto wa marehemu hao hawapati masomo itawasaidia nini? Ningependa kusema, hizo fedha zielekezwe kuwasomesha watoto hao, sio semina za kila siku ambazo hatuoni mwelekeo wake. *(Makofi)*

Vile vile ningependa kuungana na Mbunge aliyezungumza asubuhi, aliyesema fedha hizi za Mfuko wa Elimu zielekezwe katika maeneo ambayo bado wako nyuma sana kielimu, tuwasaidie maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Ahsante. Atafuata Mheshimiwa Ponsiana Nyami, halafu atafuata Mheshimiwa Jackson Makwetta baada yake. Mheshimiwa Ponsiana Nyami.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, jina langu sahihi la kwanza ni Ponsiano, maana yake Ponsiana ni mwanamke. *(Kicheko)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Ah, Ponsiano.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianzie na kupongeza Bajeti hii na awali ya yote niiunge kabisa mkono kuanzia mwanzo asilimia takriban zote na baada ya hapo naomba niende katika maeneo machache kutoa mchango wangu na kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Katika ukurasa wa 55 Serikali imefanya jambo zuri sana kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa na mitambo ya kuchimbia visima vya maji. Lakini pia nilikuwa naishauri Serikali kutoa msamaha kama huo kwa mitambo inayoletwa nchini kwa ajili ya kutengeneza barabara. Nasema hivyo kwa sababu barabara za maeneo mengi zina matatizo, lakini zinahitaji zitengenezwe ili zifike kwa wananchi na bidhaa zao ziweze kuchukuliwa kwa urahisi, lakini mitambo hiyo ni ya ghali sana. Kwa hiyo, ili kusudi tuweze kupata miundombinu hiyo ambayo ni bora, ni vizuri angalau kwa muda fulani niweze kusamehewa ili kusudi mitambo hiyo iingie kwa wingi zaidi na gharama za ukodishaji na utengenezaji barabara ziweze kupungua.

La pili, kuhusiana na Redio binafsi pamoja na *TV*, wamepewa eneo dogo sana la kuendesha shughuli hizo kwa mfano Redio Mikoa mitano wakati kwa mfano Tanzania Bara tuna Mikoa 21, Zanzibar Mikoa mitano, wanapewa eneo la Mikoa mitano ambayo ni michache. Nilikuwa naomba nijaribu kusaidia upana wa kutoa matangazo maana binafsi sioni *logic* au mantiki, *BBC* inasikika nchi nzima, Ujerumani inasikika nchi nzima, kuna vinchi vingine vidogo vidogo kama vile Rwanda vinasikika nchi nzima halafu

Redio yetu ya Wazalendo kama *Radio Free Africa*, *Radio One* na nyinginezo unawanyima, unawaambia Mikoa mitano. Mantiki iko wapi? Naomba hilo lifikiriwe na Serikali tusizidi kupitwa na wakati. *(Makofi)*

Jambo lingine nataka kulisema hapa inawezekana likaonekana la kuchekesha lakini katika ukurasa wa 46 tunapotazama kuwaongezea pensheni wale wastaafu, kuna watu wengine ambao hawajawahi kufanya kazi za Serikali, lakini ni wazee. Wana miaka 80 hivi, 85 hawajawahi kufanya kazi. Mimi nadhani wakati umefika wa kuwapa walau tuzo la ahsante kama ni kwa kuwajengea Makazi au na wenyewe kuwafikiria angalau kuwapatia chochote kile kwa ahsante ya kuishi miaka mingi ukitilia maanani kwamba walio wengi siku hizi kufikia miaka hiyo ni kitendawili. *(Kicheko)*

Katika ukurasa wa 68 kifungu kidogo cha tatu, kuna ile kodi ambayo imebakizwa *Property Tax* ambayo itatozwa kwenye Halmashauri. Lakini hapa naona kuna utata kidogo. Kuna maeneo fulani Halmashauri inatoza lakini pia Serikali Kuu unakuta nayo inatoza. Kwa hiyo, kunakuwa na mwingiliano nani hasa ambaye anatakiwa atoze? Lakini hata hivyo bado naiona kodi hii kwa kiwango fulani kama bado ni kero kwa wananchi hasa wale wa kawaida. Mimi nadhani kungekuwa na utaratibu kwamba kuanzia thamani fulani ya nyumba, yale majumba makubwa makubwa. Zamani ilikuwa wanasema nyumba inayoanzia Shilingi laki moja, zamani sana huko mwaka 1967. Lakini wakati huu tunaweza tukataja baadhi ya milioni kadhaa. Unakuta mwananchi amejenga nyumba yake ya kawaida kwa wakati huu labda milioni mbili au milioni tatu, analipia kiwanja, analipia nyumba, kwa hiyo unakuta bado hiyo ni kero. Nilikuwa naomba, kwa wananchi wa kawaida iweze kufutwa na yabakie yale majumba makubwa makubwa kama kule Mikocheni, Raskazoni na kwingineko.

Kuna suala la uingizaji wa mafuta ya petroli na dizeli, Serikali inasema kwamba waingizaji hawa watalipa kodi kwa mara moja. Lakini ninachokifahamu, hawa wanaoingiza mafuta haya ni mawakala tu wa Serikali, sasa unapomwambia aingize mafuta hayo na alipe kodi mara moja, maana yake unachomwambia ni kwamba aende akakope fedha mahali fulani. Akishakopa fedha hiyo akiileta Serikalini, akishakwenda kusambaza hayo mafuta yake, maana yake ni kwamba unampatia hasara nyingine ya kulipa riba kule alikokopa bila sababu. Kwa hiyo, nadhani ilikuwa ni vizuri pengine badala ya kulipa yote, labda alipe kidogo au mumruhusu akasambaze na halafu alete pesa ile. *(Makofi)*

Lakini pia, wenzetu wa *TRA* wamefanya kazi nzuri sana mimi nawapongeza, lakini katika baadhi ya maeneo nina ushahidi wa maeneo machache kama vile Mbeya, Rukwa kwa upande wa Sumbawanga. Wafanyabiashara wanalalamika sana kwamba wanawakadiria makadirio makubwa ambayo hayalingani na biashara zao na wanafanya hivyo kwa sababu Serikali imewapa kiwango kikubwa kuwalazimisha kwamba *TRA* Rukwa, *TRA Mbeya*, Arusha au Mwanza lazima mlete fedha kiasi hiki. Kwa hiyo, kwa sababu wamepewa lengo na kadirio hilo pengine la juu mno wanalazimika na wao kupandisha makadirio kwa kila mfanyabiashara. Sijui niite lugha gani, kuwalalia au kuwafanyaje wale Wafanyabiashara! Yaani kuhakikisha kwamba wanawakamua hata pale mahali ambapo haiwezekani. Nilikuwa naomba hili litazamwe upya tena ili kusudi wanaofanyabiashara na wenyewe waweze kufaidika na kulipa kodi kwa moyo mkunjufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la fedha bandia. Mimi nilikuwa naomba kufahamu kutoka kwa Serikali kwamba, mara kwa mara tunapobadilisha noti zetu, hata kabla mwezi haujaisha noti bandia zimekwishaingia, sasa udhibiti wake ukoje? Zile *specimen* wanazipataje? Halafu huu mtandao wa hawa watu ukoukoje? Tatizo ni nini hasa? Maana nchi nyingi kwa mfano za jirani zinazotuzunguka unakuta hawana matatizo makubwa kama hayo tunayoyapata hapa Tanzania. Tatizo ni nini hasa? Hii ni kero kubwa kwa wananchi kwa sababu wanaoathirika zaidi ni wanyonge, wananchi wa kawaida wa chini ndio hao wanaosumbuliwa kwa kupata fedha hizo na baadaye pengine hata kutupwa Mahakamani bila sababu za msingi. Nilikuwa naomba hili litazamwe.

Katika ukurasa wa 21, nilicheka kidogo, kifungu kile cha 26 pale chini kuhusu madeni kwamba Serikali inafanya mazungumzo tena kwa bidii kabisa na Zambia na Libya. Lakini wanasema bado hawajatuahidi chochote. Eti kufutiwa madeni ya Zambia! Madeni gani na Zambia? Zambia kwanza ni maskini kuliko Tanzania, ninyi mnakwenda kuwabembeleza wawafutie madeni. Mahindi tunawapatia tena kwa msaada. Serikali inang'ang'ana kuwabembeleza jamani, tufutieni deni. Ah!

**WABUNGE FULANI:** Madeni. *(Kicheko)*

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Madeni eh! Madeni samahani. *(Kicheko)*

Sasa nilikuwa naomba hilo kwamba Serikali ijaribu kutazama angalau kwa Zambia kulikoni? Deni gani hilo? Lilipeni hilo! Wazambia wale maskini, ndugu zetu wale! *(Kicheko)*

Halafu jambo lingine, mnaweza kuona kama la mzaha lakini nadhani wakati umefika na lazima tuwe *serious.* Hapa Wizara zinakuja zinabembeleza tunatoa fedha, kafanyieni kazi, wakishapata fedha hizo wengine wanakwenda kuzichezea. Mamilioni ya fedha zinapotea katika Wizara halafu tunaacha tu. Mimi nadhani wakati umefika kwamba fedha zikishapotea ambazo tumezitoa hapa Bungeni, Waziri apelekwe kitimoto kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi na baadaye Kamati hiyo ikiona haijaridhika impeleke kwenye Kamati ya Haki na Maadili, ile ya Mheshimiwa Eliachim Simpasa ili kusudi aweze kuambiwa wewe na wewe hiki! *(Kicheko)*

Ndiyo! Si hela zetu? Ili ikiwezekana *judgment* ikitoka na wewe mwenyewe hatukupi tena fedha! Wewe si unaziharibu ovyo ovyo! Lazima uwekwe kitimoto kule mahali. Inawezekana likaonekana la mzaha lakini kwa kweli ndiko tunakokwenda, mabilioni ya fedha anakula nani? Ninyi wenzetu tumewatuma mmekaa hapo, kwa nini? Tuwaweke kitimoto basi kama hamtaki kuwaweka kitimoto hao ma-*accounting officers* wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kufahamu hawa Watendaji wa Vijiji ambao wataajiriwa kwa mikataba na kwamba watalipwa kuanzia Januari mwaka kesho 2004. Kwa kipindi hiki cha sasa mpaka Januari, 2004 ni nani anawalipa wakati Halmashauri tumeshawanyang'anya mapato yao mengine mengi tu? Tupate utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile kengele ya kwanza imeshalia, ninaomba nianze kuishukuru Serikali kwa Shilingi milioni 20 ambazo Serikali imeandaa kutupatia Wilaya ya Nkasi kwa ajili ya nyumba ya *DC.* Ninashukuru sana. Halafu niishukuru Serikali kwa kufidia gharama za mbolea katika Mikoa ya *The Big Four,* yaani Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma. Tunaishukuru sana Serikali. Lakini pia Serikali imeruhusu wananchi kuuza mazao nje hasa yale ya chakula na Mkoa wa Rukwa ni mmojawapo unaouza nje.

Tunaishukuru Serikali kwa mara nyingine tena, wananchi wetu wanauza mahindi sana kule Zambia, Kongo na wanauza kwa wingi tu, tunashukuru sana. Lakini nilikuwa naomba kuishauri Serikali kwamba ione uwezekano wa kututengenezea ile barabara inayotoka Sumbawanga kwenda Zambia kupitia Mji wa Mbala. Barabara ile ni mbaya sana. Barabara hii haijatengenezwa sijui miaka mingapi iliyopita, lakini ndio magari mengi sana yanasomba mahindi kupitia barabara hiyo. Kwa upande wa Zambia ni nzuri lakini kwa upande wa Tanzania ni mahandaki makubwa na ni aibu kubwa kupita kiasi. Nilikuwa naomba Serikali kwa kweli kwa njia ya pekee kabisa iitazame barabara hiyo ya kutoka Sumbawanga kupita Kasesha, kuingia hadi pale Mbala. Upande wa Zambia hauna matatizo.

Kuhusu maeneo ya kilimo, Serikali itenge maeneo ambayo yako mbali kidogo na wananchi na siyo kunyang'anya maeneo ya wananchi, maana kero kubwa ni kunyang'anya mashamba ya wananchi katika vijiji, watafute maeneo mengine, katika *land bank* ilikowekwa, ndipo wale wawekezaji wakubwa waweze kutoa maeneo hayo ili pia huko watatutengenezea barabara na mambo mengine.

Mwisho kabisa, kuhusu uwanja wa michezo. Tunashukuru umepewa shilingi bilioni 5. Lakini bilioni 5 unajenga uwanja wa namna gani? Labda uwanja kama ule wa Sumbawanga pale mjini labda inawezekana. Lakini uwanja mkubwa ambao una mambo mengi, sijui na vijiji na kadhalika, bilioni 5, mmh, huu naona ni mzaha huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri katika eneo hilo, ajaribu kutafutafuta mahali panapowezekana, ili kusudi fedha nyingi zipatikane na uwanja huo ukamilike ukitilia maanani kwamba mpaka mwaka 2005 utakuwa umekwisha kamilika.

Baada ya kusema hayo, ninaomba kwa mara nyingine tena kuunga mkono hoja hii na kuunga mkono Bajeti hii ambayo ni nzuri na ninaamini kila Mheshimiwa Mbunge, mwenye kujua mambo ya uchumi aliyepo hapa na anayejua wananchi wake walimtuma kwa namna gani kwa kweli ni muhimu kuiunga mkono hoja hii. Akikataa ana mambo yake ya siri. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na pia ningependa kuungana na wenzangu kuwakaribisha Wabunge wapya katika Bunge letu Tukufu na kuwaomba tushirikiane katika kuwatumikia Watanzania, yaliyopita si ndwele tugange yajayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa vile vile kuwapongeza Mawaziri wawili, waliotoa hotuba hizi kwa hotuba zao nzuri na nzito na bila shaka haya ni matokeo ya ushirikiano wao na wataalam walio chini ya Wizara zao.

Pili, ni hii tabia ya Serikali kuanza kusikiliza mawazo ya wananchi kupitia kwa wawakilishi wao yaani Wabunge. Hii ni nchi yetu sote na ni vizuri kama tunaheshimu *democracy* basi tusikilize maoni ya wananchi kupitia kwa Wabunge ambao wapo hapa. Haiwezekani Watanzania wote yaani Watanzania milioni 34, waje hapa kuzungumza. Ssisi ndiyo sauti ya watu na sauti ya watu ni sauti ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nathubutu kusema kwamba hii ni Bajeti ya watu, ni Bajeti ya Watanzania, ni Bajeti ya kandambili. Sasa kama Waheshimiwa Wabunge, wote kwa pamoja tunakubaliana kwamba ni hii hotuba nzuri, nadhani ni vizuri wana CCM, tupokee wazo linalotoka kwa wenzetu wa Upinzani kwamba nao wanaiona ni nzuri. Wamesema hotuba hii ni nzuri, tumesikia mawazo yao. Sasa tunapinga nini? *(Makofi)*

Nilidhani, kama binti yako anapendwa na wakwe, basi ukubali na ufurahie. Unakataa nini tena? Mlitaka waseme nini? Ndugu wapinzani nawapongeza kwa kuona jambo zuri na kulisifu. Jambo zuri tulisifu. Jambo baya tulitolee maoni yetu. Ni kwa mara ya kwanza hapa kwa pamoja, sote tunazungumza lugha moja, kama tunapunguza kero za wananchi na hapa ndani tunazungumzia kujenga nchi yetu, kuwatumikia watu wetu na tunazungumza kwa sauti moja. *(Makofi)*

Mimi nadhani tumeanza kuonyesha kukomaa. Kukomaa kimawazo, kukomaa kisiasa. Yale mambo mengine yale mnayoyasema kule nje yaishie huko huko. Hapa ndani busara ndiyo itawale. Kama kuna wazo zuri, wazo zuri hata kama linatoka Upinzani tutalipokea, kama wazo zuri, kwa sababu ni wazo la kujenga nchi. Sisi ndiyo wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, kwa msingi huu mimi nadhani ni vizuri tujipongeze wana CCM. Lakini tujipongeze Wabunge wote bila kujali tofauti zetu za itikadi kwamba jambo zuri hili tumeliona wote kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huu ni wakati mzuri kwa Serikali kusikiliza maoni ya Watanzania kwa nchi nzima, kwa sababu kwanza Watanzania wengi wanasikiliza hotuba hizi. Lakini ya pili, wawakilishi wao wapo hapa kutoka nchi nzima. Utapata wapi nafasi nzuri kama hii ya kusikia maoni ya nchi nzima? Kwa hiyo, nasema ni vizuri Serikali isikilize maoni ya Wabunge. Huu ni wakati mzuri kwa Serikali kusikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia ukurasa wa 28 mpaka 31 na ukurasa wa 40 wa Bajeti ya Waziri wa Fedha. Kwa kweli ningependa nipongeze uamuzi wa Serikali wa kutoa ruzuku kwa mbolea kwa Mikoa ile minne ya Nyanda za Juu za Kusini. Waheshimiwa Wabunge, sababu ya msingi hapa ni kwamba ile ardhi kutokana na mvua nyingi imepoteza yale madini na rutuba yake. Kwa hiyo, bila mbolea wakulima hawawezi kupata chochote. Kwa hiyo, peleka mbolea au chakula. Watu wana bidii sana. Pia hali ya hewa ni nzuri na wakati fulani ndiyo wamekuwa wanatoa chakula hata kwa nchi za Malawi, Zambia, Congo, Comoro, Zanzibar na hivi sasa pale Makambako yamejaa malori kutoka Kenya, Malawi, Zambia, Zanzibar, Comoro, Congo yanachukua viazi, mbao na mahindi. *(Makofi/Kicheko)*

Tupeni mbolea kwa bei nafuu tutalisha Taifa hili na nchi hii. Mwaka huu wakati mvua imekuwa ni kidogo na watu wa Nyanda za Juu wamepata mazao mengi zaidi kwenye maeneo ya miinuko, kwa mfano sehemu za Njombe Kati, Lupembe, Igominyi, Igongolo Mtwango, Imalinyi kutokana na mvua

kuwa kidogo, mimea imepata nafasi ya kustawi vizuri zaidi. Tumepata mazao mengi kuliko miaka ya mvua nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tuliyonayo tuitumie Tanzania ina bahati nzuri ya kuwa na tofauti ya hali ya hewa na mvua. Kuna tofauti kati ya eneo na eneo , eneo moja likakosa mvua, eneo lingine likapata mvua. Bahati hii ndiyo tuliyonayo na ndiyo hata matunda mengine yanayopatikana nchi za baridi, Nyanda za Juu kule Makete, Mufindi na Njombe.

Sasa kuomba kwamba kote wapelekewe mbolea kama Njombe au Nyanda za Juu ni kutoona ukweli wa mambo. Kwa sababu kama wewe ni mgonjwa wa ugonjwa fulani, lakini mwenzako haugui ugonjwa huo, vipi nyote mpewe dawa ile ile? Ni kwamba ardhi ile haina *minerals* fulani kutokana na mvua nyingi mno. Imechuja madini, chumvi chumvi hazimo. Ardhi haina rutuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu gani? Wewe siyo mgonjwa kwa nini upewe dawa? Msingi wa maana hapa ni kwamba tuzalishe chakula kwanza. Kwa mtu anayezalisha chakula mimi nadhani tungekuwa na busara kwamba hawa wenzetu wanasema wazalishe chakula ili wakati wote tuwe na uhakika kwamba kuna chakula ndani ya nchi yetu. Ndiyo maana mimi naunga mkono lile wazo kwamba kila Wilaya ichague zao moja la biashara na zao moja la chakula ingawa natofautiana kidogo.

Dhana hii nayo imepitwa na wakati. Hivi lipi ni zao la biashara. Mahindi je? Lakini hivi unasema uchague zao moja, kwa mfano Wilaya ya Njombe, zao lipi, Chai, Kahawa, Pareto, Viazi, Mbao na kadhalika kwa kutumia vigezo gani?

Mimi nadhani suala la msingi hapa ni kawaida kila Wilaya ilime mazao yale ambayo yanafuata sifa za eneo lile na hali ya hewa ya eneo lile. Hiyo ndiyo *point* na siyo kulima zao moja kama alivyosema Mheshimiwa William Kusila, tuangalie sifa ya ardhi na hali ya hewa hizi. Bangi siku hizi imepigwa marufuku na Njombe hatulimi bangi siku hizi. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, watu wa Dodoma walime Mtama, watu wa Arusha walime Ngano na Kahawa na mazao mengine kwa kufuatana na *ecology* na hali ya hewa ya mazingira yao. Lakini kwa mazingira ya sasa hivi huwezi ukazungumza lugha hii ambayo imepitwa na wakati. Hili zao moja una-*guarantee* gani kwamba bei itabaki ile ile. *Strategy* iwe ni *diversification* kwa kufuatana na sifa ya ardhi na sifa ya hali ya hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mtu unapotembea katika nchi ya watu wezi, na una hela nyingi, njia ni kuweka fedha nyingine katika mfuko mmoja wa suruali, kwenye koti, ili wakikuibia, upande mmoja, upande mwingine inapona. Sasa ndiyo mkakati wa ku-*develop* kilimo, una-*diversify* kwa kufuatana na sifa za mazingira ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi unataka Wilaya zilete orodha au zichague zao moja, kwa nini? Hivi sisi hatujui? *Atlas* ya ardhi ya Tanzania inajulikana. Hali ya hewa ya Tanzania tunaijua na Waziri wa Kilimo na Chakula, hapa akiagiza wataalam wake walete mazao kutoka kila mahali atapata sasa hivi.

Kwa hiyo, napendekeza kuwa kabla ya kumaliza Bunge, Waziri wa Kilimo na Chakula, atuletee mazao yanayofaa kwa kila Wilaya ya Tanzania. Kwa sababu anajua sifa zake, hali ya hewa, mvua na hii inajulikana, badala ya kusubiri majibu yatoke Wilayani Njombe. Miaka 40 baada ya Uhuru hatujajua wapi, mazao gani yanastawi wapi. Tulimalize hapa hapa.

Lakini maswali yaliyoulizwa pale kwamba hivi ni kwa muda, ni kiasi gani, ni vizuri afafanuliwe wakati tukiwa hapa hapa kusudi wananchi waelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero kubwa ya wananchi ni umaskini. Hii ndiyo kero kubwa ya Tanzania, hayo mengine ni matokeo tu kwamba watu tunahangaika kuwalipisha kodi, ni sababu ya umaskini. Ninashukuru kwamba Serikali imeona ubaya wa kuwanyanyasa watu wake na kutafuta kodi. Watu wengine walikuwa wanahama hata nyumba zao kwa sababu ya kodi, walilala nje, kwa sababu ya kodi. Kwa hiyo, walau watapata usingizi.

Lakini tupeleke mwongozo kwa wananchi kuwajulisha kwamba siyo maana yake wateremshe silaha au kwamba mannah imedondoka kutoka mbinguni, kwa hiyo, hakuna kazi, mambo yatakuja tu. Hili nalo ni tatizo.

Wakati tunategemea fedha za kutoka nje kwa maendeleo yetu halafu tunafuta kodi, mtu mwingine hawezi kuelewa. Sasa tuwaeleze wananchi kwamba tunafuta ghasia hii lakini sasa njia zenu za kujitegemea, michango yetu na maendeleo na kujenga shule huko lazima kuendelee. Mpeleke mwongozo wa kufafanua jambo hili, ama la sivyo tunaweza kuzua *confusion* na tukarudi nyuma kimaendeleo. *(Makofi)*

Kufuta kodi ya maendeleo kusisababishe watu kurudi nyuma kimaendeleo. Tafadhali sana hili tusipoliangalia linaweza kuwa ni *counter productive.* Nia nzuri iambatane na mikakati mizuri.

Jambo lingine ambalo nataka nilitolee maoni ya haraka haraka ni suala la vijana. Vijana ni nguvu kazi kubwa katika nchi yetu. Lakini vijana siyo kwamba wamesahauliwa, lakini vijana hawa tusipoangalia nguvu za giza zitawatumia ovyo na watageuka maadui wa nchi hii. Vijana siyo kero, lakini vijana wako vijiweni. Vijana ndiyo wako magerezani, vijana wanaangamizwa na Ukimwi. Vijana wanaanza kupoteza matumaini. Mikakati gani tunaiweka ili kuwatumia vijana wetu? Hili ni jambo la msingi. *(Makofi)*

Nina mawazo mengi hapa, lakini muda hauruhusu. Ningependa kusema wazi kuwa Taifa lolote linalopuuzia mahitaji muhimu ya vijana wake, Taifa hilo haliwezi kudumu, linajikana lenyewe.

Ukurasa wa 23 kifungu cha tano pale, wanasema vijana wanakosa ajira mijini na vijijini. Ni kweli vijana wengi wameanza kukimbilia mijini. Mtu hawezi ku-*afford* kufa *carelessly* kama anajua kwamba kwa kupiga ngwala anaweza kupata chochote kutoka kwako, kwa nini asifanye hivyo? Lazima tuzuie hali hii isitokee? Kama hakuna njia ya ku-*arrest situation* hii jeshi hili linazidi kukua na usalama wa wale walio nacho unapungua. Kwa hiyo, napendekeza hapa kwamba kuanzishwe *programmes* za kazi kwa vijana, kuwahusisha vijana katika kazi.

Kwa mfano, mradi wa Mheshimiwa Edward Lowassa, wa kuleta maji Shinyanga. Weka makambi ya vijana, njia yote ile. Peleka vijana wa JKT wasimamie wale vijana na kuwapelekea nyama na chakula. *Keep them busy*. Washirikishe katika Miradi ya kufyatua matofali, miradi ya kujenga nyumba, miradi ya kuchimba mawe na mchanga. *Keep them busy.* Huu ni wakati mzuri wa kujenga mikakati ya kutumia vijana katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ningependa nirudie tena kusema kwamba Serikali hii inasikiliza watu na kwamba kwa upande wa nguvu kazi, tuna tatizo la kimsingi. Tukitunga sheria kwamba watu wafanye kazi kwa lazima, tutapingwa na wakubwa.

Sasa tutumie JKT. Kila kijiji kiwe ni kambi ya JKT, chini ya JKT ili kuwafanya vijana wafanye kazi kwa nidhamu, nchi hii itafufuka mara moja kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupatiwa nafasi hii ili nami niweze kutoa yale ninayoyaona katika Bajeti yetu ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niseme kwamba Bajeti hii imedhihirisha kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ni Serikali ya wanyonge na watu ambao wanatakiwa kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii haidhihirishi tu ila inawaonyesha wenzetu wa Upinzani kuweza kuangalia na kujipima ili waweze kujua nini wafanye kwa maendeleo ya nchi hii na Bajeti hii iwe ni funzo kwao kwamba CCM haina utani na inawaachia pengo kubwa la kutokufikiria kwenda mbele kama watashindwa kubadilika sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii ni nzuri sana. Lakini ni vizuri tujue kwamba watu wengine watafikiri ni Bajeti ya kufanya watu wakae tu bila kufanya kazi. Nadhani iko haja ya kila mtu afanye kazi. Hili tusioneane haya hata kidogo. Lazima kila mtu awajibike na afanye kazi ya kumpa tija binafsi au iwe ya Serikali. Tumekuwa na mambo mengi mara mikataba ya wateja. Tumetoa hapa na tumepoteza muda mwingi kwenda kuisikiliza na kuiangalia. Lakini matokeo ya mikataba hii iko wapi? Tumepoteza mambo mengi sana na kwa muda mwingi bila hata kuweza kupata matokeo yake mazuri.

Mimi nadhani hili tuliache, maana na makaratasi yanayoandikwa mambo ambayo hayana tija ni uharibifu na upotevu wa fedha ya umma. Tuwe waangalifu. Naomba mipango yetu iende na kuleta manufaa na maendeleo ya watu, hapo ndipo tutakapokwenda. Ukiona huko nje kila Wizara na Taasisi zinazotegemea Bajeti hii sasa ndiyo wanajua kufika kwao kumefika. Madai yao ya posho ya miaka ya nyuma sasa ndiyo *voucher* zinasogezwa ili Bajeti ikishapita walipwe posho hizo. Matokeo tunarudi pale pale hakuna kinachoonekana.

Nilikuwa naomba kwa kweli, sasa tuelewe na Serikali iwe na utaratibu, kuwa hela hizo za Bajeti za Wizara kama alivyoonyesha tusije tukamwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba ni *Father Chrismas*, kwamba anatoa fedha hizi kama zawadi tu. Lazima tuwe na chombo kitakachodhibiti. Wote watakaopewa fedha hizi walete matokeo ya kazi zao. Haya mambo ya kubaki na viporo na magofu tuyaache. Waziri ambaye mradi wake hautakwisha kwa fedha iliyopangiwa pale, kwa kweli huyu tumbane na aje ajieleze mbele ya Bunge kwa nini ameshindwa kukamilisha miradi aliyotoa na kuthibitisha yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Hiyo ndiyo itakayotusaidia kwa kweli, halafu kila Wizara itoe taarifa kwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha tumpe mamlaka ya kuchunguza na kutathmini kama *value* ya kazi ya fedha zile inalingana. Lakini sasa inakuwa tunamchukua *Auditor General* ndiyo aje afanye mahesabu. Mwishoni tunakuta hela nyingi zimetumika na hatuna la kumfanya.

Mimi nadhani liko tatizo, tumemweka *Pay Master General*. Hivi *Pay Master* anawachukulia hatua gani? Kwa nini kila mwaka *PAC* ione matumizi mabaya, hatuoni wanaokamatwa vizuri, bado wanaendelea wale wale na hela zinazidi kupotea mwaka hadi mwaka. Nadhani tubadilishe, kama *Pay Master General* hana uwezo basi nafasi hiyo haina haja ya kuwekwa, tukamweka mtu anapata sifa bure na bila kazi yoyote yenye maana kwa maendeleo ya nchi yetu. Nadhani hilo tuliangalie kwa namna hiyo. Watu wanaoonekana matumizi yao ni mabaya, wala hawa tusiwaite ni ndugu zetu, tuwahesabu ni watu wabaya, ni maadui kabisa na hawana haja hata ya kuitwa ndugu, hawa tusiwaite ndugu ni maadui kabisa. Tukianza kuacha masuala haya mikononi mwa watu hawa wanavyotaka, hatuendi mahali. Nadhani hilo litatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kodi zingine ambazo ni ndogo ndogo sana, lakini zinakatisha tamaa na zinapingana na maendeleo tunayolenga, tunasema tujali mazingira. Ndugu yangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, anakazana na mazingira. Lakini umeme, hata ukitumia kidogo lazima *VAT* ipo pale. Hivi hii inawapa moyo wananchi kuingiza umeme kwa matumizi yao?

Simu, tunasema zinatokea. Hizi simu sasa zitabaki ni za watu wachache tu. Tukiingiza bahati katika sehemu hizi za umeme, maji, tunawafanya watu kwa kweli waishi na maisha magumu sana, basi walipie gharama ile ambayo wameitumia na kwa manufaa na maendeleo yao. Hii itatusaidia sana. Nilifikiri ni vizuri liangaliwe hilo na Waziri ajaribu kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ieleweke kwamba katika uchumi wetu unategemea sana usafiri. Kwa hiyo, suala la barabara ni la muhimu sana na tusifanye mchezo wa kuweka makandarasi hawa wa kubabaisha, analima, baada ya miezi miwili barabara vumbi tupu. Kwa kweli hii hatuendi mahali. Tunazidi kujiletea matatizo tu na vile vile hata hii reli tunayozungumzia, tuna reli moja tu hapa katikati hapa. Hivi kweli tunashindwa hata ku-*maintain*? Wakati jumuiya yote kutoka huko Kigoma, Mwanza, Bukoba, Dodoma wote wanategemea hiyo reli. Hivi maana yake nini. Hivi tunataka tuje tumbinafsishe mtu ndiyo aje atutengenezee? Hivi tuna usalama na reli hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kwa kweli Waziri aangalie, akokotoe mahali, angalau asaidie kwa kweli kuwezesha reli hii iweze kufanya kazi. Kwa taarifa hii reli ya kwenda Singida au Mpanda, hii kwa kweli inakwenda kwa bahati ya Mungu tu. Tusije tukawa tunasherehekea matatizo na vifo vya watu wakati tungeweza kupisha na kupunguza matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawatatuelewa, tumepata janga kubwa. Kwa hiyo, janga hili angalau tujaribu kulifuatilia na kulipunguza kama ni bahati mbaya itokee ni bahati mbaya tu na ikitokea mara moja kwa miaka mingapi afadhali. Lakini sasa inakuwa kila mara mabehewa ya mizigo yameanguka hivi, mara nini. Sasa hii inatuonyesha kama hatuna thamani nayo reli hii na hatutii nguvu nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninaomba tuache lugha ya maneno, tufanye vitendo. Mimi nashukuru sana Serikali kwa kule kutoa punguzo la mbolea au pembejeo kwenda mikoa hii minne ambayo ni ya uzalishaji. Ninaishukuru sana. *(Makofi)*

Tumewahi kusema huko nyuma kwamba jamani, tupeni pembejeo mtudai chakula. Sasa leo hii tunahangaika pembejeo hatukutoa tunalia njaa, njaa. Sisi tupeni pembejeo na mtudai chakula. Nina hakika tukipewa mbolea mapema, mwaka kesho hatuna haja ya kuhangaika kwa chakula. Hatuna haja ya kuhangaika. *(Makofi)*

Vile vile tukubali kwamba malengo yawepo. Hii tulifanikisha wakati wa Siasa ni Kilimo, watu walikamilisha malengo yao. Kilichokuja kuondoa mipango ya malengo ni nini? Mpaka sasa tunashindwa kuwa na malengo yenye ufanisi ni kitu gani? Watu wanasema *Extension Officers*. Tulikuwa na katabu cha Siasa ni Kilimo kilitoka mwaka 1972, kile kitabu kimeeleza kila kitu na kila eneo katika nchi hii. Wala hatuna sababu sisi. Mimi nasema huko kwetu Kusini huko Nyanda za Juu, hatuna haja ya *Extension Officers* maana sasa hawa wanatakiwa wawe wasomi wa ngazi yake, tupeni pembejeo. Kitabu kile kinatusaidia kabisa. Sisi tutafanya na kuzalisha inavyotakiwa. Hatuna sababu tusipoteze muda sana.

Halafu suala la kutuletea mbolea ni la kimapinduzi kwa kweli. Mimi nimepata simu nyingi karibu ya 40 sasa hivi kutoka Mkoa wa Mbeya, wakishangilia na kushukuru Serikali iliyofikia uamuzi huo na wameniahidi na wakasema ukipata nafasi ya kusema waambie kwamba wao wako tayari na wanaanza mwezi ujao kutayarisha mashamba kwa ajili ya kilimo cha mwezi wa kumi na moja na hili ninalisema kwa moyo safi na kwa nia njema ili tuweze kufanikisha shughuli zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kidogo tumezoea huko kwetu akina mama msione ajabu, hatuna Wenyeviti wanawake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunaajiri wafanyakazi, watumishi walipwe kijijini na kodi hawatakusanya. Basi kipimo chao tukiweke katika uzalishaji. Kiongozi yoyote katika kijiji ambaye atashindwa kuzalisha, Katibu Tarafa ana pikipiki, hawezi kusimamia uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara katika Tarafa yake. Hivi anatufaa nini huyu. *(Makofi)*

Tusioneane haya, vitu hivi tuviamue kwa lengo la kuleta mafanikio na kila mtu na nafasi yake na kazi yake ajibu hili kwa mafanikio ya Taifa hili. Hapo ndipo tutakapoweza kufanikisha na uundaji wa Idara zingine zingine hizi na vi-Tume ambavyo kwa kweli havileti lengo la mafanikio, ni vizuri tukaviacha na hali hii ya ujambazi inayozidi tunaomba na Wizara hii ya Katiba na Sheria, ituletee wale waamuzi wa kesi. Watu wanafikiri kukosa au kufanya madhambi bila kuchukuliwa hatua wanadhani ni kitu kimehalalishwa.

Tunaomba basi Mahakimu wafanyiwe utaratibu wa kupatikana angalau kwa sehemu mbili waweze kwenda sehemu hii na hii, ingawa pia nayo si kazi njema kwa Mahakimu maana usalama wao haupo. Tunasema kwamba kwa kweli wajitahidi ili waweze kutusaidia kubadili hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaomba niseme kwamba mimi binafsi naunga mkono Bajeti hii na maelezo ya Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuwa ndiyo msingi na msimamo wetu na hasa uwakilishi wa Ilani yetu ya Uchaguzi wa mwaka 2000 na ninaomba hata wenzetu wapinzani walione hili na waone

kwamba watakapokuja kupata baada ya miaka kama 74 hivi, basi wafuate *speed* hiyo ili iweze kuwasaidia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nijumuike na wenzangu katika kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge hili. Natumaini ya kwamba wameanza kuelewa kwamba nyumba hii ni nyumba muhimu, nyumba maalum, inahitaji heshima zake katika lugha na hata katika kuonekana mwenyewe kwa sababu sisi ndiyo tunaowawakilisha Watanzania. Tunawakabirisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, ningependa niunge mkono moja kwa moja na mia *plus* hii Bajeti na nitakayoyasema yatafsiriwe kama uboreshaji na upeanaji wa mawazo ili kuimarisha tu utekelezaji kwa sababu Bajeti hii itahitaji mikakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkakati wa kwanza ambao ninao na ninadhani Mheshimiwa Waziri ataukubali, ukiangalia katika majedwali tuliyopewa ni kwamba utekelezaji wa Bajeti mwaka 2002 ulikuwa asilimia 52, mwaka huu tunataka angalau ifike asilimia 90. Katika hilo ningeomba pia kwamba ni vema tuweze kupata maelezo, asilimia 52 ilitekelezwa wapi, katika maeneo yapi na katika shughuli zipi na pale ambapo tumekwama, tumekwama wapi. Haya ni ya muhimu sana ili kuona namna tutakavyosonga mbele kwa sababu Bajeti tuliyoletewa hapa inaonyesha mia kwa mia, lakini ikitekelezwa asilimia 52 hata basi tujue ni maeneo yapi ambayo yametekelezwa na ni wapi katika nchi hii ya Tanzania. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuhusu hili pia nipendekeze kitu ambacho kinalingana na *TRA*. *TRA* ni Taasisi mpya siyo ya miaka mingi, tulipoona ya kwamba ukusanyaji wa kodi unatupa matatizo tuliunda *TRA* ili iweke msukumo na mimi napenda kuwapongeza *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya, si kazi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwamba kuwe na Taasisi nyingine mpya itakayojulikana kama *Tanzania Budget Implementation Authority (TABIA)*, Mheshimiwa Waziri nadhani ananisikiliza vizuri. *TABIA* ili *TRA* inapokusanya na kudhibiti ukusanyaji na wale wanaokiuka, *TABIA* inasimamia ufanisi, *the value of the project* kwa mfano kama barabara inajengwa, kweli hiyo barabara inalingana na zile pesa au kama ni shule imejengwa, inalingana na zile pesa.

Kwa hiyo, ningependa nitoe hilo pendekezo, nadhani mapendekezo ni kwamba kila mtu ana haki ya kutoa, mtu aliyetoa pendekezo la *TRA* hakuwa ananizidi akili kuliko mimi ninayependekeza *TABIA*.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri natumaini atalipokea pendekezo langu la kuwa na *TABIA* itakayotuwezesha kudhibiti na kufuatilia na kama ilivyo *TRA* kila Wilaya, iwepo pia *TABIA* katika kila Wilaya, hiyo itatuwezesha kusonga mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niliseme ni kwamba Bajeti hii imepangwa vizuri, wasiwasi wangu ni mikakati ya utekelezaji, kwa mfano katika eneo la mifuko ya uwezeshaji, ipo mingi tu, *TASAF* na kadhalika, tuna mifuko kibao. Lakini mifuko hii mingine ambayo tutaianzisha ya uvuvi, mifuko ya mifugo na pia ya wakulima, ni vema basi tuilinde ili isije ikawezesha makundi ambayo si wafugaji, si wavuvi na pia si wakulima. Maana yangu ni kwamba inawezekana mtu ambaye havui akachukua zile pesa akawafanya wenzake vibarua.

Kwa hiyo, kama hukumwezesha mvuvi utakuwa umemwezesha huyu ambaye anakwenda kule anawafanya wenzake ndiyo vibarua wake. Unaweza pia ukamfanya mtu akanufaika na mfuko huu kwa sababu anajua namna ya kuzitafuta hizi pesa akazitumia, watu wengine wakamfugia na yeye anakuwa tu anatumia matokeo yake.

Mimi natumaini ya kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha alipoweka mifuko hii maana yake ni kumwezesha Mtanzania, kumwezesha Mtanzania wa chini ya kwamba huu mfuko kama ni wa wafugaji

basi apate yule Mmasai, ndiyo apokee zile pesa, kama ni mvuvi apate yule Mkerewe na kama ni mkulima apate yule wa Kusini anayelima mahindi, apate Msukuma, apate Mchanga na kadhalika. Kwa maana hiyo siyo kuwepo na *middleman* na hili nalisema kwa makusudi kwa sababu tumeona katika uwezeshaji wa ubinafsishaji, ukiuangalia kwa ndani haujamfanya huyu anufaike. Tazama katika sekta ya madini, unapokuwa umekalia dhahabu miaka nenda rudi halafu mtu anakuja anasema hapa kuna dhahabu, tulitegemea yule mtu angebadilika mara moja siyo angehama halafu na yeye akabaki kuhangaika kama wale ambao hawana dhahabu au mtu aliye na ng'ombe anakutwa anahangaika kama vile hana ng'ombe na mfuko wa ufugaji upo, hanywi maziwa wala nyama, wanakula watu wengine.

Sasa uwezeshaji huu ndiyo Mheshimiwa Waziri nadhani ataufikiria kwa makini kwa sababu kupeleka tu kwenye Taasisi kama *BIT*, mkulima wa kawaida, mfugaji wa kawaida na mvuvi wa kawaida hajui hata *BIT* iko wapi, kuhangaika mpaka afike huko itamchukua muda. Kwa hiyo, nadhani ni utaratibu tu, mimi sipingi mifuko hii, lakini ni utaratibu wa kawaida ili kuwawezesha hawa watu wa kawaida ambao ndiyo wamefanya kazi miaka yote kwa uaminifu kabisa ili waweze kuyabadili maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka kulizungumzia, ni suala la mitaji. Mitaji nitachukua sehemu ndogo tu ambayo ni ya mtu wa kawaida, *Bank*. Sasa hivi ukipeleka *Bank* pesa zako zikakaa kule, kwa *interest* unayopata na *inflation rate* ukikaa kwa muda kama wa miaka miwili, mitatu, unakuwa umepoteza. Sasa hilo nalo napenda tusaidiwe katika kulielewa kwa sababu miaka ya nyuma watu walikuwa hawaweki pesa *Bank*, tukawahamasisha waweke pesa *Bank* ili tuweze kuwa na usalama wa pesa zao na faida; je, inapofika mahali zile pesa zinapungua thamani, mtu anaweka tena chini ya mchago?

Kwa hiyo, hilo nalo lizungumzwe katika mkakati wa kuondoa umaskini, hatuwezi kuondoa umaskini kama *savings* zitakuwa zinapungua thamani kwa sababu ya sera ya Mabenki ya kutoangalia jinsi mtu anavyoweza kunufaika na *saving* hiyo anayoifanya katika *Bank*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulisema ni juu ya msukumo wa kilimo. Kumekuwa na msukumo mzuri sana katika Bajeti hii kuhusu kilimo. Nataka kuwapongeza wenzetu wa Mikoa minne ambayo watapata pembejeo, hongereni sana, najua mtaifanyia kazi.

Lakini napenda kuweka utani kidogo tu kwamba msisahau mkabaki kutafuna ugali bila kitoweo. Kwa hiyo, nafikiri ya kwamba Mheshimiwa Waziri, katika mikakati yake na Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta wanaohusika, watazingatia sana lishe ya Mtanzania siyo ugali tu, ni lazima ale samaki, ni lazima ale mayai na pia ni lazima ale nyama. Ninamsifu Mheshimiwa Waziri Edward Lowassa, alivyokazana kutuambia tunywe maziwa, hivi vyote ni sehemu ya chakula, tusipofanya hivyo, tutakuja kushangaa wenzetu wamelima mahindi na bado Watanzania wanakuwa na kwashakoo.

Kwa hiyo, mimi nataka niliweke hilo nadhani Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Mawaziri wa Sekta mbalimbali wataungana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili watakapoanza sasa utekelezaji Sekta zote hizi zifanye kazi kwa pamoja ili huyu Mtanzania apate mahindi kutoka Mikoa hii minne na Mtanzania huyu aweze pia kupata vyakula vingine kutoka sehemu nyingine kwa sababu na sehemu hizo nazo zimeimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba haya ya kuimarisha uchumi hatutaweza kuyatekeleza kama hatutakuwa na amani. Hivi tunaingia katika Bajeti hii katika wimbi la ujambazi, ujambazi unaondeshwa na watu wasiokuwa Watanzania, mara nyingi tumekuwa tukijitazama sisi wenyewe kwamba sisi watoto wetu wamekuwaje, kumbe ndani yetu kumekuwa na mchwa anayetutafuna.

Napenda kuwapongeza sana Polisi ni kwamba waendelee na kazi hiyo na sisi tusianze kuwaandama, tukianza kuguna guna tutawanyima nguvu, acha wafanye kazi, vijana wafanye kazi na ni vizuri ya kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameangalia katika mgao kwamba amewaongezea. Sasa tunachokitaka kama agizo lilivyotolewa, tushirikiane, sisi tunaotoka katika maeneo ya mpakani tumewaona wageni wengi wamekuja kujificha katika maeneo yetu wakitumia sababu mbalimbali za kufanya biashara na mambo mengine, hawa wanatuvurugia nia yetu ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi.

Kwa hiyo, mimi kupitia kwa Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tuendelee kushirikiana na Polisi na pia tushirikiane na kila mtu ili tuwafichue hawa ili tuweze kuishi kwa amani na tuweze kulitekeleza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ningependa kusema kwamba hii Bajeti bado inahitaji tafsiri kwa sababu Bajeti ni Bajeti, tafsiri itatolewa na Waheshimiwa Mawaziri, lakini wakati mwingine tunaishia hapo, sisi Waheshimiwa Wabunge tunajitahidi kufanya tafsiri lakini na wataalam lazima waifanye tafsiri na pia kule kwenye *Local Government* tuna matatizo, usipokuwa na *DED* mzuri na mweka fedha mzuri, wao wanafanya kazi ya kuzitafuna hizi fedha. Ukerewe kuna fedha zimeliwa shilingi milioni 14, mtu anachukua *with the single signature*, sasa yule atakwenda Mahakamani kwa sababu atahonga kwa zile pesa atashinda.

Mimi napendekeza kwamba watu wa namna hiyo ni kunadi nyumba zao na vitu walivyonavyo ili hizo pesa zirudi wala Mahakamani tusiende, wewe unakuta umeshachukua pesa tunakuuliza ziko wapi hutuambii, tunanadi vitu ulivyonavyo. La sivyo tukibembelezana Bajeti hii inakwenda kutafunwa na mchwa na tutakuwa tunawaangalia wanahamisha kutoka hapa wanakwenda pale wanarudi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa *Local Government*, tunakuomba sana angalia tena watumishi wako katika *Local Government*, mtu mbovu hawezi kutoka Wilaya hii akapelekwa Wilaya nyingine, unarudisha nyuma maendeleo. Angalia hii Bajeti tunataka tuitekeleze *seriously* lakini watu watakaotusaidia sana kule ni Ma-*DED*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Serikali kwa kufuta kodi. Wamefanya vizuri sana kufuta hiyo kodi kwa sababu ilikuwa ni kero ambazo zilisemwa katika Ilani ya Uchaguzi ya kwamba tutafuta kero na wale wote ambao hawajasoma Ilani ya Uchaguzi uwe wa Chama cha Mapinduzi au Chama kingine tunaomba uisome. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Nadhani unaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHANI HASHIM KHALFAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili ambazo tumezisikiliza siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Napenda kuwapongeza sana kwa hotuba zao nzuri walizoziwasilisha kwetu kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuwapongeza wataalam wote katika Wizara zote hizi mbili, wataalam wa upande wa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji na wataalam wa Wizara ya Fedha. Naamini hiki tunachokisifia hapa ambacho ni kizuri ni wao ambao wamekishughulikia usiku na mchana na kikaweza kufika kwetu kikiwa na sura hiyo ya ubora. Kwa hiyo, nawashukuru na napenda niwapongeze sana wataalam katika Wizara hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ningependa kuipongeza Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge, kwa kazi nzuri iliyoifanya ya kuchambua Bajeti hii na jinsi walivyotoa maelezo yao leo wakiwa wameyagusia maeneo yote muhimu. Kwa kweli ile inathibitisha jinsi walivyokuwa wamelichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili, utaalam ambao wameonyesha katika kuchambua na jinsi walivyoweza kusaidia kurekebisha pale ambapo palikuwa na mapungufu hapo nyuma. Kwa hiyo, nataka niwapongeze wote katika Kamati hii ya Fedha na Uchumi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, ningependa mimi kwa upande wangu nichangie katika eneo la kodi na ada zinazotozwa na Serikali za Mitaa na hii iko katika kipengele cha 17 na kipengele cha 59 cha hotuba ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nataka kuzungumzia maeneo hayo? Nataka kuzungumzia maeneo hayo nikijaribu kutoa sababu zinazonifanya niunge mkono hoja ya Serikali ya kufuta kodi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sielewi vizuri lakini wenzetu wengine wanapodai kwamba uamuzi huu unatokana na fikra zao wanaweza kuwa sahihi, lakini labda tuwakumbushe tu kwamba, habari tulizonazo au taarifa mbalimbali ambazo wanaweza kuziona sehemu mbalimbali zinaonyesha kwamba nchi hii imekuwa ikitawaliwa na Chama cha Mapinduzi tangu wakati wa Uhuru mpaka leo, lakini mwaka 1968 Serikali ilifuta kodi hii wao hawakuwepo. Sasa kama ilifutwa mwaka 1968 na hawakuwepo leo wanasema ni wazo lao inawezekana, tukubali tu lakini nadhani si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1992 kodi hii ilirudi na tukawa nayo mpaka kufikia mwaka huu wa 2003 tumekuja kuiondoa. Kwa nini tumeiondoa? Mimi siamini kwamba yalielezwa tu mambo juu juu na wenzetu basi sisi tukayaona mazuri tukayafanyia kazi hapa, naamini Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu, Serikali ambayo inaamini juu ya masuala ya utafiti na Serikali ambayo inapenda kuchambua mambo ambayo yapo mbele yake na kuona nini cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kimefanyika? Labda ni machache tu nataka nigusie kwa yale ambayo pengine yatasaidia ili tuweze kuelewa Serikali ilikuwa imeelekea uko kwenye uamuzi huo kutokana na kitu cha namna gani.

Katika kipindi cha Aprili, 2000 hadi mwezi Juni, 2001 kulikuwa na utafiti ambao ulifanywa na *Urban Authorities Partnership Program.* Mradi huu ulifadhiliwa na *DFID,* hawa wenzetu waliliona tatizo hili na walifanya utafiti kwenye Halmashauri 12 katika Mikoa nane ya Tanzania, baadaye waliamua kushughulikia zaidi au kujizatiti zaidi katika Halmashauri tatu tu za Tanzania ambazo ni Mbeya, Mtwara Mikindani na Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini walichokiona huko? Kwa kweli walichokiona nadhani ndiyo hicho ambacho kimekuja kufanyiwa kazi na Serikali, wingi wa kodi ambazo nyingi hazina maana, basi tu ziko pale ili kuwasumbua watu, gharama ya kukusanya kodi hizo ni kubwa kuliko faida inayopatikana na pia taabu nyingi kwa wananchi mbalimbali katika maeneo mbalimbali.

Kwa hiyo, hiyo nadhani ilikuwa moja ya mambo ambayo yalikuwa yanafuatiliwa kwa karibu sana na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoe mfano wa hiyo kodi ambayo tunaizungumzia leo kwamba imefutwa. Kodi hii kwa kweli ilikuwa adha kwa wananchi hasa Vijijini. Mimi natoka katika eneo ambalo kwa kweli ndugu zangu kule ni watu wa kipato kidogo sana, watu wenye mapato duni kwa hiyo, hii kodi ilikuwa inawasumbua sana. Nataka nieleze hali ilivyokuwa mbaya katika maeneo kama yale ya kwetu kule Pwani, tuchukulie mfano wa Wilaya ya Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bagamoyo kwa Sensa ya hivi karibuni, Wilaya ile ina wakazi 230,164. Ukichukua labda wastani wa asilimia 25 kwamba hao ni watu wanaoweza kulipa kodi, unakuta kwamba pengine unazungumzia watu 57,500. Lakini kodi iliyokuwa ikilipwa katika maeneo yote yale katika Wilaya hiyo kwa kipindi cha miaka mingi iliyopita ilikuwa kwenye wastani wa shilingi milioni saba tu. Sasa shilingi milioni saba tu na kodi yetu sisi, kiwango chake kilikuwa cha chini sana. Kwa upande wa Bagamoyo ni shilingi 1,000/= na mpaka hivi sasa inafutwa ilikuwa ni shilingi 1,000/= lakini bado mtu alikuwa anashindwa kuilipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kodi hiyo ya shilingi 1,000/= kodi inayokusanywa ni shilingi milioni saba, ina maana ni watu 7,000 tu waliokuwa wakilipa kodi hiyo, lakini tukikumbuka kwamba kuna watu ambao wangestahili kulipa kodi kama 57,500 wananchi 50,000 hawalipi. Nimetoa mfano wa Bagamoyo kwamba watu 50,000 hawalipi, lakini hali iko hivyo hivyo kwa nchi nzima. Utafiti huu uliofanywa na hawa wenzetu ulionyesha kwamba uwiano wa kukwepa kulipa kodi yaani katika ile hali ya kukwepa kulipa kodi Tanzania nzima ni uwiano 1 kwa 167. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha kuridhia kulipa kodi, kwangu mimi kule ilikuwa kwenye kiwango hicho cha asilimia kama 12 tu ya watu walinaostahili kulipa kodi, kwa hiyo, asilimia 88 walikuwa hawalipi na walikuwa wanakubali kupiga piga chenga kwenye mikorosho, kwenye mitaro na nini alimradi asikutane na mtu anayetafuta kodi hii. Lakini nchi nzima kiwango vile vile hakikuwa kizuri sana ni asilimia 38 tu ya watu ndio ambao wako radhi kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kodi ziko zaidi ya 60 kwenye Halmashauri, nilikuwa najaribu kupitia baadhi ya vitabu vya Halmashauri juzi juzi tu nikawa naangalia hizi kodi na wakati huo pendekezo lilikwishatolewa kwamba Halmashauri ziangalie kodi ambazo wangeweza kuzifuta.

Sasa wakati napitia pitia kodi hizi kitu cha kushangaza ni kwamba kodi ziko nyingi, lakini tukiizungumzia hiyo kodi ya maendeleo ambayo ndiyo iliyokuwa inawakera watu kupita kiasi, makusanyo katika kodi hiyo ya maendeleo kwa kiwango chochote cha pesa ambazo zilikuwa zinakusanywa katika Halmashauri asilimia 69 ya kodi hiyo ilikuwa inatumika kwa masuala ya utawala katika Halmashauri zetu, asilimia 12 ilikuwa ni gharama ya kukusanya kodi hiyo, sasa 12 na 69 ni 81. Asilimia 81 ya kodi hiyo ni gharama za ukusanyaji wa kodi na utawala tu, maendeleo yako wapi? Kodi ya maendeleo lakini hakuna maendeleo ni asilimia 19 kama inakumbukwa ndiyo inayopelekwa moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo lakini adha hii yote ni ya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa uchambuzi wa karibu sana katika vyanzo hivi 60 vya kodi mbalimbali umeonyesha kuwa vyanzo vitano vikubwa katika Halmashauri mbalimbali au karibu zote, vyanzo vitano vikubwa vinachangia asilimia 70 ya makusanyo yao na vyanzo kufikia 10 au 15 vinachangia asilimia 83 ya makusanyo yao.

Kwa hiyo, mimi nataka kuipongeza Serikali kwamba ilipoamua kufuta kodi hizi na kubakiza nane, nadhani wamefanya utafiti wa kina sana kwa sababu kila unapoangalia unaona kuna usahihi wa kiwango cha juu sana, si kazi ya kubahatisha, haipigwi ramli hapa, wanafanya utafiti wa kina. Wamesema tubaki na kodi nane, mimi nafikiri ni sawa kwa sababu kama ninavyosema ikiwa kodi tano kubwa zinachangia asilimia 70 ya mapato ya Halmashauri au kumi zinachangia asilimia 83 ya mapato ya Halmashauri hizi nyingine 50 ni za nini? Ni vurugu tu. Kodi hizo hizo nyingine utakuta gharama ya uchapishaji wa stakabadhi au vitabu vile vya kukusanyia kodi ni kubwa kuliko kodi wanayokusanya, kunafanyika nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisije nikasahau kwanza niiunge mkono hii hoja moja kwa moja. Nawaomba wenzangu kila mmoja kwa namna yake alivyoiona, lakini kwa kweli ziko sababu za msingi na pia ziko sababu za kisayansi katika kuiunga mkono hoja hii, hakuna ubishi. Tukitaka kuongea kisiasa tunaiunga mkono Ilani yetu ipo na tukitaka kuongea kisayansi unaweza ukachambua na ukaona ukweli kama huu ambao tunauzungumza. Kwa hiyo, kimsingi ni kwamba kwa kweli namuunga mkono Mheshimiwa Waziri kwa hii hoja ambayo ameileta, mimi kwa kweli naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nimalizie kwa tatizo dogo tu kwamba liangaliwe kama inawezekana, nalo ni kodi inayowekwa ya asilimia 15 kwenye dawa za mbu na asilimia 10 kwenye vyandarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule Pwani tuna tatizo la mbu wengi sana na mbu ndiyo mdudu mmoja anayeeneza ugonjwa wa malaria ambao sasa hivi ndiyo adui namba moja katika kuua watu wetu hapa nchini kuliko hata Ukimwi, Malaria inaua zaidi, tukizugumzia kwa *rate* ya vifo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa nataka kusema kwamba kama inawezekana, najua wataliangalia, kama inawezekana kwa sababu tuna kampeni ya kuwaomba watu watumie vyandarua vilivyowekwa dawa ili waondokane na balaa hili halafu tena tukianza kuweka kodi hizi si vibaya kwa sababu pengine itafidia kule tunakofuta lakini mimi nilikuwa naomba kwamba hili liangaliwe upya kwa sababu kwa kweli kwa maeneo ya Pwani au maeneo ambayo yana uzalishaji wa kiwango cha juu cha mbu hawa, watu wa maeneo yale tutaathirika sana.

Kwa hiyo, ombi langu ni kwamba ningeomba ikiwa inawezekana, hii kodi ya kwenye dawa za mbu za kuchoma na vyandarua iangaliwe kama inaweza kupatikana kutoka katika maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru sana na naunga mkono hoja na ninawaomba wenzangu tushirikiane katika kuiunga mkono. *(Makofi)*

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ningependa nitoe pongezi kwa Waheshimiwa Wabunge wapya na nawakaribisha sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Ukonga 519,086 ambao ndio wengi kuliko Jimbo lolote hapa nchini, ninapenda kutoa salaam zao kwamba wanaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapiga kura hawa zaidi ya nusu milioni wamefurahishwa na mambo kadhaa mazuri sana yaliyomo kwenye Bajeti hii ambayo ni pamoja na kufuta Kodi za Maendeleo, kufuta kodi nyingine zenye kero, kuongeza Bajeti kwenye vyombo vya usalama na ulinzi kama mnavyojua hali ya ulinzi na usalama si nzuri, vile vile wamefurahishwa sana na kupandishwa viwango vya pensheni za wastaafu na vile vile suala zima la kuongeza bajeti kwenye kilimo kama unavyojua kule Dar es Salaam Jimbo la Ukonga tunalima sana.

Kuna maeneo katika Bajeti yetu ambayo napenda kusema kwamba bado kuna upungufu na lazima sasa tuelekeze nguvu zetu kwenye maeneo hayo. Pamoja na kwamba Bajeti ni nzuri lakini maeneo kama manne ambayo nitayazungumzia naona kuna matatizo makubwa sana.

Kwanza ni eneo hili la Tanzania kuendelea kuwa tegemezi. Eneo la pili ni hili la nchi hii kuendelea kukusanya mapato madogo sana ukilinganisha na pato la Taifa. Tatu, kuna sera kadhaa za kiuchumi na kifedha ambazo ni mbovu na nne ni ukwepaji wa kodi na misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yote niliyoyazungumza ndio ambayo yanapelekea nchi yetu kuwa tegemezi. Nianzie na hilo la utegemezi. Inatia aibu kwamba bado asilimia 45 au 46 ya Bajeti yetu tunategemea wafadhili.

Katika mwaka huu tunaambiwa trilioni 1.176 zitakuwa ni misaada na mikopo. Lakini la aibu zaidi ni kwamba 35% ya mikopo na misaada hii bado inakwenda kwenye matumizi ya kawaida kwa maana ya kulipana mishahara. Bilioni 405 kati ya misaada hii inakwenda kwenye matumizi ya kawaida na bilioni 667 ndio zinakwenda kwenye miradi ya maendeleo na misamaha ni kama bilioni 103.

Kwa hiyo, bado hata Bajeti yetu ya Matumizi ya Kawaida tunategemea wafadhili, kwa kweli hii ni aibu. Mwaka huu tunaambiwa tutalipa mikopo bilioni 408 wakati ambapo mikopo bilioni 405 zitakuja kufidia Bajeti ya Matumizi. Kwa hiyo, kwa mwaka tunalipa tu ile sehemu ya mkopo wa Bajeti ya Matumizi ile Bajeti ya Maendeleo karibu bilioni 700 bado inaendelea ku-*accumulate* kama madeni ndio maana hatuwezi kumaliza kulipa madeni.

Tatizo hili linakuwa kubwa kwa sababu kama nchi bado tunakusanya mapato madogo sana ukilinganisha na Pato la Taifa. Sasa tunaambiwa mapato yetu tunayokusanya ni kama asilimia 12, 13 ya Pato la Taifa. Nchi za jirani zimefikia 20% ya Pato la Taifa lakini tutaambiwa aah, unajua wale wana *corporate economy* na kadha wa kadha. Sisi tunaijengaje hiyo *corporate economy?* Ndio swali la kujiuliza. Hii kuongeza kwa asilimia nukta kila mwaka 0.7, nukta moja, sasa tunaambiwa tutaongeza kwa asilimia moja kutoka 12 kwenda 13, tutafika huko asilimia 20 lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani yanayosababisha tusipande haraka sana kwa maana ya kukusanya Pato la Taifa kubwa zaidi ni haya mambo tuliyozungumzia ya ukwepaji kodi na sera fulani

fulani za kiuchumi. Nikianzia kwenye kodi, tumezungumzia suala la *VAT* toka ilipoanza kwamba hii 20% ilikuwa ni ya kuanzia na kwamba baada ya muda mfupi, tulidhani ni miaka miwili, mitatu, tutashusha kiwango hiki lakini mpaka sasa hakuna kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majirani zetu wanaendelea kupunguza sisi tumeng'ang'ania asilimia 20. Tulisema tukipunguza unapanua *tax base* ule wigo na *compliance* unaongeza kwa hiyo kimapato utapata mapato makubwa zaidi kuliko kung'ang'ania asilimia 20 lakini hili Mheshimiwa Waziri na watendaji wake kwa kweli hawalifikirii. Napenda nipate maelezo ni utafiti gani ambao wamefanya na kuona kwamba wakipunguza *VAT tax base* haitapanuka na *compliance* haitaongezeka na kwa hiyo hatutakusanya kodi nyingi ya *VAT*. Nina wasiwasi kwamba bado hawajafanya utafiti ndio maana wanang'ang'ania asilimia 20 bila utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Sera chache za Kiuchumi ambazo naona zinatufanya kama nchi tunakusanya mapato madogo sana na hivyo kuendelea kuwa na matatizo haya. Kama tungefanya yote haya tungeweza kupunguza sio Kodi ya Maendeleo tu lakini hata Kodi ya wafanyakazi ingeweza kutoka kwenye 30% tukalipa asilimia 25. Lakini kutokana na kutokusanya kodi inavyotakiwa tumeshindwa kupunguza kodi nyingine, nashukuru tumepunguza hiyo Kodi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sekta ya madini na hili kwa kweli tutalizungumza sana. Tanzania ni kama nchi ya pili au ya tatu Afrika kuwa na madini mengi, lakini ni aibu kweli kwamba sekta hii ina-*contribute only 2.5%* kwenye Pato la Taifa, ni aibu kubwa. Wa pili au watatu Afrika lakini 2.5% ndio ime-*contribute*. Kwa nini? Sera ya Madini ni mbovu, ni lazima tuseme ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2002 tuli-*export* shilingi bilioni kama 470 lakini sisi tunaambulia mrahaba wa 3% peke yake. Wizara ya Nishati na Madini imetuletea kabrasha linaloonyesha kwamba ooh tunapata kama 10.1% kwenye madini na mle ndani anaweka *Pay As You Earn*, anaweka *NSSF* zile sio mrahaba, sio mapato ya Serikali! Ule ni mshahara wa mfanyakazi, *Payee* ni mshahara wa mfanyakazi unaingiza kwamba eti Serikali imepata *Payee, is not true* ni mshahara wa mfanyakazi ambao *is part of* gharama ya uzalishaji. Sasa gharama ya uzalishaji unasemaje ni Pato la Taifa?

Kwa hiyo, ukweli ni kwamba bado tunapata *only 3%* hayo mengine yanayowekwa hapa kama gharama za uzalishaji huwezi kuleta kama Pato la Taifa, hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya kusema wanatumia *four billion* kila mwaka katika kuboresha miradi ya maendeleo kwenye maeneo ya jirani *this is nothing* na wana-*train* wafanyakazi, wana-*train* ili wawazalishie zaidi wapate hela zaidi. Huwezi kusema kwamba umefaidika kwa sababu ya *training*, wanafaidika wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine hizi *non renewable resources* kama madini unakuwa na mkakati, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anakimbia lakini nitamwambia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuwa na mkakati wa kuhakikisha kwamba una-*invest* kwenye *long term sustainable economic ventures* ambayo itasaidia wajukuu zetu. Kwa mfano, kwenye suala la madini, mapato yale tungeya-*invest* kwa sababu *this is non renewable resource* kwa mfano kwenye Bonde la Mto Rufiji, kwenye *Stiegler's Gorge Project* ambayo imekaa haijulikani inafanya nini ambapo tungepata umeme, kilimo cha umwagiliaji, uvuvi, maji Dar es Salaam na kadhalika na vizazi vyetu vijavyo vingesema kwamba angalau madini walimaliza lakini wametuachia mradi mkubwa wa *Rufiji Basin*, hatufanyi hivyo tunawaachia magofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikataba hii ni mibovu na mimi nasema bajeti hii tupitishe, lakini tulete hoja kabla ya Bunge hili kwisha kuomba mikataba hii ije tuiangalie upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya mrahaba mdogo *exemptions* chungu nzima kwa hawa wenye madini, *why?* Mrahaba upate kidogo bado unawapa *exemptions*, ni mbaya. Kwa kweli hii *actually* ni *unconstitutional*. Nasema hivyo kwa sababu kwa mujibu wa Ibara Na.138 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lina haki ya kupitia na kuidhinisha kodi mbalimbali. Sasa lazima tuidhinishe kodi hizi kwa mujibu wa Ibara hii, mikataba ile ije kwa sababu watapata misamaha mpaka lini?

Hili ni jambo zito. Katika suala la madini *we are not seeing beyond our noses* kwa kweli *we are acting as if this country is coming to an end by year 2005*, ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la utalii ambapo tunaambiwa wenzetu wana *mass tourism* sisi ni waangalifu sisi ni maskini, halafu tunakuwa waangalifu kwenye *tourism*. Tuna vivutio lakini tumepata bilioni 730 tu na wala haipandi mwaka 2001 na mwaka 2002 ni sawasawa tu *we are making no efforts* katika kupandisha sekta hii vile vile.

Lakini kubwa ni ukwepaji wa kodi, kwanza Serikali inalipa *VAT* kwa nini wengine tuwape misamaha kama vile *NGOs* na kadhalika*, why?* Kama *Government* inalipa kodi kwa nini kila mtu asilipe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukwepaji wa kodi katika sekta ya madini na mafuta hali ni mbaya sana. Tunaambiwa kwamba mwaka 2002 eti matumizi ya mafuta nchini yalikuwa kidogo kuliko mwaka 2001 *I can not understand this* kwamba tulitumia mafuta *only 1.1 million metric tons* mwaka 2001, mwaka 2002 eti ikapungua ikawa *1.06 metric tons* haiwezekani magari yanaongezeka. Kwa sababu wanachukua vyanzo vya kulipia kodi ndio wanajua matumizi ya mafuta yaliyokwepa kulipiwa ushuru, hayawi *captured* ndio maana inaonekana kwamba matumizi yanashuka, *it is not true*, matumizi yanaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuelewa eti Morogoro bei ya mafuta ni kidogo kuliko Dar es Salaam itakuwaje? Ni kwamba yale mafuta ambayo yako *on transit* yakifika pale ndio yanauzwa pale ndio maana mafuta yanakuwa chini. Haiwezekani pamoja na usafiri wa kuja Morogoro kwa nini mafuta yasiwe bei ghali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wenye migodi na ma-*agent* wa migodi wanamaliza nchi, ni wababaka uchumi kwenye suala hili la ukwepaji kodi kwenye mafuta. *Syndicate* ni kubwa viongozi wa Serikali, *TRA* pamoja na hao vigogo, lakini utakuta kwamba Watanzania wafanyabiashara hoi hoi pale, ana vituo vyake viwili anafungiwa kituo cha mafuta kwamba amekwepa kodi lakini vigogo vile haviguswi. Mheshimiwa Waziri hapa anakiri kwamba kuna ukwepaji kodi kwenye suala la mafuta badala ya kusema vile vile kwamba kuna rushwa kubwa ndio maana ukwepaji huo upo. Kwa nini asiseme la rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amesema vizuri sana kwamba hii *up front payment* kwenye mafuta itasaidia, lakini kuna suala la *contractors* ambalo ameli-*introduce* hili litaleta mwanya mkubwa. Mheshimiwa Waziri ondoa hii mambo ya *contractors* wa migodi kupewa misamaha ni mwanya mwingine mkubwa. Sisi kwenye udau tulipingapinga hii lakini kuna *Accountant* mwenzangu pale, *Auditor* mmoja pale anaonekana ndio mshauri mkubwa wa Serikali kwenye masuala haya akasema bwana lete hii mambo ya *contractors* wa madini, huu ni mwanya uondoke Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba tumefurahia *VEOs* kuwekewa mishahara, lakini *tax exemption* ya wafanyakazi kwa magari haya wanayoagiza waruhusiwe wayaandikishe kama *taxi* ikishawapeleka kazini angalau wafanye kazi kidogo wapate na Serikali ipate kodi kwenye *taxi* wasiwazuie kwa sababu ni *exempted*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Mheshimiwa Waziri kama mshauri mkuu wa Rais, amshauri sasa aunde Bodi mpya ya *NMB* kwa sababu imani inazidi kupungua. Bodi nchi nyingine ndio zinaendesha Benki. Benki nchi nyingine haiwezi kukaa *two weeks* bila Bodi imani ikaendelea kuwepo. Wakati tunaendelea kujadiliana, amshauri Rais mara moja iundwe Bodi mpya ya *NMB. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kama nilivyosema mwanzoni naunga mkono hoja, lakini haya niliyoyazungumza na hasa lile la kuleta hapa mikataba ya madini na hili la *contractors* kwenye migodi litaleta mwanya mkubwa sana wa ukwepaji kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja lakini pamoja na *VEO* lakini vile vile na Madiwani nao tuwaangalie jamani tuwape mshahara kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja haya yote ni katika kuboresha Bajeti hii ambayo ni nzuri sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lushoto, niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza wale wenzetu ambao wameingia Bungeni kwa kuchaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nianze kwa kuheshimu sana hotuba nzuri za Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Kwa mara ya kwanza napenda kusema kwamba sisi wote kama Wabunge tumekubaliana kwamba Bajeti hii ni nzuri upande wa Upinzani na upande wa Chama Tawala na yale yaliyosemwa tu kwa kejeli kwamba Maprofesa uchwara waliambiwa kwamba hawajui sasa tunaiga sera zao wanasisitiza tu kuonyesha kwamba Chama cha Mapinduzi kinaongozwa na viongozi wenye kuelewa wajibu wao. Chama kilishughulikia kwanza sera za uchumi wa jumla sasa ndio kinarudi kwa wale wenyewe walengwa wananchi. Sasa Uprofesa uchwara unaonekana pale unapotaka kuanzia chini kabla hujatayarisha nyumba yako.

Kwa hiyo, tulianzia juu sasa tunakwenda chini. Napenda kuwahakikishia kwamba mwaka 2005, aah, nafikiri ndio wasiwasi wao kwamba sasa hawa watapita bila wasiwasi wowote, kupita tutapita tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimehesabu mambo ambayo katika Bajeti hii ni ya historia hayajawahi kutokea. Bajeti hii imeondoa kero 16 kwa mara moja, ni kitu ambacho sio cha kawaida katika Bajeti zote. Juzi nimeona kwenye gazeti kuna mtu amelinganisha Bajeti zetu za Afrika Mashariki, Tanzania, Uganda na Kenya ukiangalia *highlights* za Bajeti ya Tanzania unafurahi kwamba sasa tunatawala nchi na nchi inaonekana kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero hizi ukiziangalia kwa ujumla, mimi nimejaribu kuorodhesha tu hizo 16 kwanza ufutaji wa Kodi ya Kichwa au Maendeleo.

Pili, kutenga fedha kwa ajili ya kudumisha kilimo, tatu kutoa fedha moja kwa moja katika Wilaya ili maendeleo yahamasishwe vizuri, nne, kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga uwanja wa michezo na tano, kutenga fedha kwa ajili ya mikopo ya wafanyabiashara wadogo wadogo.

Sita, kutenga fedha kwa ajili ya *exports guarantee,* saba, kutenga fedha kwa ajili ya tahadhari ya njaa, nane, kujenga mfuko wa kusomesha vijana tisa, mishahara kuongezwa, kumi, watendaji wa vijiji kulipwa, kumi na moja, kutenga fedha kwa ajili ya mahusiano yetu na Zanzibar ile 4.5, kumi na mbili, ujenzi wa barabara kwa kutumia fedha zetu za ndani bilioni 44 sio za msaada hizi ni za kwetu za ndani, kumi na tatu, kulipa mafao ya watumishi waliotokana na mashirika yaliyobinafsishwa na kumi na nne, kujenga ukumbi wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi na tano, kutenga Bajeti kwa ajili ya kusaka majambazi, kumi na sita, kushughulikia rushwa na kumi na saba, kuongeza kiwango cha pensheni. Sasa hapa wewe unataka Serikali gani na unataka Serikali ifanye nini katika hili? Sasa tunadhihirisha kwamba Maprofesa wanaomshauri Rais Benjamin Mkapa, wapo na Chama cha Mapinduzi kinafanya kazi, tunamshukuru Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nisingependa nichangie kwa utamu na uzuri wa Bajeti hii, lakini yale nitakayozungumza ni kwa ajili ya kuboresha na sio kwa ajili ya kupinga hatua zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na eneo ambalo nimemaliza nalo kule kutenga fedha kwa ajili ya kuwalipa wazee *(Pension)*. Katika Kikao chetu cha Kumi ambacho kilifanyika mwezi Machi, wakati tunachangia Muswada wa Kubadilisha Sheria Mbalimbali, niliiomba Serikali waangalie vima vya chini vya pensheni, nashukuru sana Serikali kwa kutekeleza hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda katika kuboresha, nilitamka kabisa kwamba shilingi 10,000 au shilingi 12,000 zilizokuwa zinalipwa kule nyuma ni ndogo sana, tunaomba ziongezwe na bahati nzuri

Serikali imeongeza sasa imefikia shilingi 20,000. Bado ninaamini fedha hizo ni ndogo, lakini heri nusu shari, kuliko shari kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ili kumsaidia mzee kuna masuala ambayo ni kero na yaangaliwe mfano suala la matibabu kwa wazee. Suala hili limetolewa maelekezo na Serikali lakini halijatengewa utaratibu unaoeleweka. Wazee ni kama watoto wanashikwa na magonjwa ambayo kwa kweli inabidi mtu awasaidie kwa mfano ugonjwa wa kisukari. Dawa za ugonjwa wa kisukari ni ghali sana wako wazee wengi wanahangaika sana. Sasa Serikali ni lazima itenge fedha rasmi kwa ajili ya mfuko kusaidia wazee. Pia suala la magonjwa sugu, ni vizuri Wizara ya Afya iyataje na wazee wasaidiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu kingine ambacho ninapenda kuchangia na kimesemwa vizuri, ukuaji wa sekta binafsi na uwekezaji katika nchi yetu. Suala la kukuza wazawa, mimi sitaki kuli-*over emphasis* lakini nilishasema tusipokuwa na uhakika na tusipochukua hatua za tahadhari katika kujenga uwezo wa Watanzania kumiliki uchumi kwa kweli tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana kwa sababu siku za usoni tutayumba sana.

Kwa hiyo, mimi nasisitiza kama Waziri alivyotamka katika suala hili la kuwasaidia Watanzania kwamba kupitia *UNIDO* kuna fedha ambazo zimetolewa kuwajengea uwezo Watanzania ili waweze kukopa na kusaidiwa kifedha ili waweze kuwekeza. Mimi nashauri sana elimu kwa Watanzania ambao watakuwa na haki ya kupata mikopo hii ni muhimu sana na hii mifuko na taratibu hizi zitangazwe zaidi ili Watanzania wengi wanufaike.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, atusaidie sana katika suala hili la mikopo kwa shughuli ndogo ndogo za *micro-finance* au *micro-credit schemes* ni muhimu sana kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ni muhimu sana na limetajwa katika hotuba hii ni suala la kilimo. Napenda kuipongeza Serikali kwa hatua zilizochukuliwa kwanza kwa kutenga fedha kwa ajili ya mazao na kutenga Mikoa ambayo inatakiwa ilishe nchi hii.

Napenda kusema kwamba suala hili ni zuri sana lakini pengine tuangalie katika kila Wilaya yale mazao yatakayotengwa yawe yamefanyiwa utafiti wa kutosha na kwa kweli yawe ni mazao ambayo tukiwekeza tutavuna. Hii ina maana kwamba tusiweke fedha zetu katika mazao ambayo hatuna uhakika kupata mazao ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa upande wa Jimbo langu la Lushoto, ni wakulima wa mbogamboga na matunda, usindikaji ni kitu muhimu sana Serikali itusaidie sana katika suala la usindikaji. Kwa sasa hivi tumepiga hatua ndogo sana. Naamini *Value Added* katika suala la mazao ndilo litakalokomboa nchi hii. Kwa hiyo, kuainisha uwekezaji katika viwanda na usindikaji wa mazao yetu, tusipoufanyia mchezo nina hakika tutaokoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda kuchangia ni Serikali kuendeleza na kurekebisha mishahara. Limetajwa hili lakini kwa bahati mbaya haijatajwa rasmi ni kiasi gani kitaongezwa. Naishukuru sana Serikali katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli sasa hivi maisha ni magumu sana kwa wafanyakazi wetu na si kwa wafanyakazi tu lakini katika maeneo mengi hali imekuwa ngumu sana. Pengine Serikali pamoja na kuongeza mishahara lakini iangalie pia wafanyakazi ambao wako katika sekta binafsi. Wafanyakazi wengi wanalipwa mishahara midogo sana. Kima cha chini katika sekta binafsi bado hakijazingatiwa. Mfanyakazi analipwa shilingi 1,000 kwa siku tena zile siku za kazi tu kwa hiyo kwa mwezi atakuwa analipwa shilingi 26,000 au 27,000. Kiwango hicho ni kidogo sana. Naomba Serikali iangalie suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la kushuka kwa thamani ya fedha yetu. Lipo tatizo la kushuka kwa thamani ya fedha yetu na hii ni kero kubwa ambayo inafanya maisha yawe magumu sana. Sababu kubwa ambazo zinafanya fedha yetu ishuke thamani kwanza ni udhibiti ambao sio mzuri katika hizi Benki zinazoitwa *Bureau de change* udhibiti ni mdogo sana. Ukienda kule unabadilisha fedha kama unabadilisha njugu katika duka hakuna maandishi hakuna udhibiti. Leo nchi ambazo zimeendelea sana kiuchumi huwezi kununua fedha kienyeji.

Ukienda Afrika Kusini sio rahisi kutoa fedha hapa kwetu unakwenda unanunua fedha kama njugu. Sasa unategemea vipi uchumi ukue? Kwa kweli tundu hili ambalo linaleta matatizo katika nchi yetu lazima lidhibitiwe. Kwa hiyo, nashauri maduka ya fedha za kigeni yadhibitiwe kama vile Benki zinavyodhibitiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *exports drive* bado ni ndogo. Nchi nyingine kama India unapouza bidhaa nchi za nje unapewa *export guarantee* au *export drive* ya *almost* 25%. Kwa mfano leo madawa ya kutoka India ni rahisi lakini ni rahisi kutokana na kwamba unapo-*export* India unapewa *export rebate* ya *almost* 25%. Nafikiri nchi haiwezi kuendelea kama hatuwezi kukuza uwezo wa fedha za kigeni ndio maana utaona kwamba uchumi wetu ni *cosmetic* bado hatuna fedha za kutosha za kutoka nje kwa hiyo, tunajiona kwamba tunajenga ndio lakini fedha nyingi zinazozunguka ni za wafadhili sio za kwetu wenyewe.

Kwa hiyo, *unless* kwanza tunaziba mianya inayotorosha fedha halafu tuwe na *deliberate policy* ya kuhakikisha kwamba mtu anaye-*export* kwetu sisi ni Mungu mdogo. Tukishafanya hayo nina hakika tutajenga uwezo wa ndani na tutakuwa na fedha za kigeni na nina uhakika hata suala la kushuka kwa thamani ya fedha litapungua na uchumi wa ndani utajengeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kushukuru kazi nzuri iliyotendwa na Mawaziri wote, mchango wangu ni kwamba juhudi hizi na fikra hizi ziendelee. Mwaka huu tumeondoa kero 16 ninaamini mwaka kesho tutaondoa pengine 16, tena mwaka 2005 tutakuwa tumemaliza kazi, wenzetu waangalie tu, ahsanteni sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunitambua na vile vile kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja zote mbili zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Wabunge wapya wote kwa ujumla wao kwa kufanikiwa kuingia kwenye Bunge hili Tukufu na hasa wale Wabunge wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nawapongeza Mawaziri wote, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri zenye mwelekeo. Naipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwasilisha Bajeti mwanana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Mbeya na nchi nzima wamefurahi sana na wamenipigia simu kutoka Mbalizi, Igoma wakisifia Bajeti hii hasa kwa kuondoa Kodi ya Maendeleo na kodi nyingine mbalimbali zaidi ya 58. Simu ya mwisho niliyopata inasema kwamba Wapinzani wengi wanarudisha kadi wanaingia CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naipongeza Serikali kwa kutambua kwamba kutoa ruzuku kwenye pembejeo kutaongeza kilimo kwenye chakula katika Mikoa ya Iringa, Ruvuma, Mbeya na Rukwa. Tunawaahidi kwamba sisi wa nyanda za juu Kusini tupeni hizi pembejeo tutawapa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maeneo machache ambayo nayafahamu vizuri ili niweze kuboresha Bajeti hii.

Kwanza nije kwenye mchango wa madini kwenye Pato la Taifa. Naungana na wenzangu kwamba mchango wake ni kidogo sana na matatizo ni Mikataba tuliyonayo. Kwanza labda nisahihishe neno moja tu ambalo linatumiwa hapa ndani ya Bunge, hakuna neno mrahaba kwenye Kiswahili, Kiswahili sanifu ni mrabaha, naomba mwangalie kwenye Kamusi zenu. Watu wote naona wanasema mrahaba, mrahaba nadhani hicho ni Kisukuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mrabaha au *royalty* ya asilimia tatu ni ndogo sana. Namshauri Waziri wa Madini na Waziri wa Fedha, kaeni mpange *royalty* mpya, mrahaba mpya. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mbona wewe mwenyewe unasema mrahaba?

**MHE. YETE S. MWALYEGO:** Mrabaha mpya. Unajua mazoea tena. Napendekeza asilimia kumi ili tuweze kuongeza pato la Taifa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mafuta kuna kitu kinaitwa *production sharing* lakini kwenye madini hatuna *production sharing.* Ni muhimu sana tukasema kwamba walipe kodi kutokana na faida wanayopata, siyo kusamehewa kodi. Kwa hiyo, mrabaha, halafu kodi, hapo utakuwa umeongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu kodi ya mafuta ya *petrol*. Mpango ule ulioletwa na Mheshimiwa Waziri ni mzuri hasa kuweka *flow meter* na napendekeza Tanga nako kuwe na *flow meter*, Musoma, Mwanza na Kemondo, kote kuwe na *flow meter.* Pia kwenye *debonding* kufuta *debonding,* hiyo ndiyo ilikuwa inafanya udanganyifu mkubwa sana na kama watalipa kodi wote, mafuta yanayoingia nchini na mafuta ya *transit* kwa kweli kutaongeza pato kwenye mafuta kwa zaidi ya asilimia arobaini kwa sababu udanganyifu ulikuwa mkubwa sana. Pia nilikuwa naomba tusije tukaingia kwenye mtego kwa kwenda kupima kwenye matanki yao badala ya kupima kwenye *flow meter.* Tunachokubaliana ni *flow meter* na *invoice* inatoka pale kwenye *flow meter.* Kama wana wasiwasi basi waje kwenye *flow meter* tuifanyie marekebisho, *calibration* na kila kitu, lakini tusikubali kwenda kwenye matanki kwa sababu hapo ndiyo unaingia kwenye mwanya wa rushwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ninaloliona ni *Tax Administration,* siku 15 hazitoshi kabisa. Kwa mafuta ambayo yapo kwenye *bond* sasa hivi kwa siku kumi na tano ni sawa, lakini kwa mafuta mapya yanayoingia kwa sababu inachukua karibu siku kumi na nne kuyasambaza halafu kukusanya fedha. Kwa hiyo, utakuta unaposema siku 15 alipie, lazima atakwenda benki akope kama hana basi ndiyo amekufa kibiashara hasa kampuni ndogo na tunge-*encourage* ili hizi kampuni ndogo wawepo kwenye *business.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba wapewe *grace period* ya siku 20. Wakishaingiza mafuta ndiyo anatoa *one third* ya *invoice,* siku 30 anatoa *another third,* siku ya 40 anamalizia na unafungua *ledger card* tu kwa kila mzigo unaoingia, kuna kampuni zinaingiza mzigo mmoja tu wa meli kila mwezi.

Kwa hiyo, siyo vigumu ku-*administer,* ukifanya siku 15 wataanza kuleta vi-*parcel* vidogo, kwa hiyo, mafuta yatapanda bei kwa sababu za kulipia *allege* ya meli na vile vile kutakuwa na ukosefu wa mafuta nchi nzima. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hili suala la siku 15 mliangalie upya. Haitawezekana na ni kwamba utaua makampuni madogo na utasababisha upungufu wa mafuta ndani ya nchi na hutapata chochote cha zaidi, lakini ukifanya *administration* nzuri zaidi fedha za Serikali zitakuja tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mafuta ya taa, wananchi wengi tunatumia mafuta ya taa kule Vijijini na mafuta ya taa bei ni kubwa na mengi yanatoka Kenya au Malawi, kwa hiyo, wananchi wetu wanalipa kodi za Malawi na Kenya. Sasa inakadiriwa kama asilimia 40 ya mafuta ya taa yanatoka nchi jirani na ina maana hizo kodi tunalipia nchi jirani. Najua tunaogopa kuchanganya mafuta ya taa na *diesel* au *petrol* ukipunguza bei, lakini kuna *bio-code* ambayo mtu akichanganya anaonekana mara moja na kuna *bio-coding* ya sasa hivi ukichanganya rangi inabadilika. Kwa hiyo, ni masuala tu ya wataalam waliangalie hili suala upya lakini tupunguze kodi kwenye mafuta ya taa ili wananchi wengi waweze kutumia. Hii ni kero mojawapo ambayo nadhani tumeisahau. Sasa hivi kodi ni kama shilingi 60 kwa kila lita nayo ni juu mno. Kenya bei zao zipo chini na ndiyo maana mafuta yanakwenda kuchukuliwa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *LPG* yaani gesi ya kupikia hii inatumika sana Mijini na ili tuondokane na *deforesratation* ni muhimu sana na naipongeza Serikali kupunguza kodi kwenye *LPG.* Lakini watumiaji kwa sasa hivi ni kama 4,000 hapa Tanzania na tungependa labda wafike 50,000 mpaka 100,000 ili tuweze kuwa na matumizi makubwa zaidi.

Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza au kufuta kodi kwenye majiko ya gesi na matanki ya gesi mbali ya gesi yenyewe kwa sababu unapotaka ku-*encourage* matumizi lazima uende kwenye matanki yake na majiko yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza kodi kwenye simu za mkononi mpaka asilimia 7. Gharama za simu Tanzania zipo juu kuliko nchi yoyote hapa duniani halafu tena tunaongeza asilimia 7. Mimi nipo kwenye Kamati ya Miundombinu na nalifahamu hili, naomba sana Serikali iliangalie. Sasa hivi watumiaji wa simu za mkononi wanakaribia karibu milioni moja na uki-*maintain* ile *five percent* ukafuta kodi za uingizaji wa *handset* kama *walkie talkie* utaongeza watumiaji kwa sababu gharama kubwa ipo kwenye kununua ile *handset*.

Kwa hiyo, utaongeza watumiaji na utaongeza Pato la Taifa, kwa hiyo siyo kuongeza kodi ndiyo unaweza kuongeza Pato la Taifa, *actually* kwa kupunguza kodi fulani unaongeza watumiaji wengi zaidi ile *economics of scale* kunakuwa na watumiaji wengi tunapata fedha nyingi zaidi na hili linatumika sehemu nyingi na ndiyo namna ya kupata fedha nyingi zaidi na kukuza uchumi wa nchi.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Serikali iliangalie hili upya na kwa sababu Serikali ya Chama cha Mapinduzi inasikiliza mawazo ya wananchi, nina imani kabisa wataliangalia hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lingeweza kuongeza mapato ya Serikali ni kwenye ukaguzi wa magari kila mwaka. Baada ya kuondoa kodi za baiskeli, mikokoteni na hizi kodi mbovu mbovu tuweke kodi kwenye mashangingi. Kila mwaka tulipie mashangingi yetu, magari yalipiwe kodi kila mwaka wakati wa ukaguzi na kuwe na sheria kabisa iletwe hapa Bungeni na ni fedha nyingi sana, ukifanya shilingi 10,000 kila gari utapata fedha nyingi kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na wenzangu kwamba Serikali iangalie upya suala la kodi kwenye chandarua na dawa za mbu. Kwa kweli tumefanya yote mazuri, ni sawa na mtu amevaa suti halafu ana kandambili hii inatuharibia Bajeti yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni hili la *VAT*. *VAT compliance* yake ni ndogo sana kwa sababu *rate* ipo juu. Wenzetu nchi jirani wanateremsha sisi bado tupo kwenye asilimia 20. Kwa hiyo, naomba *benchmark* yetu iwe ni Afrika Mashariki kwa maana ya Kenya na Uganda, tujaribu kwenda na wakati tuwe *around* 15% or 16%, *should be reasonable*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale Wapinzani nilikuwa naomba waungane na Chama cha Mapinduzi kuunga mkono Bajeti hii na vile vile kuondoa kero za wananchi zote zile, ndiyo sera ya Chama cha Mapinduzi na ndiyo Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero ya mwisho ambayo naiona mimi ni kufanya elimu ya shule ya sekondari iwe bure siyo kwa mwaka huu hata kwa mwaka kesho ili tujitayarishe kwa mwaka 2005 vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuweza kuniona ili niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na ya Mheshimiwa Basil Mramba, Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya ambao wameingia katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Karibuni tufanye kazi ya kuwahudumia Watanzania.

Pili, niwapongeze kwa dhati kabisa Waheshimiwa Mawaziri wawili kwa mikakati ambayo ni muafaka kabisa iliyojitokeza katika Mipango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka ujao wa 2003/04. Pongezi hizi zinazingatia hasa katika kuondoa kodi ya maendeleo, kodi za kero na kutambua umuhimu wa sekta binafsi kama ndiyo mhimili mkuu wa kuendesha uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni hatua mahsusi kabisa ambazo zinafanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Hatua ambazo mimi nawashangaa sana wenzetu katika kona ile nyingine wanaobeza

mafanikio ambayo Serikali ya CCM inayafanya. Hii ni hatua mahsusi kabisa. Hatua nyingine ambayo naweza kuikumbuka na mpaka sasa tunaitekeleza ni kwa Serikali kufuta karo kwa shule za msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni hatua kubwa sana, wengine labda wanachukulia kama ni jambo la kawaida, lakini siyo la kawaida. Kwa sababu katika mazingira ya leo ya Tanzania hatujaweza kuwaandaa Watanzania kuweza kwa mfano kutekeleza kikamilifu masuala ya uzazi wa mpango na mambo kama hayo.

Kwa hiyo, kwa nini Taifa liwaadhibu hawa watoto ambao wanazaliwa Watanzania, ni lazima liwasomeshe. Kila mara huwa natoa mfano mmoja, huko Marekani, nadhani ilikuwa katika miaka ya mwanzoni mwa 1980. Sikumbuki tarehe hasa, lakini ilitokea siku moja katika Mji wa New York, umeme ulizimika kati ya saa tatu usiku na saa nane usiku. Baada ya miezi nane hadi tisa takwimu zilionyesha kwamba watoto waliokuja kuzaliwa walikuwa wengi sana katika Mji wa New York, sembuse Ikwiriri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote mimi napenda kurejea malengo mahsusi ya kukua kwa uchumi. Ukichukulia yale ambayo yamekuwepo kwa mfano kasi ya kukua kwa uchumi kwa mwaka 2003 inatarajiwa kuwa asilimia 6.3, mwaka 2004 6.6, mwaka 2005 asilimia 7.0, mwaka 2006 asilimia 7.4. Kwa wakati ule ule mapato ya Serikali kama sehemu ya Pato la Taifa na yenyewe yanakisiwa kuongezeka kwa asilimia 13.2 mwaka 2003/04, mwaka 2004/05 asilimia 13.5, mwaka 2005/06 asilimia 13.7. Hapo hapo kiwango cha kuwekeza raslimali ambapo mwaka jana 2002 ilikuwa asilimia 17.4 na hapa Waziri wa Mipango na Uwekezaji anasema ili tuweze kuwa na uchumi ambao unawezesha kwa ujumla lazima kukua kwa uwekezaji kuzidi asilimia 25.

Mimi nazidi kusema kwamba ni kweli ili uchumi uwe wa kuweza kuhimili matatizo yetu lazima ukue zaidi ya asilimia 10 na ili kuondoa utegemezi wa Bajeti yetu lazima iwe zaidi ya asilimia 20 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango hii mizuri iliyomo katika Bajeti ambayo kwa namna moja au nyingine inalenga katika haya masuala, lakini mimi nina wasiwasi kwamba haya malengo ya kukua kwa Pato la Taifa na kuongezeka kwa mapato yetu na uwekezaji wa raslimali hayana uhusiano wa moja kwa moja na matatizo au changamoto ambazo Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ameziainisha katika aya ya 85. Katika aya ile Mheshimiwa Waziri amesema matatizo yetu ya msingi ya uchumi wetu ni pamoja na yafuatayo:-

- Bajeti tegemezi;
- Umaskini Vijijini na Mijini;
- Utamaduni mdogo wa kuweka akiba;
- Uwekezaji mdogo wa raslimali;
- Ukosefu wa ajira;
- Miundombinu hafifu; na
- Huduma duni za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka niwaulize Waheshimiwa Mawaziri kwa pamoja kwamba kwa makisio hayo ya kukua kwa uchumi na kasi ya ongezeko la uwekezaji wa raslimali hizi changamoto tutakuja kuzikamilisha lini? Maana inaelekea hata mwisho wa mwongo huu tutakuwa hatujafikia hata asilimia 10 ya Pato la Taifa. Sasa kweli tutaondoa huu umaskini? Mimi naomba sana Waheshimiwa Mawaziri muweze kutueleza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kuzungumzia ni kuhusu suala la matengenezo ya barabara ambalo linahusiana pia na hili la Bajeti tegemezi na ya kujikwamua kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kahama wamenituma nitoe pendekezo lifuatalo ambalo wametoa wenyewe, kwamba kwa kuwa kumekuwa na mafanikio makubwa sana katika mpango wa maendeleo ya elimu ya msingi katika matengenezo ya madarasa, tumejenga madarasa mengi sana ya shule za msingi, tumejenga nyumba za walimu, sasa hivi tunaendelea na ofisi na kadhalika kwa kutumia fedha za Serikali Kuu na kwa kutumia michango ya wananchi. Hili tumekuwa na mafanikio makubwa sana.

Wananchi wa Jimbo la Kahama wanapendekeza hivi kwamba Serikali ifikirie sasa kwamba katika matengenezo ya barabara za huko Vijijini, barabara za Halmashauri kwa kiwango kikubwa nguvu za wananchi zitumike badala ya makandarasi ambao wanatumia fedha nyingi lakini matengenezo siyo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili wanasema kwamba, kwanza tutapunguza gharama ama hayo matumizi ya fedha, lakini *impact* itakayotokea itakuwa ni kubwa zaidi. Lakini pia itaimarisha hii dhana ya umiliki wa maendeleo yao kwa sababu sasa hivi barabara zinajengwa lakini fedha nyingi hazionyeshi kwamba matengenezo makubwa yamefanyika. Lakini wakisimamia wenyewe fedha hizi za Mfuko wa Barabara kwa kuwa matengenezo makubwa ni ya kuweka tu taa, kufyeka kando kando ya barabara na kuchimba mifereji ya maji basi wananchi watumike na walipwe fedha kidogo za kuwawezesha kununua mafuta na mambo kama hayo, badala ya sasa ambapo fedha nyingi zinatumika kwa makandarasi. Hilo ni la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo wananchi wa Kahama wamenituma nizungumzie ni kutoa shukrani kubwa na za dhati sana kwa Serikali ya CCM kwa hatua ambayo inafanya sasa hivi kwa kuimarisha ulinzi na usalama katika nchi yetu hususan katika Wilaya ya Kahama. Kwa kipindi kirefu sana hapo katikati kulikuwa na wimbi la ujambazi kweli kweli na wananchi walikuwa wameanza kukata tamaa. Lakini sasa hivi mambo yanafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mambo yanayofanywa na Serikali ya CCM. Sasa hawa wenzetu wanaobeza hayo matokeo mimi nawashangaa sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo hiyo naomba sana kwamba kwa kuongeza Bajeti ya ulinzi na usalama kwa mwaka unaokuja Serikali itupie macho sana katika Wilaya ya Kahama ambayo ipo pembezoni mwa nchi yetu, wageni wanakuja pengine na silaha, ni Wilaya mojawapo ambayo uchumi wake unachangamka sana na mzunguko wa fedha ni mkubwa. Kwa hiyo, tunaomba sana raslimali nyingi zitakazotolewa ziende kwenye Halmashauri ya Wilaya yetu ya Kahama kwenda kuimarisha ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nizungumzie hili la kuboresha pensheni. Natoa shukrani kwani na mimi ni mstaafu, kwa hiyo, kwa namna moja au nyingine nategemea kwamba na mimi nitafaidika. Lakini lipo kundi moja la wastaafu wale ambao walichukua fedha zao au mafao yao kwa mkupuo. Katika mazingira haya ambapo wale ambao hawakufanya vile wanaendelea kulipwa kwa miezi sita, sita, wanaboreshewa mafao yao, naomba kwamba wale waliochukua mafao kwa mkupuo, tusiwaache kana kwamba wenyewe siyo Watanzania. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba Bunge lako Tukufu liweze kufikiria kurekebisha vifungu vinavyohusika vya sheria ili hawa nao waweze kuingizwa katika mafao hayo yanayoboreshwa na wenyewe waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa na mimi tu niseme kwamba ninaunga mkono kwa dhati kabisa mapendekezo yaliyotolewa na Wabunge kwamba vifungu vya sheria na Mikataba inayohusiana na mapato yanayotokana na madini yarekebishwe.

Mimi natoka katika Wilaya ambayo tuna machimbo ya dhahabu hasa katika huu mgodi mkubwa wa *Kahama Gold Mining Corporation*. Kwa kweli kinachopatikana ni kikubwa, lakini yale mazingira yaliyopelekea mpaka haya mambo yakawa yalivyo siyo mazuri kabisa kwetu sisi. Wilaya ambazo zinahusika pamoja na kwamba hayo makampuni yamejisifu yametoa misaada na kadhalika lakini ule utaratibu siyo *institutionalize*. Tunapata fedha au mapato kutoka katika haya makampuni kwa njia na taratibu za fadhila, sisi hatutaki fadhila. Tunataka utaratibu uwe *institutionalized* na uwe *more predictable* tuweze kujua kiasi gani kinapatikana, kwa wakati gani na kadhalika

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hata katika kufikia maamuzi ya ushirikiano kati ya makampuni haya ya madini na wananchi husika katika maeneo, hili liliachiwa tu eti wafanye hao walioko huko. Hii haiwezekani hata kidogo! Haya makampuni ni ya Kimataifa, yamekubuhu katika masuala ya *International Laws, Laws of Contract,* lakini huyu mwananchi wa Kahama kule Kijijini Kakola, unamwekea hayo makampuni unasema kwamba wakubaliane. Haiwezekani hata kidogo. Katika ulimwengu huu wa

utandawazi lazima kweli turejee baadhi ya maamuzi yetu tuliyofanya huko nyuma ili tuweze kuboresha maslahi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hotuba zote mbili mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

nikipongeze Chama cha Mapinduzi na mgombea wake Mheshimiwa Edward Ndeka, kwa kuweza kulirudisha Jimbo la Kigoma Kusini katika himaya ya Chama cha Mapinduzi. Nampa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwapongeze Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao ambazo wamezitoa na kwa kweli zenye mwelekeo wa kila hali ya kumwondolea kero mwananchi wa kawaida na kumwezesha kuondoa umaskini, nawapongeza sana.

Niseme tu kwamba moja kwa moja naunga mkono kwa asilimia mia moja hotuba zilizotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Bajeti iliyotolewa ni nzuri sana ni ya kumkomboa Mtanzania na kumwondolea kero. Kinachotakiwa ni azma ya utekelezaji ili tuweze kufikia malengo yaliyoainishwa katika Bajeti. Mara nyingi tumekuwa tukipata visingizio kutoka kwa watendaji kuwa walikuwa hawaelewi taratibu, walikuwa wageni, walikuwa hawajui sheria na hii imepelekea hata fedha za maendeleo kutotumika. Sasa unapokuwa hukutumia fedha za maendeleo ni kwamba kwa kweli unakuwa umewakosesha haki wananchi ambao walitakiwa kutumia hizo fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti hii tusikubali kuwa na visingizio ambavyo vitapelekea kutotekeleza yale yaliyoainishwa katika Bajeti. Wale ambao hawawezi na wale ambao hawafundishiki waondolewe ili wenye uwezo waweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa kilimo katika uchumi wetu kwamba kilimo kinabeba zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wetu na kinachangia zaidi ya asilimia 50 ya mapato yetu ya Taifa. Lakini bila kubeza kwa kweli Wizara nyingine au sekta nyingine kwa umuhimu huu wa kilimo Bajeti ya kilimo ilitakiwa iwe kubwa sana kukifanya kilimo iwe ndiyo Sekta Kiongozi katika uchumi wetu, kwa kutambua tu hizi takwimu mbili.

Naipongeza Serikali kwamba imeongeza, lakini ukiangalia imeongeza shilingi bilioni 6 tu kutoka kwenye Bajeti ya mwaka 2002 na kwa kuwa sekta hii ni Sekta Kiongozi haitoshi. Sisemi kwamba sekta nyingine si muhimu, lakini kwa kuwa ni Sekta Kiongozi ilitakiwa ipewe umuhimu unaostahili. Ukiangalia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, imeongezwa shilingi bilioni 15, ukiangalia Utawala Bora imeongezewa bilioni nyingine kama 4. Sasa ni vyema tukatambua umuhimu wa sekta hii kwamba ni Sekta Kiongozi na tukaiongezea fedha zinazostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuzungumzia kilimo kama hakuzungumzia umwagiliaji, kutegemea mvua za bahati tutakuwa hatufiki popote katika hili. Najua kama Serikali tuna *Irrigation Master Plan,* mkakati wa Kitaifa kabisa wa umwagiliaji. Lakini tukiangalia mpaka hivi sasa ni kwa kiwango gani tumetekeleza huu mkakati wa umwagiliaji wa Kitaifa. Miaka ya 1980 mimi nilikuwa nikienda *ADB* kutafuta mikopo kila siku tunaandamana na watu wa *Madibira Rice Project, Kapunga Rice Farms, Mbarali Rice Project* na nyingine nyingi. Leo hizi tumezitumia kwa kiwango gani? Leo *RUBADA* inatumika kwa kiwango gani kuweza kuzalisha *in quality,* leo *Kagera Basin* inatumika kwa kiwango gani kwa malengo yaliyokuwa yamekusudiwa awali kwa ajili ya kuongeza kilimo na chakula katika nchi yetu?

Kwa kweli ili tuweze kujikwamua kilimo chetu lazima kiwe cha kisasa cha umwagiliaji mkubwa na mdogo ili kuweza kuzalisha chakula tunachokihitaji. Na mimi naungana na wenzangu kuipongeza Serikali kwa kutoa ruzuku ya pembejeo kwa Mikoa hii 4. Lakini Bunge lako Tukufu lingependa kujua je, huu ni utaratibu wa zimamoto tu kwa sababu mwaka huu tuna njaa au ni utaratibu wa kudumu? Kama ni wa kudumu ni kiasi gani cha fedha zitakuwa zimetengwa kwa ajili ya shughuli hii, ili tuwe na uhakika kwamba huu mpango ambao tunaanzisha ni mpango endelevu kwa wananchi wetu na kwa nchi yetu.

Lakini pia tungependa kufahamu hivi ni nani anayepewa hili jukumu la kuzileta hizi pembejeo? Je, zitafika kwa wakati au zitachelewa au tutapata hadithi tena kama ile ya mbegu za pamba zilizopelekwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni muhimu ili tujiweke sawa katika kukabiliana na hali halisi ya njaa. Nalizungumza hili kwa sababu kama utakuwa ni utaratibu wa kuganga njaa hii tuliyonayo, mpango mzima hautakuwa endelevu na tutakachokuwa tumekifanya tutakuwa tumeifanya Mikoa hii kuzalisha zaidi, lakini hii ni biashara huru. Hivi mtu wa Rukwa akizalisha mahindi ana sababu gani ya kuuzia *SGR* badala ya kupeleka Kongo ambapo mahindi yana bei kubwa zaidi. Tuna uhakika gani kwamba hiki chakula kitakachozalishwa kinabaki ndani ya nchi hii na tuna uhakika gani kama hatutaweka vizuizi kumzuia kwamba hicho chakula kibaki ndani ya nchi hii. Sasa ni mambo ya kuangalia kwamba tuweke mikakati ambayo inatekelezeka na iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi Mikoa hii 4 yote imetumia mbolea kwa muda mrefu sana na kwa kweli ardhi yake imechoka bila kutumia mbolea huwezi kupata chochote. Lakini kama tutakuwa na nia ya kuuza nje, wanunuzi wengi siku hizi wanapenda mazao ambayo hayakutumia mbolea za kemikali na hii si kwa mahindi tu au kwa maharage ni hata kahawa na mazao ambayo hayakuwekwa kemikali yana bei kubwa zaidi kwenye soko kuliko hivi ambavyo tunakazania kuongeza mbolea.

Sasa lazima tulione hili na tuweze kuchukua maeneo mengine ambayo si lazima kutumia mbolea na sisi kama Serikali tuyape umuhimu na katika hili napendekeza Mkoa wa Kigoma uingizwe katika hii programu, kwa sababu Kigoma tuna mvua za kutosha, Kigoma unaweza kupanda ukapata mazao bila kutumia mbolea mpaka hivi sasa. Lakini tuna mabonde makubwa likiwemo Bonde la Mto Luiche ni kubwa na halijawahi kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuna soko la uhakika ukizalisha mazao katika Mkoa wa Kigoma ni kwamba una soko la uhakika majirani zetu wa Kongo na Burundi kila siku wako vitani hawana muda wa kuzalisha, kwa hiyo tukizalisha mazao katika Mkoa wa Kigoma tunakuwa na hakika ya soko kwa yale tunayoyazalisha. Lakini pia kwa sababu *Kigoma is a sleeping giant* haijawahi kutumiwa, itakuwa ni njia moja ya kuweza kuendeleza Mkoa huu ambao kwa kweli ukiangalia umesahauliwa kwa muda mrefu.

Mimi naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, atapokuwa anazungumzia sekta yake kwamba tusizungumzie hii Mikoa 4 tu, tuangalie na Mikoa mingine yenye *potential* ya kuweza kuzalisha mazao ya chakula na Kigoma ni mojawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwa na Benki ya Wakulima, nafikiri hili jambo limepigiwa kelele sana na Waheshimiwa Wabunge na kwa kweli limechelewa. Lakini ili tusi-*duplicate* mambo, mimi nina hakika hii benki itakayoanzishwa itaanzishwa kwa mtaji wa Serikali na itaendelea kuendeshwa na Serikali. Sasa kwa nini basi tusitumie benki ya Serikali ambayo tunayo *NMB* badala ya kuanzisha Benki nyingine mpya? Tutakachokihitaji ni kuweka *a window special for farmers,* halafu inaendelea benki kama kawaida kuliko kuanza ku-*duplicate.*

Katika hili tutakuwa kwanza tumeiendeleza *NMB,* pili tutakuwa tumeondokana na malumbano yaliyopo ya kubinafsisha *NMB,* lakini tatu azma ya Chama cha Mapinduzi *political mission* ya kufikisha huduma za kibenki huko kwa wanavijiji itakuwa imefikiwa na itakuwa ni *credit* kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu tulizonazo kila siku watoto 110 nchini hapa wanakufa kwa sababu ya ugonjwa wa Malaria, hii si namba ndogo. Sasa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amependekeza kuweka kodi kwenye vyandarua na dawa ya mbu, tutakuwa tuna *defeat purpose* nzima ya kupigana na Malaria katika nchi yetu.

Sasa mimi napendekeza kwamba hii kodi ambayo itatozwa kwenye vyandarua na dawa ya mbu iondolewe hapo, halafu kodi ambayo ilikuwa imefutwa kwenye *walkie talkie* ndiko itozwe pale kwa sababu *walkie talkies* wanatumia watu wachache na ni watu wenye uwezo wa kuweza kulipa kodi, kwa hiyo, walipe huko ili watoto wapate vyandarua na dawa ya mbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba tu niungane na angalizo ambalo amelitoa Mheshimiwa Lucas Selelii, leo asubuhi, kwamba baadhi ya Mikoa imekuwa haipati fedha za nje kwa miaka 4 mfululizo hivi sasa na hii ni hali ya hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitegemea kama tusipopata fedha za nje, sasa zile fedha za ndani kwamba zingeenda juu, lakini nazo zimeshuka na zimekuwa *stagnant* sasa haya maelezo ya kwamba wafadhili hawataki kwenda huko, kwa kweli itafika mahali tuanze kukataa kuyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wafadhili hawawezi kwenda kama hawakuambiwa waende huko na kama hakuna miundombinu ambayo inawavutia hawawezi kwenda huko, miundombinu ni kazi ya Serikali kuipeleka huko si ya mwekezaji kwenda kuanza kuweka miundombinu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoomba niwaombe Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kwamba waweke juhudi za makusudi kabisa kuelekeza hawa wafadhili waingie katika Mikoa hiyo ambayo haina wafadhili ukiwemo Mkoa wa Kigoma ili na wao waweze kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tusipokuwa na umeme wa uhakika Kigoma, tusipokuwa na barabara ya uhakika ya kutoka Kigoma kuja Tabora na tusipokuwa na mawasiliano yaliyo imara hakuna mwekezaji atakayekwenda huko.

Sasa ninachoomba ni kwamba Serikali kwa makusudi kabisa iweke hii miundombinu. Maendeleo yana gharama zake na umeme tunaoutaka ni umeme wa kutoka mabonde ya Mto Malagarasi, Dola milioni 34 zinazozungumzwa si nyingi ukiangalia *potential* iliyopo Kigoma na nchi za jirani watakaokuja kuwekeza kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukishaibua Kigoma tayari wawekezaji na wasafirishaji kutoka Burundi na Kongo watakuja kupita Kigoma na Serikali itafaidika. Mizigo itakayokuwa inatoka Dar es Salaam itapita Kigoma kwenda kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeiomba Serikali kwa makusudi kabisa itoe kipaumbele katika kuendeleza Mkoa wa Kigoma kuibua *potential* ambayo iko katika Mkoa wa Kigoma na kwa namna hiyo ndiyo njia tu pekee ya kuweza kuwavutia wawekezaji ambao hawataki kwenda katika Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyu ndiye msemaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo na wakati wa kujadili Bunge umekwisha. Kuna mmoja wetu amesahau funguo zake za gari kwenye *pigeonhole* anapokwenda nje apite kwa askari atazikuta hizo funguo.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa.01.44 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne*
*Tarehe 17 Juni, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*